ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini na Saba – Tarehe 03 Agosti, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika,(Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa kazi nzuri sana ambayo mmeifanya jana, chini ya uongozi wa Mhe. Naibu Spika. Hiyo ni kawaida yenu kutoa mashirikiano makubwa katika kuendesha shughuli zetu, nawapongeza sana. *(Makofi).*

Lakini pili Waheshimiwa Wajumbe, tulipoakhirisha hoja hii wiki iliyopita, tulielekeza na mkafurahi sana kwamba Mhe. Waziri akajipange vizuri, lakini serikali kwa ujumla ifanye kazi juu ya jambo hili. Napenda kuwaarifu kwamba kwa taarifa niliyopata ya awali serikali imejipanga vizuri juu ya jambo hili na wamekaa kitako juu ya hoja ambazo kwa heshima ya chombo hiki wameona kwamba walete majibu ambayo ni mazuri sana.

Nitakapowataja wale ambao watachangia, kama alivyosema hapa katibu majadiliano yanaendelea, basi nitaelewa kwamba kweli kazi kubwa

imefanyika. Kwa hivyo, kabla ya kumuita Mhe. Naibu Waziri ambaye ndiye tuliyeondokea juzi, baada ya yale maelekezo ambayo Waheshimiwa mliyafurahia tuliyoyatoa hapa, watakuja kwanza Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia atakuja Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, baadae atakuja Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Lakini isitoshe zaidi ya hivyo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pia atasema hapa, ili kuthibitisha kwamba serikali ilikaa na kuzingatia michango ya Waheshimiwa Wajumbe ambao waliitoa, na baadae tena tutamuita Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ili kufanya majumuisho. *(Makofi).*

Tukienda vizuri na kwa muda mfupi, siku ya kesho tulipanga kwamba imekaa kama *tentative*, tukifanya kazi vizuri leo, tukimaliza mapema na Mhe. Waziri ambaye tayari ameshaweka mezani hati yake, tukiweza kuwasilisha hiyo na Mwenyekiti wa Kamati akatoa maoni ya Kamati, pengine tukapata na Wajumbe wawili au watatu, basi kesho kwa kweli tupumzike, itakuwa kazi nzuri sana tumeshaifanya. Lakini hiyo inategemea nyinyi mtakavyosema, nawashukuru sana. Basi majadiliano yanaendelea. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na kutuwezesha kutupa afya na kutuwezesha kuwa katika kikao hiki leo. Naomba nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii, lakini naomba pia niwashukuru Wajumbe wa Baraza hili, kusema kweli kwa kufanya kazi nzuri ya kuichangia vizuri hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano.

Pia nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao. Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri pamoja na kwamba ametiwa kwenye wizara hii yenye mkondo mkubwa kweli kweli, lakini ni mchapa kazi hodari kweli kweli, yeye na Naibu wake, pamoja na watendaji wake. Sisi ndio tunafanya kazi nao, na tunawajua kwamba kusema kweli wanafanya kazi kwa juhudi zao zote.

Mimi Mhe. Spika, naomba nichangie katika maeneo kidogo sana nayo ni maeneo nadhani matatu tu.

Kwanza ilikuja hoja ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kujitoa katika Kampuni ya *AEROTECH*, lilizungumzwa sana na maelezo yakatolewa, lakini kwanza nitangulie mimi kuungana na wenzangu kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kusema kweli mageuzi aliyoyafanya pale Uwanja wa Ndege ni makubwa, kwenye sheria tunasema kuna mambo ambayo hayahitaji kuthibitishwa

ukiyaona utajua kwamba hapa pamefanyika kazi. Kwa hilo amejitahidi na naamini na Wajumbe wengi watakubaliana na sisi kwamba amefanya kazi kubwa. Lakini ukweli unabaki kwamba nchi yetu utamaduni wetu ni wa kiungwana, hata mtu maskini ukimpa shilingi milioni moja, na ikawa kwake hana hata senti tano, halafu ukamsimbulia basi atakurudishia hiyo shilingi milioni moja.

Mhe. Spika, maana yake nakusudia kwamba ukishafanya kazi nzuri, bado kunahitajika na mwenendo pia uendane na wale watu ambao unafanya kazi nao. Sasa hayo mapungufu mwenyewe Mkurugenzi Mkuu Mhe. Makamu hapa ni shahidi, serikali iliyaona na pia ikatupa kazi ya kukaa naye na kumueleza malalamiko haya, kabla ya haya kuzungumzwa hapa ndani ya Baraza na kazi hiyo ilifanyika, na mimi nilishiriki kwa sababu ilikuwa mfano tu, mmoja katika mtu ambaye alifanya kazi katika mazingira magumu mmoja ni mimi. Kuutoa uendeshaji wa mashtaka kutoka mikononi mwa polisi ukaja wa kiraia haikuwa kazi rahisi na ikanijengea uadui mkubwa, kwa sababu ni kawaida mabadiliko yoyote yana *resistance;* na ndio maana kuna taaluma maalum wanasema *change management*, namna ya kuongoza mageuzi. Sasa haya ni matokeo ya hayo, nadhani kadiri tunavyokwenda haya ni mapungufu ya kibinadamu na mtu anajifunza katika kazi, na kujifunza kuna namna mbali mbali, lakini niseme hatukulidharau, serikali ililiona zamani na tukalifanyia kazi zamani, na kila linapojitokeza naomba tushirikiane ili tulirekebishe.

Lakini suala la kujitoa alipolizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma siku ile katika bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati sisi hatukulidharau, naomba nimuhakikishie kwanza Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba hatukulidharau, tulilifanyia kazi na mimi binafsi kwa sababu ndio kazi hii niliyokabidhiwa, nililifanyia kazi nikatafuta nyaraka zote hizo alizozungumza yeye za kujitoa kwake za tarehe 24 Oktoba, nikaridhika kwamba kisheria kweli kajitoa, lakini na zile barua ambazo alizisoma humu ndani na mimi nilizipata kwa njia za kwangu mwenyewe, na nikathibitisha wasi wasi ule aliokuwa nao Mhe. Hamza Hassan.

Sasa mimi niseme tu kwamba ile ni kazi ambayo serikali yenyewe inaifanyia kazi. Kwa hivyo, kama limetokea la namna ile mimi naomba kwamba tusiichukulie ile kama ni ushahidi wa moja kwa moja, tuseme ni tuhuma bado tuachiwe tukazifanyie kazi kama tulivyozifanyia kazi hizi nyengine, naomba na zile pia tukazifanyie kazi.

Ninachoahidi kwa niaba ya serikali ni kwamba tukipata ushahidi wa namna hiyo, nina hakika kwamba serikali itachukua hatua, kwa sababu serikali ilieleza wazi kwamba uchague moja baina ya kazi au biashara. Haiwezekani ukafanya biashara katika eneo lile lile na hilo lilifanyika.

Kwa hivyo, mimi nikubaliane na Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba kuna tuhuma hizo, lakini hatukuzidharau tumezifanyia kazi na tutaendelea kuzifanyia kazi, kwa sababu bado ni tuhuma hatuwezi kuzichukulia kwamba ni *conclusive evidence*.

Suala jengine ni la wafanyakazi wa Shirika la Meli. Suala hili Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh Salmin naamini atakubaliana na mimi kwamba hata kabla hatujaingia humu Barazani tuliwahi kulizungumza, na alichokizungumza kina mantiki kweli kweli kwamba hili suala ni la muda mrefu, maana ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu ilitoa barua ya maelekezo tokea mwaka 2001 mpaka leo tuko mwaka 2013. Kama ingekuwa mtu anaidai ardhi, sheria ya ardhi unaambiwa mtu akiikalia miaka 12 kama hujamuuliza basi ile ardhi inakuwa ni ya kwake. Sasa seuze suala hili la kibarua na mafao. Mimi nimelipitia na nimepitia nyaraka zote, na namuomba sana Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba hili suala tusilijadili humu ndani, kwa sababu moja tu ya kuheshimu kanuni yetu ya 59 fasili ya 4, kwa sababu hili suala bado liko Mahakamani. Kuna ombi nambari 42 la mwaka 2013 ambalo limewasilishwa Mahakama ya Rufaa tarehe 22/03/2013, hii tunaita *notice of motion*.

Lakini pia kuna ombi jengine la kuzuia utekelezaji wa hukumu, ambalo lilipelekwa Mahakamani tarehe 12/06/2013 na limepangwa kutolewa maamuzi tarehe 19/08/2013. Kwa hivyo, naomba kwa kuheshimu kanuni zetu. Hoja iliyotolewa ina mantiki kwamba la muda mrefu, hiyo serikali yenyewe inaweza ikaongezeka gharama, zikaongezeka na hasara. Kwa hivyo, tutafute namna ya kulizungumza, lakini naomba kama nilivyosema kwamba ni vyema tuliache kwa sababu kanuni yenyewe imesema ni marufuku, ingesema hairuhusiwi tu haijambo, lakini imesema ni marufuku kulizungumza.

Jambo jengine la mwisho ni suala la *ground handling*. Mimi naomba niseme kidogo tu Mhe. Spika, kwamba kuna watu wanakuja kwenye chombo hiki kwa sababu nzuri kabisa za msingi, wameona kuna pahala pameharibika, wana haki zao na Wawakilishi ndio kazi yao kuwasemea, maana ndio chombo chao cha kuwasemea. Wala Wawakilishi kwa suala hilo wasijione wakasema aah! tumeambiwa tumekuwa mahakama, hamjawa mahakama ndio wajibu wa Wawakilishi kuwatetea wananchi wa nchi hii. *(Makofi).*

Lakini wapo wengine Mhe. Spika, ambao wanakuja kwa Wawakilishi wakidhani Wawakilishi wana uhasama na serikali, wapo wa namna hii. Hawa, mimi naomba Waheshimiwa tuwasaidie waelewe kwamba Wawakilishi au chombo hiki hakina uhasama na serikali, yanayosemwa humu kwa uchungu, kwa jazba na wakati mwengine kidogo kwa hamasa niseme hayo yote yanasemwa kwa nia ya kujenga. Ukitaka kuthibitisha kwamba chombo hiki

hakina uhasama na serikali, Mhe. Spika, ulipoingia jambo la mwanzo hapa tumeanza na dua, chombo hiki ndio peke yake kinachoiombea dua serikali kabla ya kujiombea yenyewe. Sasa mtu utamuombea dua halafu useme una uhasama naye. Ukifika hapa Mhe. Spika, unaanza dua ya kuiombea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kabla ya dua ya Baraza na sababu ya msingi ni kwamba serikali ni kama dereva.

Ukipanda gari ambayo inaendeshwa hata na mlevi basi utamuombea dua mufike salama, hutotaka gari ile iingie msituni. Unapomwambia unamwambia kwa kumuelekeza ili mfike salama, lakini wengine yale yakizungumzwa humu, wanadhani labda serikali tuna uhasama au Wajumbe wana uhasama na serikali, sio hivyo wala sio sahihi. Nadhani wanaokuja kwa Waheshimiwa kwa kudhani hivyo ni vizuri tuwasaidie.

Mhe. Spika, suala la *ground handling* hili halikuanza kwanza na *ground handling*, maana serikali kwanza kutaka kuona Uwanja wa ndege unafanya kazi imefanya mambo mengi. Imewekeza katika *runway* pesa nyingi, imewekeza katika *apron* pesa nyingi, imewekeza katika *terminal* pesa nyingi, imewekeza katika kuweka *institutional framework*, kuweka hiyo Mamlaka yenyewe haikuwekwa kumiliki Uwanja wa ndege, hapana, imewekwa kama ni chombo cha kuisaidia serikali kuendesha vizuri Uwanja wa ndege.

Ile *investment* ambayo imewekwa ni muhimu kwa uchumi wetu. Hata kabla Mamlaka kuanzishwa serikali ilikuwa katika majadiliano na kampuni ya Kituruki kwa ajili ya kufanya *Management* ya *Airport;* kwamba jamani tunawekeza katika *terminal*, tunawekeza mambo yote haya hatuwezi tukawa na *management* ya wasi wasi, lakini hatukukubaliana Kampuni ile, tumezungumza nayo zaidi ya miezi sita, hatukuafikiana, tukasema hapana masharti hayo hatuyawezi, tukaanzisha Mamlaka.

Sasa baadae ikaja kama ilivyo kawaida ya wawekezaji mbali mbali wanakuja. Walikuja wawekezaji wakataka kuwekeza Zanzibar katika maeneo mbali mbali. Moja walilotaka kuwekeza ni kujenga ghala hapa Zanzibar la kuuzia *spare parts* za ndege, wao ni wasambazaji wa *spare parts* za ndege wa kampuni kubwa ya Kimarekani ya Hanway; katika *distributor* wanne wao ni mmoja, na wakasema kwa Afrika tunataka tuifanye Zanzibar ndio *centre* yetu. Mtu yeyote tunaye-*deal* naye anayenunua *spare* Afrika azichukue kutoka Zanzibar, tupeni sehemu *preferable* katika eneo la Uwanja wa ndege tujenge kwa gharama zetu ili tuwekeze na miradi mingine mbali mbali sina haja ya kuizungumza hapa.

Lakini moja anasema kutokana na haiba ilivyo ya Uwanja wa ndege na hasa serikali yenyewe ndio iliyoanza kusema kwamba moja katika eneo lenye

tatizo ni kwamba Uwanja wa ndege wenyewe katika suala la *ground handling*, na katika eneo hili akasema sisi tuko tayari tunaweza ku-*mobilize* kitu tukakifanya ndani ya miezi miwili, na tuko tayari katika *package* hii hii, serikali itupe eneo tuwajengee *VIP lounge* ya kisasa ili kujenga haiba zaidi ya Uwanja wa ndege.

Kwa hivyo, na walivyokuja hawakuja kwa siri, walikuja ofisini kwa Makamu wa Pili wa Rais na mimi binafsi nilialikwa kama Mwenyekiti wa Kamati ile ya mapatano ya serikali. Mimi binafsi nikasema kwamba kwa utamaduni wetu tunasema *seeing is believing.* Kwa hivyo, hebu anzeni na mradi mmoja mdogo ambao tutapata *quick gain* watu waone uwezo wenu.

Kwa hivyo, hatimaye niseme serikali ikakubali kwamba hawa watu hii *package* yote wawezeshwe ili waweze kuifanya, ya ghala la *spare*, ya kujenga *VIP lounge*, ya *ground handling*. Kwa hivyo, hawa walioitwa ni ku-*facilitate* hiki kitu kifanyike na wakaelekezwa kwamba basi tayarisheni *invite expression of interest* ili hiki kitu kiweze kufanyika. Huo uongozi wa Mamlaka uliitwa ukaelezwa, ukafahamishwa wazi na wala haikuwa siri. Sasa leo uongozi huo wenyewe waka-*mess* walipo-*mess*, wakafanya walivyofanya, sasa hivi imekuwa hoja kwamba serikali inawaingilia, mimi haya yananipa muda kidogo kuyafahamu, maana ilipokwama wananchi hawataki kuhama ikajengwa *apron* wao ndio waliokimbilia serikalini ili serikali iwasaidie, lakini haikuambiwa serikali imewaingilia. Sasa muingilio huu labda tumuombe Dk. Sira, lakini ni shida kufahamu hiyo hoja ya kwamba serikali inakuingilia vipi wakati tumekupa maelekezo tunataka kufanya hili, kwa utaratibu huu. Tumekwenda kwa sababu sasa umeingiza na yako, unasema sasa serikali inakuingilia na kisa umesema sisi tumefuata utaratibu, serikali haitaki tufuate utaratibu.

Lakini Mhe. Mjumbe, leo ni Jumamosi tuko Barazani hapa, tokea lini Baraza likaja Jumamosi, ni kwa sababu tulitaka Baraza mambo yetu yaende. Sasa na hili ni kwa sababu waliolisimamia hawakutaka liende vile serikali ilivyoona inafaa, kwamba sio mtu ni *package* ni *concession*. Sasa leo mtu anajificha nyuma ya utaratibu. Mlipokwama mmeitwa Mhe. Makamu wa Pili kawaita hakuwaita siri, kamuita Mwenyekiti wa Bodi, Mkurugenzi Mkuu, Katibu Mkuu, Waziri haya hili mmekwama wapi. Aah! sisi hili tutalikwamua tupeni muda kidogo.

Sasa leo ugomvi mkubwa imekuwa tunazunguka, tunasema hili ni la fulani. Kwa sababu Mhe. Mshimba ukituletea *investor* nchi hii wenzako watanuna kumbe, watasema huyu *investor* wa Mhe. Makame Mshimba, kwa hivyo asipate hii kazi ndio inavyoelekea.

Mhe. Hamza Hassan ukimleta *investor* hapa basi inaonesha kwamba hiyo itakuwa ni hoja kuwa huyo *investor* asipate, maana hivyo ndio visingizio. Mhe. Spika, yanazungumzwa mengi katika hili, lakini mimi nasema naomba nimuhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba kwenye hili huu sio mradi wa mtu ni mradi wa serikali; ambayo imeona kuna maslahi kuwekeza kama ni *package*. Inashangaza kwa sababu Mwenyekiti wa Bodi na Waheshimiwa Mawaziri wamekuja hata ofisini kwangu kutafuta ushauri wa kisheria. Nikawaambia huu hamjatoa *award*, hakuna *liability* yoyote. Tutakwenda kurekebisha.

Mara ya pili Mwenyekiti wa Bodi anasema tutakwenda kurekebisha. Mara ya kwanza kasema mbele ya Mhe. Makamu wa Pili, na mara ya pili kasema mbele yangu, serikali labda mlivyolikabidhi hili mlikosea. Kwa hivyo, haya Mheshimiwa kama tutayafanya namna hii, kusema kweli nchi hii hapatawekezwa hata senti tano, maana mtu atazungushwa huko, halafu akiona huko kashindwa atakuja kwenye chombo hiki ili hiki chombo akitumie vibaya, lakini siamini kama chombo hiki kitatumika vibaya katika kukwamisha. *(Makofi).*

Mimi niseme kwamba hawa wawekezaji waliokuja wote ni wa hapa hapa Zanzibar, wala hawana shida na sisi kwamba wanatafuta pahala pa kuwekeza, hapana, sisi ndio tuna shida nao. Kwa sababu mradi mmoja mkubwa waliokusudia kuwekeza ni wa mafuta, wajenge kwa pesa zao pamoja na bandari ya kuteremshia mafuta, kazi yetu sisi ni kuwapa ardhi, *investor* hawa hawa. Leo tumefika pahala hapa tunasema kama kwamba wanataka kuja kuiba hapa kwetu, kusema kweli hatuwapi moyo wawekezaji.

Kwa hivyo, mimi naomba tuwasaidie sana watu wetu waone kwamba nchi hii baada ya miaka mitano tuwe na kitu cha kuonesha kwamba serikali hii pamoja na Baraza hili tuli-*facilitate* kuwekeza hivi na vile. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama tutatumia utaratibu huu kwamba mtu atazunguka amepewa kazi ya serikali akaingiza na yake, na halafu akasema utaratibu hakuna uwekezaji ambao utafanywa. Kwa kweli hili si la mtu isipokuwa ni la serikali, na jambo la msingi tuwasaidie wenzetu wasiwe na njaa ya kichwa na badala yake wawe na njaa ya tumbo tu. Kwa maana hiyo, ukiwa na njaa ya kichwa mambo haya yatakwama, maana kichwa hakishibi Mhe. Spika, lakini tumbo ukila litashiba na kichwa hakishibi! *(Makofi)*

Kwa hiyo, huu ni mradi wa serikali, na serikali kama unaweza kuufanya chini ya Sheria ya *Concession* ya mwaka 1999, lakini labda kosa lililofanya ni kuamini kwamba tunao watu wazuri na watalisimamia hili litakwenda nadhani hilo ndio kosa lililofanywa. Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii

kuwatoa wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe, kwamba huu si mradi wa mtu, isipokuwa ni mradi wa serikali kwa maslahi ya watu wa nchi hii, vijana wetu wapate kuajiriwa pamoja na uchumi wa nchi yetu uweze kukua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nawaomba sana wenzangu tuiunge mkono hii hoja, ili tumuwezeshe Mhe. Rashid Seif Suleiman na timu yake waweze kufanyakazi. Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu, ahsante sana naona katika mchango wa Mhe. Mwanasheria Mkuu neno moja limewasumbua watu '*kichwa kutoshiba'*. Waheshimiwa Wajumbe, ni kweli kwa sababu kichwa hichi wakati wote fikra zinakuja hizi na zile, tena wataalamu wanasema katika muda wa dakika moja kiasi zaidi ya fikra sabini zinaingia humu na wala hakishibi kichwa hichi. Nadhani nimekifafanua kichwa chenyewe. *(Makofi)*

Baada ya mchango huo wa Mhe. Mwanasheria Mkuu sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, na mimi nataka nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa asubuhi ya leo tukiwa sote wazima wa afya.

Pili Mhe. Spika, nataka niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao waliyoitoa katika kuimarisha Wizara yetu ya Miundombinu na Mawasiliano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba michango iliyotolewa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi haikuwa na lengo la kumlenga mtu yeyote ndani ya Baraza hili au ndani ya Uongozi wa Wizara hii, bali ilikuwa na lengo la kuimarisha tu utendaji wa shughuli za Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, na mimi nawashukuru sana kwa hilo.

Kwa kweli Mhe. Spika, michango ilikuwa mingi, mimi basi nataka nijielekeze katika ujenzi wa *Terminal Building*. Mhe. Spika, najielekeza huko kwa nini? Kwa sababu serikali iliunda Kamati kupitia Baraza la Mapinduzi, iliunda Kamati kwa ajili ya kuangalia matatizo yaliopo katika *Terminal Building*.

Kwa bahati nzuri sana Mwenyekiti wa Kamati kwa mujibu wa tamko la Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein alimteua Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kutokana na hali hiyo, suala hili nalijua sana na nimeona na mimi nisaidie kuchangia kidogo, ili Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wao

wapate fursa ya kufahamu hasa nini kilichojiri mpaka tukausimamisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege kwa kipindi cha miezi takriban 7 mpaka 8. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wengi wa Wajumbe wa Baraza lako tukufu walitaka kuelewa tatizo ni nini na kwa nini? Na wengine walisema kuhusu habari ya fedha, na wengine walisema tulitie viringi tulisogeze nyuma, na wengine walisema tulibomowe. Kwa kweli michango yote ilikuwa na manufaa kwetu sisi serikali na ilikuwa na faida kubwa sana. *(Makofi)*

Nataka nianze kwa kusema kwamba serikali ilifanya uamuzi wa kuunda Kamati baada ya kupokea matatizo yaliopo ndani ya Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, nataka Waheshimiwa Wawakilishi wanisikilize vizuri na wala wasisikilize haya mengine yanayotoka nje.

Kwa kweli serikali ilipokea matatizo matatu ya msingi ndani ya Uwanja wa Ndege kuhusu ujenzi wa *Terminal Building*.

Tuliambiwa tatizo la kwanza uwanja umesogea mbele kwa mita 65, yaani ile *position* ya jengo imekwenda mbele mita 65. Kwa bahati mbaya hatukuambiwa athari yake ni nini kusogea mbele mita 65 na hata kwenye jeshi Mhe. Spika wakati wa gwaride kuna kitu ukienda pale kama kwenye Sherehe za Mapinduzi au Muungano wanakuja *step* au hatua za mbele kiasi kumi. Sisi hatukuambiwa athari zake ni nini jengo kusogea mbele.

Tukaambiwa tatizo la pili la uwanja uko *point* 9 *of a meter down the level of apron*, yaani *Terminal Building* iko chini *point 9 of a meter* ya ile *apron na take way*, ambayo inayojengwa na mkandarasi wa Kifasansa *SOGEA SATO*. *(Makofi)*

Tukaambiwa tatizo la tatu kwamba *position* ya Uwanja hutaweza kufunga *ILS*. Mhe. Spika, *ILS* ni chombo ambacho kinampa muongozo *pilot* kama yuko juu mita mia mbili aweze kuuona Uwanja hata kama uwanja una mawingu basi anauona, hivyo uwanja wetu hauna chombo cha *ILS*, lakini tunatarajia kukifunga siku za baadaye, hivyo kwa *position* hiyo hataweza *pilot* kutua.

Mhe. Spika, tukasema sawa kama hayo ndiyo matatizo *solution* yake ni nini? Kwa hivyo, zikatoka pale Mhe. Spika ufumbuzi wa matatizo, marekebisho mbali mbali; *designing* za uwanja, na yakatoka mambo matatu; *design* A, B na C. Sasa *design* C hiyo ndiyo iliyokuwa, kama A haikuwezekana twende C, na hayo ndiyo maagizo ya Baraza la Mapinduzi, ambapo C ni nini? Ni kulivunja na kulirejesha nyuma. *(Makofi)*

Vile vile na Kamati yangu ikapewa *mandate;* kama kutahitajika fedha za ziada basi Mhe. Waziri zungumza na *Exim Bank of China* pamoja na Serikali ya China, kwa ajili ya kutusaidia kupata fedha za ziada kwa marekebisho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna mambo ambayo ndani ya *Terminal Building* nataka Waheshimwia Wajumbe wa Baraza lako tukufu wafahamu, kwamba serikali ilijifunza mambo mengi sana. Kwanza ujenzi wa *Terminal Building* ulikuwa *design and build*, mimi nathubutu kusema kwamba hatukuwa na uzoefu wa *design and build*.

Lakini ilikuwa imeamuliwa kwamba *Terminal* ile iende katika *design and build*, na uzuri wa *design and build* ni kwamba unaweza ukarekebisha mchoro, maana yake unau-*design* na halafu munauangalia munau-*approve* na mnaweza mkaurekebisha kadri mnavyokwenda na ujenzi wa lile jengo.

Kwa hivyo, tulipomu-*hire consultant*, au msimamizi ama mshauri Kampuni ya *ATN* ya Uturuki katika mkataba wake hakukuwa na kipengele kinachosema *approve design*. Kutokana na hali hiyo, ikawa kidogo kuna msongomano na Kampuni ya *BCEG* ya China, inapotengeneza ile michoro kumpelekea yule wa *ATN* a-*approve* yule anachelewa, kwa sababu ile kazi haimo kwenye mkataba wake na ikawa kidogo kuna mvutano baina ya msimamizi na mkandarasi.

Mhe. Spika, mvutano ule Kamati yangu ikaona si busara kutumia ripoti za msimamizi huyu ziweze kutuongoza, basi kamati yangu ikafanya maamuzi ya kumuajiri *an independent consultant*, ambaye *ADPI* Kampuni nyengine ya Kifaransa ije sasa kwa ajili ya kuuangalia Uwanja mzima na kutupa ushauri wa kitaalamu kabla hatujafanya mazungumzo na Serikali ya China na wala hatujafanya mazungumzo ya *Exim Bank of China*, ambayo ndio waliotupa mkopo *SATO* milioni 70.4. *(Makofi)*

Kwa kweli nawapongeza sana washauri *ADPI*, walitupa ushauri mzuri na wakatuambia kwamba hakuna ambalo haliwezekani na huo ndio ushauri wa *ADPI*, wakajibu hoja moja baada ya moja na baada ya sisi kuwapelekea *terms of references* tunataka waangalie masuala yepi, yaani tuliwapa zaidi ya yale ambayo tuliyopewa na Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, tuliwapa pia waangalie gharama za ule mradi watushauri kama kubwa au ndogo ama *size* kulingana na kimataifa.

Mhe. Spika, Kampuni ya *ADPI* ni nzito na imefanya kazi nyingi sana za viwanja vya ndege. Vile vile sasa wao ndio waliokuja kutuambia kwa *position*

ya jengo haina matatizo, isipokuwa mnapaswa kuzi *reallocate* zile ndege na mwanzo ilikuwa ndege ina *park*, yaani zinatoa mikia kwenye *take way*.

Kwa hivyo, wakatuambia kwamba utaratibu wa kutoa mikia kwenye *take way* ndege kubwa kama hizi wakati unapozi-*push back* zitaingia kwenye *take way*, na kama kuna ndege nyengine inakuja itabidi ile isimame mpaka iruhusu hii itoke, na huo ni utaratibu wa kucheleweshe abiria.

Kwa maana hiyo, wakaziweka *South* na wame-*design* vizuri na kiutaratibu huo jengo *position* yake haina matatizo sana na mukizi-*reposition* ya ndege, lakini mutahitajia kujenga *apron* ya ziada kwa kuweka ndege *South*, na sasa ndege zita-*park South* zile kubwa na zielekee *North*, lakini *apron* ya ziada itahitajika.

Mhe. Spika, tulikuwa na fedha za kujenga *apron* nadhani ilikuwa *27square meters*, na hivi sasa itabidi ijengwe *apron* ya 34 au 35 *square meters*.

Lakini la pili wakasema kwamba *level* haina matatizo kwa sababu pale mnaweza mkarekebisha na tukaandaa michoro ikawa ile inatumika kama ni *service way*.

Kwa bahati nzuri wale wenzangu wote tuliokwenda China wapo Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na Mawaziri, Uwanja wa Beijing *Terminal II* ambao inashuka *Emirates* umejengwa na Kampuni hii ya *BCEG* na wala hii sio kampuni ndogo, na tumeona hizo *service road* zinavyofanywa, na wakasema na hili nalo si tatizo tunaweza kulirekebisha. Pia *ILS* walisema inaweza kufungwa na chombo hichi kikafanya kazi.

Kutokana na hali hiyo, tukawaomba sasa watusaidie kukamilisha ile ripoti, ili baadaye tuwe tunayo *independent report from independent consultant* na tuweze kukaa kitako na wenzetu wa Serikali ya China pamoja na *Exim Bank of China* kwa ajili ya kuweza kutafuta fedha za ziada.

Option ya pili waliy otupa wao *ADPI* wakasema kama haya munaona hamuyataki na fedha munazo munataka *simple* tu basi livunjeni musogeze nyuma, ili muweze kufanya hivyo mnavyotaka, lakini wakatuambia mukirekebisha *cost* yote ya jengo pamoja na hizo mulizozitumia, jengo litafika dola milioni 115, yaani mukilirekebisha *cost* yake, *final* itakuwa 115 *US dollars* na mukilivunja *cost* yake ya kujenga ya jengo jipya itakuwa 140 *million dollars*.

Mhe. Spika, nimefanya kazi kubwa sana tokea niko ndani ya Serikali ya Muungano mpaka nimekuja SMZ, naelewa utaratibu wa kupata fedha

unachukua zaidi ya miezi 12 kupata fedha, na tungelilivunja hili jengo maana yake *we have to submit a new project*, yaani *project* mpya.

Kwa msingi huo Mhe. Spika, ndio maana tukaenda China kwa sababu tayari Baraza la Mapinduzi lilikuwa tayari limeshatupa *mandate*, tukiona kwamba kuna uwezekano wa kulirekebisha na likakaa vizuri zaidi basi twendeni China. Kwa hivyo, tukaenda mimi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, nikaongoza *delegation* na tukaenda tunazungumza na *Exim Bank of China*, tukawaomba na tuliwaelezea *story behind* na wakatuuliza maswali mengi na tuka-*submit report* zetu na wakasema tuna-*grant* mkopo huo, kwa sababu ule mkopo ulikuwa *by* 31 *of July*, na kama tusingekwenda mkopo ule ulikuwa unakwisha na kufungwa, yaani ulikuwa ndio mwisho wa ule mkopo, hivyo tulikwenda tukaomba mambo mawili. Jambo la kwanza *extension* ya mkopo uongezwe muda, lakini tumeomba *addition resources* kwa ajili ya kuifanyia matengenezo *Terminal*.

Lakini baadaye tukazungumza na Serikali ya China; kwa sababu zile ni fedha kutoka serikali ya China zinakuwa *governed* tu na *Exim Bank of China* na *Ministry of Commerce* wakasema tuko pamoja na Zanzibar, kwa hiyo endeleeni na sisi tutawaambia wenzetu wa *Exim Bank of China* watoe hizo fedha, ili jengo liweze kuendelea.

Faida yake ya marekebisho nini? Mhe. Spika, katika ile *initial design*, mchoro huu haukuwa na *lobby* . Mhe. Spika, nitajaribu kutoa ufafanuzi kidogo waweze kunifahamu *lobby* nini? Kwa kweli *airport* nyingi Mhe. Spika, unapokwenda ukashusha abiria wako kuna pahala mnaweza mukaingia mukaagana na ile inaitwa *lobby at the airport*, na *airport* yetu *design* yake haikuwa nacho hicho kitu, unashusha abiria yuko kwenye *counter* hakuna sehemu ya kuagana na sawa sawa na *airport* hii tuliyonayo hivi sasa ukikitoa kile kipaa kile.

Kwa hivyo, katika mchoro wa sasa tunataka iwepo na *lobby*, ili abiria mkishuka pale ndugu zako, mna pahala mnasimama mnaagana, na tumeiongeza kidogo hii, na nataka niseme kwamba tumei-*redesign* kidogo, ili iweze kuleta haiba *airport* yetu. Mhe. Spika, tumefanya kwa nia safi kabisa na tumeona ipo haja hiyo.

Vile vile tumeangalia Mhe. Rais wa China Xi Jinping alipokuja alionana na Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein alimwambia naomba unisaidie miradi ya Zanzibar, na wakati huo tayari tumeshaiwasilisha miradi 7 ya

Zanzibar. Kwa bahati nzuri Mhe. Rais wa Zanzibar alipoalikwa China alikutana na Rais Xi Jinping, tena na mimi nilikuwepo katika kikao hicho akaambiwa miradi ya Zanzibar tutaisaidia yote; *put priority one by one* upi uanze mwanzo na sisi tukafikiria uhusiano wetu na China, tena Kampuni ya *BCEG* uhusiano wetu na China.

Mhe. Spika, China alianza uhusiano na sisi Zanzibar kabla ya Tanzania, yaani tulianza na sisi Zanzibar na tukasema *it will be no point* kusema kwamba mshauri ameshatuambia kwamba linarekebishika jengo na halafu sisi tukatumia *option* ya pili ya kulivunja.

Mhe. Spika, *mtaka cha mvunguni siku hizi hainami anabirua kitanda*. Kwa kweli kuna miradi saba tunataka tufanye kazi na China, basi tumeona ni vyema tukatumia *option* ya kwanza ya mshauri *ADPI* Mfaransa yule; na walikuja Wafaransa zaidi ya watatu kwa ajili ya kufanya hiyo kazi hapa *independent report*.

Kamati yangu mimi ni Mwenyekiti, Mhe. Rashid Seif Suleiman Makamo Mwenyekiti, yumo Mwanasheria Mkuu, pia yuko Katibu Mkuu Miundombinu na Mawasiliano, yumo Katibu Mkuu Fedha, yumo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wote hao kwa pamoja tukasema kwamba tumeshaondoa kinu juani, na *option* hii itatusaidia kuipeleka kwenye *cabinet*.

Mhe. Spika, tumeipeleka kwenye *cabinet; option* ya kufanya marekebisho na Waheshimiwa Mawaziri wote hawa walituuliza maswali mengi sana kwenye *cabinet* kama hivi ambavyo Waheshimiwa Wawakilishi wameuliza. Kwa kweli niliyajibu maswali yote haya, na namshukuru Mwenyezi Mungu akatumbia kwamba sasa tuendelee.

Lakini Mhe. Spika, nilitaraji kwamba baada ya muda ule Mhe. Rais ambaye ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi angesema kwamba Kamati hiyo sasa nimeshaivunja na tuwaachie wizara wenyewe, Baraza la Mapinduzi likasema Kamati iendelee kuufuatilia ujenzi huo mpaka utakapokamilika. Kwa hivyo, Kamati yangu bado iko *on the ground* inafanya kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako tukufu kamati zetu mbili, yaani Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi pamoja na Kamati ya *PAC* wawe karibu zaidi na wizara hii, ili waweze kuisaidia. Kwa hivyo, Mhe. Spika ni kweli Uwanja wetu ulikuwa na matatizo, pia ni kweli tumezungumza sana, ni kweli tuliusimamisha, lakini tulifanya hivyo kwa nia safi kabisa, na tulifanya hivyo ili tuweze kupata Uwanja mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niliona nikupe hayo angalau na mimi nichangie hivyo, lakini nataka nimalizie kwa kuwaomba Wajumbe wote kwamba tuwaunge mkono wenzetu tuipitishe bajeti yao hii, ili na wao waweze kutumia, kwa sababu fedha zao tayari zipo zimeshakuwa *allocated.* Mimi naunga mkono na nawaomba wenzangu waunge mkono wizara hii. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tunakushukuru sana. Mhe. Ismail Jussa Ladhu useme kwa utaratibu na wala usiingilie tu wakati wowote. Sasa ni zamu yake Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kutujaalia yote mema waja wake.

Pili Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu katika mnasaba huu mzima wa bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii nitamke wazi kwamba mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo la Chwaka tunaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Aidha Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi kutoa mchango wangu kwa kupitia njia ya kupunguza ama kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizoletwa au kuelekezwa katika bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutoka katika Baraza lako tukufu na Wajumbe wako makini, weledi na wenye uchungu wa nchi yetu.

Kwa hivyo, naamini kwamba malengo nia na dhamira sote ni kuitaka kuifanya Zanzibar iwe njema; yenye faraja na matumaini makubwa kufikiwa katika kutoa huduma kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sote tutimize dhamira yetu hiyo, ili kuweza kufikia yale mahitaji wanayoyahitaji wananchi tunaowaongoza.

Mhe. Spika, naomba nianze na hoja iliyohusishwa moja kwa moja katika Idara ya Mawasiliano, na swali hili liliulizwa na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, ambaye alielekeza hoja yake katika kujua faida ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayopatikana katika Shirika la Simu la Kampuni ya *ZANTEL*.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa 18 kati ya hisa 100 kwenye Kampuni ya *ZANTEL*, na kila mwaka gawio lake linatolewa kuelekea

serikalini, na naamini ufafanuzi mzuri kuhusiana na suala hilo utatolewa katika Bajeti ya Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hapo kesho itakapowasilishwa bajeti hiyo.

Hoja ya pili ilikuwa ya Mhe. Asaa Othman Hamad aliyetaka kujua utaratibu wa malipo ya kodi kati ya *TRA* na *ZRB*. Mhe. Spika, *ZANTEL* inaendelea kulipa kodi ya *ZRB* kwa zile kodi zinazostahiki kulipa katika chombo hicho cha *ZRB*, na inaendelea kulipa kodi katika *TRA* kwa kodi zinazostahiki kulipa katika chombo hicho cha *TRA*. Kwa kweli hakuna mabadiliko yoyote ya kodi tokea kuanzishwa kwa *ZANTEL* mpaka sasa na kama yatakuwepo, basi tunaamini kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa ya kwanza kujua kupitia wawakilishi katika Bodi ya Wadhamini na katika Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni hiyo.

Mhe. Spika, taarifa kutoka *ZANTEL* ni kwamba suala la kufukuzwa wafanyakazi 113. Kwa hivyo, taarifa kutoka *ZANTEL* ni kwamba suala la kuwafukuza wafanyakazi na kuwadhalilisha wafanyakazi hao halipo, isipokuwa Kampuni ya *ZANTEL* mnamo tarehe 31 Disemba, 2012 ilimaliza mkataba na wafanyakazi 113 na kuwalipa mafao yao yote.

Hata hivyo, suala hilo liko Mahakamani na tunaomba tu Mhe. Spika, kwamba tuendelee kusubiri maamuzi ya Mahakama na wala tusiwe sehemu ya kuliamulia kama ambavyo lilivyofikishwa katika chombo hicho cha sheria kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni kuhusu Kampuni ya *ZANTEL* kuhamisha Makao Makuu yake hapa Zanzibar. Mhe. Spika, Makao Makuu ya *ZANTEL*, yaani *Corporate Headquarters* yapo Zanzibar na mkakati wa *ZANTEL* ni kuwabakisha wateja wa Zanzibar waendelee kuitumia *ZANTEL* ambayo ni *retention strategic* na kutafuta wateja wapya (*inquisition strategic*).

Kwa hiyo, *ZANTEL* imeingia katika soko la Tanzania Bara kama mashirika mengine ya Bima na *PBZ* na Zanzibar tunachangia asilimia 3 ya soko la huduma za simu kwa Tanzania yote kwa jumla. Aidha katika soko hilo la asilimia 3 tayari asilimia 98 limeshatumika na asilimia 97 ya soko hilo liko Tanzania Bara, ambapo limetumika kwa asilimia 60 hadi muda huu.

Kutokana na hali hiyo, mwekezaji yeyote anahitaji kukua au kuendeleza mtaji wake, basi atawekeza nguvu kubwa katika sehemu ambayo kuna soko linakua na kubuni mikakati ya kuwabakisha wanaoendelea kutumia *ZANTEL* na hicho ndicho kinachofanyika na *ZANTEL* sio kama wamehamisha Makao Makuu yao au biashara. Mhe. Spika, wamefuata soko, kwani upande wa Tanzania

Bara kuna soko kubwa, kwa hiyo wanaimarisha huduma zao katika kuhimili soko kwa kutambua kwamba Zanzibar soko tayari wanalo na wanachohitaji ni kuliendeleza, ili kuwadhibiti wateja wao.

Vile vile kuna masuala ambayo yameelekezwa katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara; ambapo pia Mhe. Mbarouk Wadi Mussa aliulizia swali lake la usafishaji wa uwanja wa mpira wa Banyamulenge pale Potoa.

Mhe. Spika, Wizara ina nia ya kuikamilisha kazi na kukifanyia matengenezo kiwanja cha mpira wa miguu cha timu ya Banyamulenge kilichopo katika Jimbo la Mkwajuni kama tulivyokubaliana na Mhe. Mwakilishi. Kazi hiyo inahitaji kufanyika kwa kupitia chombo cha *bulldozer* ambalo limeshindwa kusafirishwa mpaka katika eneo la uwanja huo kutokana kuharibika kwake pamoja na matatizo mengine.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba mwaka jana tulitoa ahadi hii, lakini mimi mwenyewe binafsi nimeshawahi kwenda na Mhe. Mwakilishi na tulikusudia katika mwaka uliopita tukaifanye hii kazi. Bahati mbaya matarajio yetu wakati tunafanya barabara ya Kijini/Matemwe tulikusudia kwamba kazi hii ilikuwa ifanywe, lakini bahati mbaya chombo chetu kiliharibika na tukapatwa na tatizo la upungufu wa mafuta. Imani yetu kwamba tukipata nguvu na chombo chetu kikitengenea, kazi hii tutakwenda kuifanya kama ambavyo tulivyomuahidi Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, swali jengine la Mhe. Hija Hassan Hija alitaka kujua mchanganuo wa gharama za ujenzi wa barabara ya Mgagadu/Kiwani kwa kiwango cha kifusi. Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imetumia jumla ya shilingi milioni 437 kwa kazi za ujenzi wa barabara ya Mgagadu/Kiwani kwa kuanzia mwaka 2009 hadi mwaka 2013. Barabara hii ina urefu takriban kilomita saba. Mchanganuo wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa Barabara ya Mgagadu/Kiwani hadi hivi sasa ni kama ifuatavyo:-

Mwaka	**Matumizi**
2009/2010	Milioni 50
2010/2011	Hakukuwa na matumizi
2011/2012	Milioni 200
2012/2013	Milioni 187

Mhe. Spika, suala jengine ni matengenezo ya barabara katika Jimbo la Uzini. Suala hili limeulizwa na Mhe. Mohammedraza Hassanali Daramsi, alitaka kujua makisio ya gharama za kazi yalikuwa ni milioni 87.

Ni kweli Mhe. Raza alichangia shilingi milioni 20. Hata hivyo hakuna mkataba baina ya Wizara na Mhe. Raza katika utekelezaji wa kazi hiyo. Kazi iliyofanyika kwenye matengenezo ya kilomita mbili, barabara ya kutoka Mpapa, Pagali hadi unafikia Umbuji kwa kiwango cha kifusi. Kazi hii ilisita baada ya *bulldozer* lililokuwa likitumika katika kazi hiyo kuharibika na kuhitaji matengenezo yanayogharimu zaidi ya shilingi milioni 16.

Mhe. Mohammedraza Hassanali analijua hilo na *bulldozer* hilo bado lipo katika eneo hilo. Aidha Mhe. Spika, tunaishukuru na kuipokea ofa ya Mhe. Mohammedraza, tunaamini kwamba utaratibu wake utakuwa ni mzuri.

Ninachotaka kumuomba Mhe. Raza kwamba ofa ile aiwasilishe katika Halmashauri husika katika Wilaya ya Kati pamoja na Wilaya nyengine. Sisi kama Wizara ya Miundombinu tungependa tuzungumze na taasisi ili kuondoa mivutano na kupishana kwa lugha. Tunaamini kama chombo cha Serikali tukiweza kuzungumza na taasisi za serikali, ufanisi utapatikana mkubwa zaidi, sote tukiwa na dhamira moja ya kutaka kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, aidha Mhe. Omar Ali Shehe alitaka kupata maelezo ya utaratibu wa bajeti zote mbili ya Idara ya Ujenzi na Utunzaji barabara. Mhe. Spika, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa barabara ina bajeti moja kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Kazi za matengenezo ya barabara hufanywa kwa kutumia fedha za Mfuko wa barabara, bajeti ambayo inatoka kwenye Wizara ya Fedha.

Aidha, alisema kuna ubadhirifu katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Amani Mtoni. Kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya Amani Mtoni ni kuwa awamu ya pili ya mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2011 kwa kutumia fedha za ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na kutokamilika kwa kazi ya ujenzi wa barabara hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2012 iliamua kuendelea utekelezaji wa mradi huo kwa kutumia fedha kutoka Mfuko wa barabara Zanzibar. Taratibu za manunuzi na matumizi ya fedha zinazingatiwa katika hali zote za uendeshaji wa mradi huo kama tulivyoeleza.

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Asaa Othman Hamad, walitaka kupata maelezo kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi barabara hiyo ya Amani/ Mtoni. Mradi wa barabara ya Amani\ Mtoni awamu ya pili ulianza mwaka 2011 kwa jumla ya fedha shilingi bilioni 1.6, zilitolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwaka 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 500 kutoka mfuko wa Barabara zilitumika kuendeleza ujenzi huo ambapo kilomita 2.2 zilijengwa kwa kiwango cha lami na mita 800 zilijengwa kwa kiwango cha kifusi. Aidha shilingi milioni 119 zilitumika kwa kulipa fidia kwa baadhi ya nyumba ili kuruhusu ujenzi huo uendelee.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara imepanga kutumia jumla ya shilingi milioni 500 kwa ulipaji wa fidia ya nyumba za wananchi zilizokuwemo kwenye eneo la barabara hiyo, na shilingi milioni 558 kwa ajili ya ukamilishaji wa kazi ya ujenzi wa barabara hii.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Bakari Makame ametaka maelezo kuhusiana na kutoonekana kwa barabara zilizofanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, kazi ya matengenezo ya barabara za Pemba zimeoneshwa katika viambatanisho vya kitabu chetu cha hotuba ya bajeti katika ukurasa wa 62, 63, 64,65 na 66 kwa kazi za matengenezo mbali mbali za barabara na daraja. Kwa mwaka wa fedha 2013 ukurasa wa 69,70,72,73 na 74 ambazo zinafanyiwa matengenezo mwaka ujao wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, Mhe. Saleh Nassor Juma, alitaka kujua barabara za Vikunguni, Ng'ambwa na Uwandani, hazifanyiwi matengenezo na ni muhimu kwa wakulima.

Mhe. Spika, Wizara imekuwa ikichukua juhudi na kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za ndani kwa kutumia fedha za Mfuko wa barabara ili ziweze kupitika wakati wote. Katika jimbo la Vitongoji wizara tayari imekwisha kuzifanyia matengenezo ya kawaida na maeneo korofi barabara za Wawi, Vikunguni, Mzambarau Mboko ambayo ina urefu wa kilomita nane, Ole Kianga, Ng'ambwa, Mkoroshoni ambayo ina urefu wa kilomita 6 pamoja na ujenzi wa daraja dogo la kuweka kifusi kilomita moja 1 katika barabara hiyo. Barabara hii imetoa ufumbuzi mkubwa kwa wananchi wa Ng'ambwa na vitongoji vyake kwa kwenda Chakechake au Wete.

Mhe. Hamza Hassan Juma, alitaka kutofanyika matengenezo ya barabara ya kwa Abasihusseni, Shaurimoyo na malipo ya fidia ya nyumba kwa barabara ya Amani / Mtoni kufanyiwa mapitio ili iendane na wakati.

Mhe. Spika, Wizara katika kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais kuhusiana na matengenezo ya barabara hiyo, tayari nimeingiza kwenye makubaliano ya matengenezo ya Mfuko wa barabara kwa kuifanyia matengenezo maeneo

korofi kwa kuweka lami na itafanyika sambamba na ujenzi wa barabara Amani/Mtoni.

Mhe. Spika, Mhe. Abdi Mossi Kombo, pamoja na Mhe. Kazija Khamis Kona na Mhe. Ussi Jecha Simai, wao kwa ujumla walikuwa wanataka kujua mpango wa serikali wa kuyafanyia matengenezo madaraja membamba na mabovu kwa barabara za Kaskazini Unguja; Ujenzi wa barabara ya Mkwajuni, Kinyasini hadi Kivunge ambayo inaishia Mkokotoni.

Mhe. Spika, madaraja hayo yote yamo katika mradi katika jumla ya mradi wa barabara unaohusisha barabara zinazoingia mjini Unguja. Ambazo upembuzi yakinifu umekamilika ambao barabara hizo zimo katika mpango wa kutafutiwa mfadhili kama ilivyoelezwa katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 15 kifungu cha 33.

Kuhusu ujenzi wa barabara wa Mkwajuni/Kinyasini na Kivunge/Mkokotoni. Wizara kwa sasa inahitaji kuzihami sehemu mbaya za barabara hizi hadi hapo utekelezaji wa mradi wa barabara zinazoingia mjini utakapoanza.

Mhe. Spika, Mhe. Nassor Salim Ali alitaka kujua matengenezo ya barabara za Jimbo la Rahaleo zikiwemo barabara za Mlandege, Kwabiziredi na kadhalika. Barabara za ndani ya Jimbo hili ziko chini ya uangalizi wa Baraza la Manispaa la Mji wa Zanzibar. Hivyo ni vyema kuwasiliana na uongozi wa Manispaa na kuangalia namna wanavyoweza kushirikiana na kuzifanyia matengenezo barabara hizo, ukiwemo uzibaji wa mashimo katika barabara hizo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Nassor alitaka kujua kiwango cha ubora wa barabara ya Ole, Kengeja ambayo imepangwa kujengwa kwa kutumia nguvu kazi. Napenda kuchukua nafasi hii kumuomba Mhe. Mwakilishi yeye asiwe na wasi wasi na ujenzi wa barabara hii, kwa kutumia mfumo ulioeleweka Wizara inawahakikishia barabara hiyo itakuwa na kiwango kizuri kwani tayari ina uzoefu wa kutosha kuhusu ujenzi wa aina hiyo na matatizo yaliyojitokeza.

Mhe. Spika, Mhe. Salma Mussa Bilali alitaka kujua barabara ya Umbuji haikuorodheshwa katika kitabu cha bajeti. Barabara hiyo inayotoka njia nne hadi Umbuji ina urefu wa kilomita 5 imo katika mpango wa matengenezo kwa kiwango cha lami kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti ukurasa wa 29 kifungu cha 80.

Mhe. Spika, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Shadya Mohammed Suleiman na Mhe. Rufai Said Rufai walitaka maelezo kutopatiwa kazi waliokuwa wafanyakazi wa mradi wa TRRT. Wafanyakazi hao wamepatiwa mafunzo ya

utunzaji barabara na hivi sasa wanaendelea na kazi kwa mkataba wa kuzitunza barabara hizo kwa mwaka mzima. Wafanyakazi walikuwa wakilipwa 18 *bonus* ya mshahara wao katika mradi huu. Kwa hivyo hawakustahiki kulipwa motisha, hii ilitegemea kazi waliyofanya kushuka baadhi ya nyenzo.

Kuhusu barabara Kuukuu imo katika mpango na imeamuliwa kujengwa kupitia ujenzi wa barabara ya Mkanyageni/Pangani, barabara hiyo tayari imefanyiwa matengenezo katika shemu zote mbaya kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Vile vile barabara hii imo katika mradi wa barabara za vijijini zitakazojengwa kwa kupitia mradi *Mirvaf* chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo.

Mhe. Spika, aidha limekuja suala la matengenezo ya barabara tatu za Micheweni, barabara ya Wingwi Mjini, zimefanyiwa matengenezo na barabara ya Micheweni / Shumba Mjini na Micheweni / Kiuyu zitafanyiwa matengenezo hivi karibuni kupitia fedha za Mfuko wa babara wa mwaka uliopita.

Mhe. Spika, pia Mhe. Subeit alitaka kujua suala la mashimo ya uchimbaji wa vifusi kwa kampuni ya *H. Young.* Kutokana na mkataba wa ujenzi na mkandarasi na hakutokuwa na kurejesha eneo lililohusika lilochimbwa kifusi katika hali ya kuweza kutumika kwa kupanda miti na kufikia kwa maeneo fulani. Kampuni hiyo tayari imefanya kazi ya kufukia mashimo katika eneo la Finya, maeneo ya Pandani na eneo la Micheweni.

Imani yetu kwamba kampuni hii itazingatia kwa kina na itafanya kama vile ilivyoelekezwa kwenye mkataba, lakini na sisi kama wizara tutalisimamia hilo ili kuona jambo hilo linafanyika vizuri kama vile mahitaji yanavyohitajia.

Mhe. Spika, Mhe, Rufai Said Rufai na Mhe. Hamad Hassan Hamad, walitaka kujua maharibiko ya nyumba katika ujenzi wa barabara ya Mzambarauni hadi Mapofu.Wizara inalitambua hilo kwa kushirikiana na MCTA tayari kwa mara ya sita mfululizo yatafanyika malipo mengine hivi karibuni kwa nyumba zilizoathirika na kuthibitishwa na wakaguzi na kukubaliwa kulipwa fidia. Fidia hizo zitalipwa hivi karibuni baada ya kukamilika taratibu za malipo katika barabara ya Chwale / Kojani, Mzambarauni / Pandani, Finya / Mapofu na barabara ya Bahanasa / Daya Mtambwe.

Mhe. Spika, kutofanyia tathmini watu 14 katika barabara ya Chwale Kojani. Tathmini ambazo zimefanyika zikiwemo za watu, kwenye barabara hiyo ambazo zimekubaliwa na hatua mbali mbali zimeshachukuliwa na ambapo wamethibitika kulipwa fidia, watalipwa fidia hizo hivi karibuni.

Kuhusu barabara Mtijuu, Shengejuu, haikupangwa kutekelezwa mwaka huu kutokana na matengezo ya barabara ya Meli tano/Maganjani iliyo katika Jimbo hilo. Tunaomba Mhe. Mwakilishi, tunaomba ufanye subra kabisa, tukamilishe miradi hii ambayo tumeitaja kabla, baadaye tutaendelea na *second phase* ya kwenda kuona hayo maeneo ambayo Mhe. Mwakilishi anayaomba.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis, alitaka kujua utoaji kifusi Mlima wa Mkia wa Ng'ombe na ujenzi wa barabara ya Msuka/Kiuyu hadi Makangale. Matengenezo ya mlima huo yanaendelea na kutiwa kifusi sambamba na ujenzi wa daraja unaomalizika hivi karibuni. Kuhusu barabara ya Msuka iliyokuwa ikitengenezwa na Japan mradi wa JICA imekamilika. Hivi sasa barabara hiyo itaimarishwa kupitia mradi wa *MIRVAF* wa Wizara ya Kilimo.

Kuhusu barabara ya Kiuyu ambayo inapita katika Msitu wa Ngezi, tayari imo katika mpango wa barabara zitakazotekelezwa mwaka 2013/2014. Ukiangalia kitabu chetu cha bajeti kiambatanisho kipo ukurasa wa 71.

Mhe. Spika, Mhe. Kazija Khamis Kona alitaka kujua matengenezo ya barabara ya Kijini/Muyuni yenye urefu wa kilomita sita. Wizara imezipokea shukurani alizozitanguliza kwetu, na kuhusu matengenezo ya barabara iliyojengwa kwa kutumia fedha za mfuko wa Barabara. Wizara imepanga kwa kuifanyia matengenezo ya kawaida ya kurejesha kifusi kwenye maeneo yaliyoharibika baada ya mvua kubwa kunyesha na kuondosha kifusi hicho.

Aidha naomba tu Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi akumbuke kwamba barabara hii ni miongoni mwa barabara tano za vijijini Unguja ambazo serikali imo katika mchakato wa kutafuta mfadhili kuweza kujenga katika kiwango cha lami.

Mhe. Spika, Mhe. Ussi Jecha Simai, alitaka kujua ni lini mtaro wa Bububu/ Kijichi utamalizika. Ufukuaji wa mtaro kwenye barabara ya Bububu/Kijichi hadi Mndo umekamilika kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara; ambapo jumla ya kilomita mbili zilifukuliwa na sehemu ya mitaro iliyobaki itafanyiwa usafi kwa kutumia kikundi cha jamii kilichopo katika maeneo hayo ya Bububu.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa alitaka kujua *variation* ya kazi ya *junction* ya Mchina mwanzo. Zabuni ya kazi katika eneo la Mchina mwanzo ilitokana na usanifu uliofanywa na Kampuni ya *ICT* ya India katika mradi wa barabara zinazoingia mjini yaani *Town Entry Road.* Mkataba wa ujenzi wa kazi hiyo ulikuwa ni jumla ya shilingi milioni mia mbili, kumi na mbili na laki moja (212,100,000). Wakati wa ujenzi wa eneo hilo ilibainika kuwa makutano hayo

kama yangejengwa kwa kuzingatia usanifu wa *ICT* usingekidhi haja iliyokusudiwa. Hivyo Wizara ililazimika kufanya mabadiliko kadhaa yaliyokusudiwa kuimarisha usalama wa watumiaji na kupunguza msongamano wa magari katika eneo hilo. Kazi zilizoongezeka ni kama zifuatazo:-

1. Kuliongezeka eneo la kufanyia kazi kutoka urefu wa mita 157 hafi kufikia urefu wa mita 258, kukiwa na ziada ya mita 101. Ambapo kazi zote awali ziliongezeka katika urefu huo, kazi ya utanuzi, kifusi, uwekaji wa lami na uwekaji wa mawe ya pembeni ya kati kati.

2. Aidha kazi ya kuchimba iliongezeka kutoka kina cha sentimita 40 hadi kufikia sentimita 170 na kuwa na ongezeko la uchimbaji wa kina cha sentimita 130. Hii imetokana kuondoa udongo mchafu na takataka ambazo zilibainika wakati wa uchimbaji.

3. Kazi ya kung'oa visiki na kubandua zege kwenye eneo la maduka. Ambapo awali eneo hili halikuwemo kwenye eneo ambalo limesarifiwa kwa mujibu wa mchoro wa ICT.

4. Kuongezeka maeneo ya kusimamia gari za abiria.

Kwa kuangalia ongezeko hili la kazi, ni wazi kwamba kazi iliongezeka ni sawa na kazi ya awali hivyo kufanya gharama kufikia shilingi milioni mia nne ishirini na moja, laki saba arubaini na saba, mia tatu na arubaini (Sh. 421,747,340).

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh alieleza *concern* zake katika Idara ya Usafiri na leseni ambapo alitaka kujua hatua zilizochukuliwa za kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazoikabili Idara ya Usafiri na Leseni hasa katika suala la makaazi na ofisi za kufanyia kazi. Ni kweli Idara hii inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo uchakavu wa jengo la Idara.Wizara inakusudia kujenga jengo jipya la kuweka vifaa vya kisasa vya upasishaji wa magari katika kulipatia ufumbuzi wa kudumu jambo hilo. Aidha wizara inaendelea na juhudi za kumpata mfadhili atakayesaidia mradi wa ujenzi wa jengo hilo pamoja na uwekaji wa vifaa vya kisasa vya ukaguzi katika eneo hilo.

Mhe. Mgeni Hassan Juma, alitaka kujua majukumu ya Jumuia ya Madereva na Matingo. Idara katika utekelezaji wa kazi zake na majukumu inashirikiana na wadau mbali mbali wa usafirishaji ikiwemo Jumuia ya Madereva na Matingo kwa lengo la kuleta ufanisi na ushirikishwaji wa jumuia hizo katika maamuzi mbali mbali yanayohusu jumuia hizo. Kwa mujibu wa sheria namba 7 ya mwaka 2003. Wizara tayari imewateua wajumbe wawili kutoka Jumuia

za Magari mmoja kutoka Pemba na mwengine kutoka Unguja kuwa wajumbe wa Bodi ya Usafiri na Leseni.

Mhe. Spika, ni kweli katika utendaji kazi wa Idara tunalazimika kushirikiana na taasisi mbali mbali ikiwemo taasisi ya Jumuia za Madereva pamoja na Matingo. Lakini pia tumekuwa na jambo ambalo limekuwa likisemwa kwamba taasisi hizi zimekuwa zikifanya baadhi ya kazi ambazo zingepaswa kufanywa na Idara. Jambo hili sisi kama wizara tumeliona na tunaiomba idara yetu kwa kupitia bodi yao wakae walitafakari upya, ili kuona kwamba yale majukumu ya msingi ya kufanywa na idara yaendelee kufanywa na idara na yale ya msingi ya kufanywa na taasisi hizi kama washirika waendelee kufanywa na taasisi hizi.

Mhe. Spika, pia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alitaka kujua kuhusiana na wafanyakazi usiku gari zinazobeba Makontena. Mhe. Spika, magari yanayobeba makontena yanafanya kazi mchana kutokana na uhaba wa nafasi katika Bandari ya Malindi. Hata hivyo wizara kwa kushirikiana na taasisi nyengine husika inafanya kila juhudi kuhakikisha kuwa magari hayo yanafanya kazi kwa usalama wa hali ya juu.

Ni kweli Mhe. Spika, kumekuwa na tatizo hili wenzetu hawa wanaotoa huduma ya usafiri wa makontena wanaotumia magari, wamekuwa wakitumia barabara zetu nyakati za mchana na bahati mbaya hawapo waangalifu katika suala zima la mwendo, wamekuwa wakiendesha magari haya kwa mwendo wa kasi sana. Jambo ambalo linaweza likasababisha maafa au majanga tusipokuwa makini.

Sisi kama wizara tutahakikisha kwamba Idara kwa kushirikiana na wenzetu wa jeshi la polisi kuona kwamba jambo hili tunakaa na kulijadili na kuona namna gani tunaweza kulipatia ufumbuzi utakaoweza kuondoa taswira hiyo ambayo inaweza kujengeka ya muonekano wa ajali ambazo zinaweza kusababisha maafa makubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pia Mhe. Farida Amour Mohammed alitaka kujua vifaa chakavu kupelekwa Pemba. Ni kweli katika eneo ambalo sasa hivi panajengwa *passing* za *Terminal* katika eneo la Bandarini ilikuwa ndio sehemu kubwa ya mitambo ya matengenezo kwa Idara hii ya Usafiri na Leseni. Baadhi ya mitambo imetumika kupelekwa katika Karakana Kuu iliyopo Chumbuni, baadhi ya mitambo imetumika kwa kupelekwa Pemba, na baadhi ya mitambo ambayo haitumiki tukaiuza kama vyuma chakavu.

Kwa hivyo kupeleka vifaa hivi Pemba sio kama vimepelekwa kwa ajili ya kwamba kumepelekwa mitumba, hapana. Ni wale ambao mafundi

wameangalia na kujiridhisha kwamba vifaa ambavyo wanavihitaji wamevichukua kuvipeleka Pemba, vifaa ambavyo vinahitajika Karakana Kuu Chumbuni vimepelekwa, na vile vifaa ambavyo havihitajiki vimeuzwa kwa kupitia mfumo wa vyuma chakavu.

Mhe. Salma Mussa Bilali alitaka kujua uimarishwaji wa Karakana Kuu ya Unguja. Kama nilivyoeleza katika hotuba ya bajeti ukurasa wa 31. Serikali ina lengo la kuimarisha Karakana Kuu ya serikali iliyopo Chumbuni ili iweze kufanyia matengenezo magari ya kisasa. Miongoni mwa jitihada hizo ni kuendelea kuwapatia mafunzo ya matengenezo ya magari ya kisasa wafanyakazi katika sehemu hiyo pamoja na kuimarisha maslahi yao.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alitaka kujua suala la udhibiti wa madereva wasiokuwa na leseni na madereva wenye umri chini ya miaka 18 na watoto wadogo. Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 ya Usafiri Barabarani imekataza wale wote ambao hawajafikia umri wa miaka 18 kuendesha vyombo vya moto isipokuwa vyombo vya moto visivyozidi TC 50 yaani *speed* 50 kilomita kwa saa.

Kuhusu watoto wadogo kuendesha baskeli barabarani. Wizara inalichukua na tutakaa na wenzetu jeshi la polisi ili kuweza kufikia na kuona namna gani jambo hili linaleta ufanisi bila ya kusababisha bughudha au matatizo ambayo yamejitokeza.

Mhe. Spika, naomba niendelee tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, lakini pia naomba nichukue nafasi hii kwa kuwasihi na kuwaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi, watafakari sana kwa kina, na naamini kwamba wakirudi katika malengo au wito wetu hapa wa kuwasaidia wananchi watukosoe, watuelekeze, lakini mwisho wa siku watupitishie bajeti yetu ili tukafanye kazi ya kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache naomba niseme kwamba naendelea kuunga mkono hoja asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu tunakushukuru sana. Sasa kwa heshima kubwa naomba nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na afya njema tukaweza kukutana hapa leo katika shughuli zetu za kawaida za bajeti. Mategemeo yangu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kwa uwezo wa Waheshimiwa Wawakilishi bajeti hii itapita bila ya matatizo. Na mimi

ningependa kuwasihi sana Wajumbe wenzengu wa Baraza lako tukufu, kuipitisha bajeti hii ili kuwapa nguvu na kuipa nguvu Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano kufanya kazi zake.

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba siku niliyofanya majumuisho ya hotuba ya Ofisi yangu, nilianza kwa kusema kwamba mimi ni mmoja ambaye nachukia sana ubadhirifu, ninayechukia sana wizi na nachukia sana ubinafsi na bado ninao msimamo huo. Lakini pia serikali haipendi ubadhirifu, haipendi wizi na haipendi ubinafsi. Kwa sababu tunaamini mambo haya ya ubadhirifu, wizi na ubinafsi hauwezi kabisa kuleta maendeleo katika nchi yetu. Ndio maana kila wakati inapogundulika kuna ubadhirifu serikali inachukua hatua za kinidhamu na kisheria kwa wahusika.

Napenda niahidi Baraza lako tukufu kwamba serikali itaendelea kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kufanya ubadhirifu, wizi wa mali ya serikali na ubinafsi, kwa sababu jambo hili halitotusaidia.

Mheshimiwa mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Mawaziri, kwa hivyo yale maeneo ambayo mimi nilitaka niyachangie kwa kweli yamechangiwa vizuri sana na Mwanasheria Mkuu wa serikali pamoja na Waziri wa Fedha. Mimi ninachotaka kukifanya hapa leo ni kuwaahidi tu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza, kwamba ubadhirifu, wizi, hautovumiliwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dokta Ali Mohammed Shein, kabisa kabisa hatutoweza kufanya hivyo.

Mhe. Spika, suala la wizi na ubadhirifu limezungumzwa sana katika Baraza lako, na ikaonekana serikali hii kazi yake na watendaji wake ni wabadhirifu, watendaji wake wezi, watendaji wake wala rushwa. Serikali huizingatia sana michango ya aina hii ndani ya Baraza lako tukufu. Tunawashukuru sana Wajumbe kwa kuitanabahisha serikali, kwamba ndani ya serikali kuna jambo hili linatendeka, kuna jambo hili linatendeka. Na niseme kila itapobidi Mhe. Spika, serikali itamchukulia hatua mtu yeyote ambaye atabainika na madhambi haya ya wizi na ubadhirifu, yeyote. Serikali haitomuogopa mtu yeyote.

Mhe. Spika, kuna suala hapa limezungumzwa sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu nafikiri na Wajumbe wengine. Suala la *Ground Handling* la *Airport*. Namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu amelitolea maelezo ya kutosha. Maana kwa namna ilivyotolewa hapa Mhe. Spika, inaonekana kama huu ulikuwa ni mradi wa Balozi Iddi. Mimi sina mradi wala sina maslahi ya mradi wowote, maslahi ni ya nchi. Serikali siku zote itasimamia maslahi ya nchi na sio maslahi ya mtu.

Kama Mhe. Mwanasheria Mkuu alivyosema kwamba mradi huu uliungwa mkono na serikali; na serikali ikatoa maagizo, na popote pale serikali inapoona mradi fulani una maslahi kwa nchi ni lazima iunge mkono. Ndivyo ilivyofanywa kwa mradi huu. Mwekezaji aliyejitokeza ambaye tunaona alikuwa ana faida kubwa kwa serikali, ana faida kubwa kwa nchi, ndio serikali ikamuunga mkono mwekezaji huyu. Maelekezo nilikuwa nayatoa, maagizo niliyokuwa nayatoa hayakuwa maagizo yangu yalikuwa ni maagizo ya serikali.

Maana kuna baadhi ya Wawakilishi huenda wamelishwa maneno, kwamba mwekezaji huyu anaungwa mkono na Balozi Iddi lazima amepata kitu chochote. Mheshimiwa, mimi nina heshima kubwa katika Serikali ya Zanzibar na pia Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Nimefanya kazi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa muda wa miaka 30. Tangu niingie katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nataka mtu a- *challenge,* aje mtu aseme kwamba wewe Balozi umefanya hili, wewe umefanya hivi. Mimi siku zote nagombea maslahi ya nchi sio maslahi yangu. Ikiwa kwa muda wa miaka 30 nimefanya kazi sikuwa tajiri, basi siwezi kuwa tajiri kwa miaka miwili mitatu, kwa sababu ya kuweka ubinafsi wangu mbele. *(Makofi*)

Kwa hivyo Mhe. Spika, mradi huu kwa kweli una faida kubwa kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa nchi. Faida amezieleza Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwanza inaleta pato kubwa kwa serikali, italeta maendeleo makubwa ya kiuchumi kwa serikali na itapunguza matatizo ya ajira kwa vijana wetu. Kwa sababu hii ni *package* ya miradi karibu minne mwekezaji huyu anataka kuleta. Na mimi nilipokutana na mwekezaji huyu sikuwa peke yangu kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, nilikutana na mwekezaji huyu Dubai nilipopita pale nilipokuwa narudi safari, nikawaita watendaji wa Wizara zote zinazohusika.

Nilimwita Katibu Mkuu Fedha, Katibu Mkuu Miundombinu, Katibu Mkuu Ardhi, na ZIPA tulizungumze hili. Sote tukawafiki kwamba mwekezaji huyu kwa kweli atatufaa kwa maendeleo ya nchi yetu. Tulivyorudi sote tukaenda kwa Rais kwenda kumtaarifu juu ya mwekezaji huyu, Rais akakubali akasema kweli kama hali ni hiyo huyu mwekezaji atatufaa. Miradi ile ameizungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu tunataka kitu gani sasa.

Waheshimiwa Wawakilishi siku zote wanazungumza maslahi ya nchi, leo serikali ikizungumza maslahi ya nchi aa fulani kapata chochote, hivi tutakwenda Mhe. Spika, hatuwezi kwenda, na hata hao wawekezaji wataogopa kuja na kila siku serikali inakwenda nje Rais anakwenda nje, mimi nakwenda nje kwenda kushajiisha wawekezaji waje kuwekeza hapa nchini petu, lakini wakija tukianza kuwazungusha kwa sababu tu mtu anataka chake

kwanza tutakwenda wapi? Mhe. Spika, hili hatuwezi kulivumilia hata siku moja, na hatutakubali maslahi ya nchi yakapigwa teke kwa sababu ya maslahi ya mtu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kama nilivyosema mengi yamezungumzwa; mambo ya *ground* hili limezungumzwa, ujenzi wa jengo jipya la abiria limezungumzwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ujenzi wa barabara za Pemba limezungumzwa, kwa nini limechelewa? Kweli limechelewa kwa muda mrefu lakini matatizo yameelezwa, matatizo yalikuwa ya kifedha.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema sikutaka kuchukua muda wako lakini nilitaka nisisitize kabisa kwamba serikali haitavumilia ubadhirifu, haitavumilia wizi, haitavumilia ubinafsi; ambayo yatarudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru kwanza namshukuru Allah kwa kutujaalia uhai, uzima na *taufiq* ya kufika hapa. Mhe. Spika, kabla sijaanza kutoa majumuisho naomba kwanza niwashukuru sana Wajumbe wote ambao wamechangia kwa kauli zao na wale waliochangia kwa maandishi. Kama wangelikuwa hawana imani na hii Wizara wangenyamaza kimya tukatoka tukaenda zetu, na mimi nikatoka na mambo yangu. Lakini naamini sana wana imani na wana uchungu na hii Wizara, kwa hivyo mimi nawapongeza na nawashukuru sana kwa michango yao ambayo wameona mambo mbali mbali yanayotokezea katika Idara zetu, katika mashirika yetu, na mengine ambayo pengine nimefanya mimi; yote hayo sisi sote ni binaadamu, sote tuna taratibu zetu na kila moja na anavyoona. Kwa hivyo mmefanya kazi yenu vizuri hii ndio kazi ya Baraza la Wawakilishi, kazi ya kuiongoza serikali, kazi ya kuielekeza serikali, kazi ya kuitaka serikali ifanye yale ambayo yaliyokusudiwa kwa wananchi.

Ila Mhe. Spika, naomba niseme jambo moja dogo, mtu yoyote unapomkabidhi kazi hata kama ni fundi umemkabidhi nyumba kujenga akikosea humshiki ukosi ukamtupa nje, unamwambia hapa umechemsha, hapa tofali halikukaa sawa, hapa hivi, ukishamuelekeza hivyo muangalie sasa atakavyobadilika yeye na yale maelekezo yako. Kwangu mimi haya ni maelekezo ya mwanzo Mhe. Spika, katika Baraza hili lako tukufu, kwa sababu nilishika nafasi hii kipindi hiki hiki cha bajeti ya mwaka katikati ya bajeti, nusu ya bajeti ya mwaka jana mimi nilikuwa *backbencher* na nusu nikawa Waziri. Sasa haya ni maelekezo yangu ya mwanzo kuyapata. Sasa nasikitika sana na nastaajabu sana wale wanaotaka kunitoa nje wakati hata hawajanielekeza. Kwa hivyo Mhe. Spika, hawatonitendea haki, kabla hawajanielekeza wanitoe nje, bora kwanza umuelekeze halafu umtizame je atafuata yale maelekezo au atachukua nafsi yake.

Mhe. Spika, Rais Obama ni muafrika wa mwanzo wa Marekani kuchaguliwa kuwa Rais na alipokewa kwa hisia mbali mbali wakati anapata Urais. Mimi ni mmoja kati ya mfuatiliaji mkubwa wa hizi habari za ulimwengu Mhe. Spika. Hali ya uchumi ilivyokuwa Marekani mpaka baada ya miaka mitatu kuwepo yeye wanafanya ile sherehe nusu kipindi bado hali ya uchumi hairidhishi kabisa Marekani, lakini hakutolewa, alipewa muda, na baada ya wananchi kumpa muda ni mwezi huu Mhe. Spika, wa Julai, inatangazwa rasmi kwamba Marekani inaongoza katika uchumi wake ulimwengu mzima na Rais ni yule yule Obama, muafrika. Je Rashid Seif ana kosa gani la kutopewa muda ikabidi arushwe dirishani, naomba Mhe. Spika, Wawakilishi watuvumilie sana, pale tunapokosea watukosoe, watuweke sawa lakini watupe muda ili tutekekeze yale malengo yetu.

Baada ya maneno hayo Mhe. Spika, kwa ufupi kabisa naomba kwanza niwataje kwa kuwashukuru na kuwapongeza wale wote walioichangia Wizara hii. Mhe. Spika, kwa *list* niliyonayo hapa 17 walichangia kwa kauli na 17 wengine walichangia kwa maandishi, hawa ni wa mwanzo. Wale ambao wameongezea mchango wao ni 4, kwa hivyo wote wote tunafanya idadi ya 38 waliochangia, nawashukuru sana.

Kwanza nampongeza sana na namshukuru Mhe. Panya Ali Abdalla Makamo Mwenyekiti wa Kamati aliyetoa maelezo ya Kamati pamoja na maelezo yake mwenyewe.

1) Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
2) Mhe. Hija Hassan Hija
3) Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
4) Mhe. Omar Ali Shehe
5) Mhe. Asha Bakari Makame
6) Mhe. Salim Abdalla Hamad
7) Mhe. Salmin Awadh Salmin
8) Mhe. Saleh Nassor Juma
9) Mhe. Hamza Hassan Juma
10) Mhe. Asaa Othman Hamad
11) Mhe. Mgeni Hassan Juma
12) Mhe. Subeit Khamis Faki
13) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
14) Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
15) Mhe. Hassan Hamad Omar
16) Mhe. Hamad Masoud Hamad

Wa maandishi sehemu ya kwanza:

1) Mhe. Marina Joel Thomas
2) Mhe. Thuwaybah Edington Kissassi
3) Mhe. Fatma Mbarouk Said
4) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
6) Mhe. Suleiman Hemed Khamis
7) Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi yeye alisema kwa maandishi na kauli; zote mbili alileta
8) Mhe. Rufai Said Rufai
9) Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
10) Mhe. Salma Mohammed Ali
11) Mhe. Farida Amour Mohammed

12) Mhe. Salma Mussa Bilali kwa maandishi na kwa kauli
13) Mhe. Abdi Mossi Kombo
14) Mhe. Nassor Salim Ali
15) Mhe. Kazija Khamis Kona
16) Mhe. Mlinde Mabrouk Juma
17) Mhe. Abdalla Juma Abdalla

Wengine ambao napenda niwapongeze kwa mchango wao ni Mhe. Mwanasheria Mkuu; Mhe. Othman Masoud Othman, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Omar Yussuf Mzee, Mhe. Issa Haji Ussi Naibu Waziri Miundombinu na Mawasiliano ninamshukuru sana kwa kunisaidia kazi na pongezi pekee nazitoa kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi; yeye amekuja hapa kwa madhumuni mawili, kwanza kuiunga mkono hii hoja tuliyonayo, lakini nataka niwaeleze Waheshimiwa kwamba mimi ninavyoichukulia ni kwamba ni nafasi aliyoitoa maalum kwa kuiunga Wizara na kuihakikishia jumuiya hii ya Wawakilishi na wananchi kwa jumla kwamba yupo pamoja na Wizara katika kutekeleza majukumu yake na kuona kwamba yanakwenda kama yalivyopangwa, yale ambayo tunayafanya sisi yuko katika mstari wa mbele katika kuiangalia.

Kwa hivyo anatoa *insure* kwa Wawakilishi kwamba yote yaliyochangiwa yuko pamoja na utekelezaji wake na ufuatiliaji wa utekelezaji wake.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba sasa niingie katika sehemu ndogo ambayo

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa masikitiko makubwa sana tena Mhe. Waziri katika majumuisho yake mimi hakunitaja, nimempelekea kwa maandishi, sasa sijui kama kapitikiwa au ndio kitabu chake cheusi hiki, na nikamuuliza kanambia kapokea mchango wangu kwa maandishi ukurasa mdogo sana lakini mzito.

Mhe. Mwenyekiti: Umemsahau kumtambua Mhe. Jaku Hashim ambaye ameleta mchango wake kwa maandishi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Naomba radhi sana Mhe. Mwenyekiti kutomtaja, nadhani ananipokelea radhi yangu na kila ambaye nilimsahau, sababu si madhumuni ya kusahau kama *chance* ni moja tu katika 38 basi inajulikana kwamba haikuwa kwa makusudi.

Mhe. Spika, mimi naingia katika michango ambayo bado haijapata majibu, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu suala la uratibu wa miradi ya maendeleo kufanyika makao makuu ya Wizara. Mhe. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepewa majukumu ya uratibu na usimamizi wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya serikali. Kazi za Idara hii hufanyika Unguja na Pemba kulingana na sehemu ya mradi husika unavyotekelezwa. Hata hivyo kwa kuzingatia hoja iliyotolewa, Wizara tayari imeshachukua hatua ya kuanzisha kitengo cha usimamizi wa miradi Ofisi Kuu Pemba ili kurahisisha kazi ya usimamizi wa miradi kwa upande wa Pemba. Kitengo hicho kitafanya kazi chini ya kitengo kikuu cha mradi kiliopo Makao Makuu.

Hoja ya mtu mmoja alidai haipingi hoja kuwa Katibu Mkuu ndiye aliyeelekeza, kwa hivyo Katibu madhali aliyeelekeza ile ndio hoja ambayo iliopo, mwengine aliyemwambia kwamba wewe usifuate, sasa yeye Afisa angelijiuliza Katibu Mkuu ndiye muendeshaji mkuu wa shughuli za Wizara ameshatoa kauli ndio hiyo. Kwa hivyo kauli ya mtu mwengine yoyote haisihi, kwa sababu Katibu Mkuu ndiye anayeendesha Wizara, kama kulitokezea mtu yoyote akamwambia usifuate kauli hiyo, hiyo itakuwa kauli ya binafsi wala haifuatwi.

Na kwa taarifa yako Mheshimiwa kabla wewe hujalisema hapa sisi baada ya kupata hiyo tulifuatilia, tulikwenda ziara maalum mimi, Katibu Mkuu na wakurugenzi wawili Pemba na kufuatilia kauli hiyo na tukaifanyia kazi na tukatoa indhari ya mwisho; kwamba hakuna kauli ambayo itapindukia Katibu Mkuu, Afisa mwengine yoyote wa chini.

Mhe. Saleh Nassor Juma na Mhe. Suleiman Hemed Khamis malipo ya fidia kwa wananchi. Kikawaida tathmini ya fidia za nyumba hufanywa na tathmini kutoka Wizara inayoshughulikia masuala ya Ardhi, na fidia ya vipando hufanywa na wataalamu wa Wizara ya Kilimo. Taratibu za Malipo ya fidia hizo hufanyika baada ya Wizara kujiridhisha na tathmini iliyofanyika. Malipo ya fidia hizo hufanyika kwa kadri ya hali ya upatikanaji wa fedha. Mimi binafsi baada ya kuona kwamba kuna tatizo kubwa la ulipaji fidia katika ujenzi wa barabara hasa hizi zinazotolewa mkopo, nimezungumza na uongozi wa ADB waliokuja kunitembelea ofisini na nimewapa rai yangu kwamba ADB iangalie uwezekano wa kuingiza *component* ya ulipaji fidia ndani ya mkopo, kwa sababu tatizo kubwa ni kwamba mkopo unaotoka ADB na kwengineko ukiachilia mbali ule msaada uliotolewa na MCC hawataki kuingiza *component* ya kulipiwa fidia ya wananchi, wanasema hii ni *component* ya serikali, lakini kwa sababu sisi tunahitaji maendeleo ya barabara tunakubali ile na baadae kunakuwa na mkwamo wa kulipa fidia.

Mwezi uliopita wa Julai, ilikuja hapa timu ya African Development Bank na wamekubali kulichukua shauri letu kulipeleka Makao Makuu yao kwenda kujadiliwa, kwamba ndani ya mkopo ule wa ujenzi wa barabara iwemo *component* ya ulipaji fidia, ili mradi ukiwekwa saini tu tayari ujenzi unaanza. Kwa hivyo tunalishughulikia kwa ukamilifu Mhe. Spika, katika kiwango hicho.

Kuhusu fidia ya vipando kwa wananchi wa Vitongoji kwa ajili ya kupitisha *line* ya umeme nimeshalijibu suala hili katika bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati binafsi yangu na niliwaahidi kwamba mara baada ya bajeti hii mwezi wa Agosti basi watu hawa watapatiwa malipo yao, kwa sababu sisi Mhe. Spika, kwa hili tulipeleka umeme wa dharura Kware ya Vitongoji ambayo inachukua kasha ya kokoto na mtambo wa lami; ilikuwa inatumia majenereta. Majenereta yote mawili yalifeli kwa wakati mmoja na yakawa hayatengenezeki, kwa hivyo tulitumia hali ya dharura ya kupeleka umeme na baada ya kupeleka umeme ndio kukawa na malipo ya fidia kwa wenye vipando. Lakini hili tunalichukua kwa nguvu zote na *inshaallah* katika kipindi kifupi kuanzia baada ya kupita hii bajeti, naomba tuipitishe wananchi hawa tutawapa fidia zao wala hawatakosa hata mmoja.

Mhe. Spika, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Rufai na Mhe. Hamad Masoud Hamad walizungumzia kuhusiana na ujenzi wa barabara za Pemba ikiwemo Gando/Wete na Konde/Wete. Mheshimiwa kama ilivyozungumzwa kwamba sisi kwa upande wetu tunajitahidi kulipa deni. Barabara hizi kama nilivyokwisha eleza katika maelezo ya mradi, ulipangwa kutekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilipangiwa kujenga barabara za Wete/Gando na Wete/Konde kutokana na fedha ziliopo. Awamu ya pili ya mradi huu utahusisha barabara ya ChakeChake/Wete. Utekelezaji wa mradi huu ulichelewa kuanza kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo kuchelewa kumpatia mkandarasi eneo la kufanyia kazi kutokana na taratibu za uondoshwaji wa huduma za jamii, kuchelewa kumlipa mkandarasi kwa wakati kwa upande wa serikali na wafadhili wa mradi huu.

Pamoja na kuwepo kwa mgogoro baina ya kampuni ya MECCO Ltd. na mbia wake kampuni ya COGEL mwanzoni mwa mradi, mgogoro huu ulichukua muda mrefu kutatuliwa na kusababisha malimbikizo mengi ya malipo. Aidha sababu nyengine ya kuchelewa mradi huu ilikuwa ni kumaliza muda wa mkataba wa msimamizi wa mradi ambapo ulichukua muda mrefu kwa mfadhili kukubali kuongeza muda. Hali hii ilipelekea pia mshauri kuondosha wafanyakazi wake kutokana na kutolipwa madai yake, hali hii ilimuathiri

mkandarasi kwa kutowepo msimamizi wa kuthibitisha nyaraka za malipo yaani *certificate* za kazi zilizofanyika.

Kutokana na hali hiyo mkandarasi aliamua kusimamisha kazi mpaka atakapopata malipo yake yote. Madai ya MECCO yalikuwa kama ifuatavyo, kutoka SMZ inaidai pesa za Tanzania 699,314,805 na dola za kimarekani 455,028. BADEA ilikuwa inadaiwa 1.578 milioni USD na *Saudi fund* 1.25. Sasa hizi zote zimeshalipwa kwa wakati huu.

Wizara katika mwezi wa Aprili 2013 ilizungumza na msimamizi wa mradi na kumuomba arudi eneo la kazi kwa ajili ya kuthibitisha hati za malipo ambaye alikubali kufanya hivyo na hatimaye jumla ya USD 2.74 milioni tayari zimeshalipwa na BADEA pamoja na *Saudi fund* tarehe 17 Juni, 2013.

Aidha Wizara mwishoni mwa wiki iliyopita ililipa jumla ya shilingi 1.4 bilioni kati ya 3.1 bilioni zinazodaiwa ikijumlisha malimbikizo ya riba na mradi huo na kukubaliana na mkandarasi huyo baada ya kupata ithibati ya Wizara ya Fedha kukamilisha deni la shilingi 1.7 bilioni ndani ya mwezi wa Agosti. Kwa hatua hiyo iliyofikiwa mkandarasi huyo tayari ameahidi kuanza kazi mara moja za ujenzi wa barabara zilizobakia na kukamilisha kazi ndani ya kipindi cha miezi mitatu hadi minne ijayo.

Kuhusu hoja ya Mhe. Suleiman Hemed Khamis kuharibiwa nyumba za wananchi katika ujenzi wa barabara ya Wete/Chake. Naomba kumuarifu Mheshimiwa kuwa Wizara bado haijaanza utekelezaji wa barabara hiyo.

Kuhusu hoja ya mkopo wa *Saudi fund* serikali ya SMT tayari imeshatiliana saini mkopo wa jumla ya dola za kimarekani milioni kumi na juhudi za kupata fedha kwa *SAUD FUND* zinaendelea. Ujenzi huu unatarajiwa kuanza mara zitakazopatikana fedha.

Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Omar Ali Shehe na Mhe. Ismail Jussa barabara za Kaskazini Pemba MCC, tathmini na malipo barabara ya Kaskazini Pemba zimesimamiwa na MCAT nyaraka zote na taratibu zote zilifanywa na MCAT kutokana na tathmini iliyofanywa na taasisi hiyo iliyo chini ya Wizara ya Ardhi chini ya usimamizi wa MCAT. Taarifa ambazo Wizara imezipata ni kuwa kwa vile viwanja vilivyopimwa kihalali mfadhili alilipa Tanzania shilingi 5000 kwa *square metre* na vile ambavyo havijapimwa kihalali mfadhili alilipa Tanzania Shilingi 1000 kwa *square metre*. Jumla ya Tanzania shilingi 150,000,000 zilizotengwa kwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya mradi huu zimekusudiwa kulipia madai ya athari zinazojitokeza nje ya eneo la ujenzi yaani *road reserve* wakati wa ujenzi unaoendelea ambazo ni MCAT hawatalipa.

Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Salma Mussa Bilali na Mhe. Hassan Hamad Omar, uimarishaji wa kiwanja cha ndege cha Pemba. Mradi wa uimarishaji wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba unahusisha uwekaji wa taa za kuongozea ndege na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu na huduma za abiria na mizigo. Uwekaji wa taa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara ilianza taratibu za kumpata mkandarasi wa kufanya kazi za uwekaji wa taa za kuongezea ndege ambapo jumla ya kampuni mbili tu ziliwasilisha zabuni hizo. Kwa mujibu wa sheria ya manunuzi Wizara haikuweza kuendelea na mchakato huo, hivi sasa Wizara inazifanyia marekebisho nyaraka za zabuni ili ziweze kuwavutia wazabuni wengi zaidi. Hii ni kutokana na taratibu za *procurement* ya hapa Zanzibar kwamba kampuni angalau ziwe tatu ndio mnaweza mkaifungua tenda.

Kuhusu upembuzi yakinifu na usanifu wa huduma za abiria na ndege katika kiwanja cha ndege hicho, Wizara tayari imeanza taratibu za kumpata mshauri elekezi wa kufanya kazi hiyo ambapo imetoa *request proposal* kwa kampuni saba za kimataifa. Ni matarajio yetu kuwa kampuni hizo zilizoombwa kuwasilisha maombi yao zitakuwa zimewasilisha maombi yao ifikapo tarehe 14 Agosti, 2013.

Napenda niwahakikishie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kama mimi ni Waziri basi hata Mhe. Rais wetu Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein *priority* yake ni kutiwa taa katika kiwanja cha ndege cha Pemba. Hiyo ni uhakika kwa sababu ya kauli yake wazi wazi tunazungumza katika kikao. Kwa hivyo mimi siwezi tena kuiepuka kauli hiyo hata kama mimi nitakuwa sitekelezi lakini hiyo ndio kauli ya Mhe. Rais na lazima niifuatilie na iweze kufanyika.
Kwa hivyo msiwe na wasiwasi, pamoja na kwamba mimi nalaumiwa kwamba nilikuwa nikitetea lakini sasa hivi nahakikisha kwamba bado ninaitetea lakini upatikanaji wa fedha, upatikanaji huo wa kandarasi waliokosekana kwa kutimiza ile idadi ya *procurement act* ilisababisha kukwama katika 2012/2013. Lakini *inshaallah* katika kipindi hiki cha 2013/2014 tutahakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa na kiwanja cha ndege cha Pemba kinakuwa na taa kama ambavyo ingepaswa kuwa.

Mheshimiwa Uwanja wa ndege wa kimataifa jengo la *Terminal II* namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha Mipango na Uchumi akitoa ufafanuzi wake akiwa yeye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu iliyoundwa na serikali. Na kwa nini serikali iliunda kamati kutokana na umuhimu na uzito wa ile kazi, kutokana na umuhimu na uzito wa ule mradi kwamba utakaoipa hadhi Zanzibar. Kwa hivyo kamati inaongozwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo

akiwa ni Mwenyekiti, mimi msaidizi wake, kuna na Mhe. Said Ali Mbarouk; Waziri wa Habari Utamaduni kwa sababu yeye amechukua nafasi kubwa ya utalii. Sasa kiwanja cha ndege vyovyote kitakavyokwenda utalii nao ni sehemu muhimu ya kuushughulikia. Kwa hivyo serikali imemuingiza yeye kwamba ana nafasi kubwa pale ya kuona kwamba zile shughuli zinakwenda. Mwanasheria Mkuu yumo katika kamati hii, sasa angalia uzito wa ile kamati iliyoundwa kulishughulikia hili suala pamoja na Makatibu Wakuu wawili wa Fedha na wa Wizara yetu, na *DG* wa *Airport*. Yote hayo ni kamati ambayo imeundwa na inaendelea na kazi yake. Kwa hivyo napenda nimshukuru Waziri na tuhakikishe kwamba hilo suala linashughulikiwa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na Mhe. Omar Ali Shehe kutowasilishwa kwa taarifa zilizotakiwa na PAC. Kwanza hili mimi binafsi naliombea radhi kwamba kama lilitokezea, hivyo naomba radhi sana na nawataka Wajumbe waelewe kwamba mimi nilikuwa ni sehemu ya hii, kwa sababu nilikuwa sina taarifa nalo ukamilifu, naliombea radhi na nawahakikishia kwamba tutashirikiana na Kamati ya PAC kuona kwamba kila *document* sio hii tu kila *document* inayotakiwa iliyoko Wizarani inapatikana kwa kamati hii, kwa sababu ndio madhumuni ya Kamati kuchunguza, isipokuwa tu hivi sasa tumo katika *transition* kutokana na mambo tofauti yaliyotokea ikiwemo kampuni ya *PHILTEX* kubeba ile lawama ya kusajili meli za Kiirani ambazo zimekataliwa katika dunia, kwa hivyo sisi tupo katika *transition* sasa hivi ya kuondokana na hili, na mchakato huu na nyinyi tutawaomba tushirikiane wakati ule wa kuondokana mahesabu yatizamwe uzuri ili nayo Serikali ione pahali gani ipo. Kwa hivyo kupitia CAG, kupitia PAC tutashirikiana kikamilifu ili suala hili liende kwa ufanisi kabisa. Sisi hatuto-*deal* tena na kampuni hii katika siku zijazo.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kuhusu kurudishwa kazini kwa mfanyakazi aliyetuhumiwa. Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilipokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora yeye kutuarifu juu ya mabadiliko ya viwango vya wastaafu wa Wizara yetu. Wizara baada ya kupokea taarifa hiyo iliunda kamati ya kuchunguza suala hili ambapo iligundua kwa njia moja au nyengine mfanyakazi anayetajwa alihusika katika kadhia hiyo. Wizara iliwasilisha hili Tume ya Utumishi Serikalini pamoja na vielelezo vyote kwa barua yenye kumbukumbu Namba *MOIC/M140/C5/VOL.II/50* ya tarehe 10/8/2012 kuomba muongozo na hatua za kuchukua kuhusiana na suala hili lililojitokeza.

Mhe. Spika, Tume ilijibu kwa barua yenye kumbukumbu nambari *TUS/OR/C/WMMM/20/3/17* ya tarehe 6/3/2013 iliyomtia hatiani muhusika kwa kosa hilo na kuagiza Wizara impe adhabu ya kinidhamu muhusika chini

ya kifungu nambari 82.1(a) na (b) cha sheria ya Utumishi wa umma nambari mbili ya mwaka 2011, kwa kosa la kutokuwa muaminifu na kufanya makusudi kubadilisha kumbukumbu za watumishi hawa waliostaafu ambapo kungepelekea kuitia Serikali hasara. Kifungu hicho kinampa mamlaka Katibu Mkuu kutekeleza na kutoa adhabu kwa makosa yaliyoelezwa katika jadweli la pili yaliyofanywa ndani ya Ofisi kwa kosa la udanganyifu; la kwanza ni kupunguzwa mshahara au kuteremshwa cheo au kusimamishwa kazi kusubiri uchunguzi.

Mhe. Spika, kutokana na kosa hilo muhusika alipewa adhabu ya kushushwa cheo ya kutoka Msaidizi Afisa wa Utumishi kuwa Msaidizi Msamamizi wa Barabara kanda ya Kaskazini Unguja. Hata hivyo napenda kutoa ufafanuzi kwamba adhabu hiyo imetolewa na Wizara kwa kuzingatia mikataba yake katika kutoa adhabu ya kinidhamu kisheria, lakini haizuii mamlaka nyenginezo za kisheria kutoa adhabu kwa mujibu wa makosa ya kijinai.

Mhe. Spika, hichi kipande hichi Mhe. Naibu Waziri alinisaidia kazi sana namshukuru kwa masuala aliyoyajibu. Sasa ninakwenda katika masuala ya mamlaka ya viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, kabla sijajibu moja moja napenda niseme hivi. Kwa sababu kumetolewa malalamiko mengi kuhusiana na utaratibu wa kuendesha kiwanja cha ndege, baadhi ya masuala ameeleza Mwanasheria Mkuu, lakini niungane naye, na napenda niseme kwamba mimi binafsi pamoja na kwamba nilikuwa nafuatilia na kuna mambo mengi mimi nimeshayasawazisha lakini napenda niwahakikishie Wawakilishi wote kwamba nitaendelea na juhudi na nitaongeza juhudi zaidi za kuona kwamba sio Mamlaka ile tu lakini mamlaka zetu zote zinaendeshwa kwa taratibu na kama kuna tatizo lolote litakalojitokeza basi mimi nitalivalia njuga kulitekeleza. Ila Mamlaka zile napenda kuwatanabahisha tu Wawakilishi kwamba zinaongozwa na Bodi za Wakurugenzi, kwa hivyo kuna *management*, kuna Bodi ya Wakurugenzi halafu ndio anafika Waziri. Sasa naomba sana Wawakilishi mnapokwenda katika Kamati mujaribu sana kama inavyowezekana kukutana na Mabodi ya Wakurugenzi vile vile badala ya kukutana na *management* tu peke yake isitoshelezeke, fanyeni utaratibu mukutane na mabodi ya wakurugenzi ili zile hisia zenu na maelekezo yenu muwape na wale bodi ya wakurugenzi, kwa sababu *management* inakuwa ni wadogo mbele ya bodi ya wakurugenzi.

Mhe. Spika, mimi binafsi napenda nitoe *experience* yangu. Nilivyochaguliwa katika Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi, wenzangu ni mashahidi, tulikutana na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme, tukakutana na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Bandari na mambo yetu yalikwenda vizuri tukafahamiana na wakajua kwamba nini tunachozungumza, kwa hivyo badala

ya kamati kwenda katika Mamlaka tu, kwa sababu mamlaka ni mas-ul kwenye Bodi ya Wakurugenzi watake *forum* na mabodi ya wakurugenzi ili waweze kupata zaidi na kutoa maelekezo zaidi kwa sababu wako ni mas-ul kwa hili Baraza la Wawakilishi.

Hivyo nasema pamoja na majibu tutakayotoa hapa bado ikiwa kuna malalamiko tutayafuatilia ili kuona kwamba hali inarekebishika na hali inakwenda katika hali ya utulivu. Mamlaka ilitoka kutoka Idara kwa sheria tuliyoipitisha wenyewe hapa ikawa ni mamlaka, kwa hivyo mabadiliko lazima yapo na kama alivyosema Mwanasheria Mkuu pale kiwanja kimebadilika lakini yako mambo ambayo yatakuwa yanakwenda vizuri na yako mambo ambayo yatakuwa hayaendi vizuri, lakini ni juu yetu kushirikiana kuona kwamba kila siku tunayasahihisha na kuyaweka katika nafasi yake.

Mhe. Spika, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu malipo ya maegesho ya magari wanayolipwa madereva wanaohusika katika kiwanja cha ndege cha kimataifa. Utaratibu uliowekwa na Mamlaka ya viwanja vya ndege kuhusiana na magari yanayoingia ndani ya uwanja; ni kwamba gari zote za binafsi zinatakiwa kulipia zinapoingia ndani. Utaratibu huu umepata baraka za bodi ya mamlaka ya viwanja vya ndege Zanzibar. Kuhusu magari ya wafanyakazi wanalipa kama magari mengine isipokuwa wao hupata punguzo maalumu.

Mhe. Spika, sasa hapa tulipata maelezo kwamba na hawa wafanyakazi waonekane kwamba ni sehemu ya kazi hili tutalichukua tulipeleke kunakohusika na kuona kwamba jee wafanyakazi badala ya kwenda huko kulipa jee kutakuwa na njia gani ambazo watakuwa pengine na *permit* zao, ili wale wafanyakazi nao wanufaike na ile sehemu yao ya kazi. Hili tutalichukua ni suala la kutoa *order* mara moja tukakae na *management* na bodi tuzungumze ili tuone sisi tunafikia wapi.

Mhe. Spika, malipo ya ada ya matumizi ya ukumbi wa viongozi mashuhuri (VIP). Mamlaka imeweka utaratibu wa malipo ya ada ya matumizi ya kumbi hizi kwa viongozi wanaotumia ukumbi wa watu mashuhuri. Kutokana na muongozo wa Serikali uliotolewa, utaratibu huu wa malipo kwa viongozi unatumika katika viwanja mbali mbali duniani kwa ajili ya uboreshaji wa huduma katika eneo hilo. Mfano wa kiwanja cha ndege cha Oliver Tambo cha Afrika ya Kusini, malipo ya VIP ni USD 100. Hata hivyo mimi nikiwa ni Waziri, na Waziri ni mshauri wa Rais, napenda niwahakikishie kwamba hili nitalichukua nipeleke ushauri huko juu na nitaomba liangaliwe upya kwa sababu ya malalamiko ambayo wametoa Wawakilishi na tuone kama kuna *correction* yoyote itakayofanywa ili tuweze kurahisisha na kuona kwamba hali inakwenda vizuri.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Salmin Awadh na Mhe. Shadya na Mhe. Hassan, malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya viwanja vya ndege. Malalamiko yamesikikana, Waziri anapitisha *scale* ya mishahara na sio mshahara wa mtu mmoja mmoja, kwa hivyo inawezekana kwamba matatizo haya yalijitokeza na kwa kushirikiana na Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, tumesema tutalishughulikia suala hili,mishahara ile tutaipitia upya na kuona kwamba pahali ambapo pana kasoro, pahali ambapo pana upendeleo basi hatutosita kuchukua hatua zinazofaa. Hili tunakuhakikishieni kwamba tutalifanya, na kwa sababu silifanyi peke yangu Mhe. Waziri wa Utumishi na Utawala Bora ananisikia ni suala letu pamoja na Mamlaka ya uwanja wa ndege, ili pale ambapo pana kasoro tutalisawazisha kwa pamoja na tutakuja kutoa maelezo hapa katika kipindi ambacho kinafaa.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan, Mhe. Hamza Hassan Juma, walizungumzia hili suala la *architect* limeshazungumzwa na Mwanasheria Mkuu naheshimu maelezo ya Mwanasheria Mkuu na naamini mmeyasikia uzuri kwamba kisheria ameshajitoa, sasa na yeye hiyo sehemu ya pili muliyoichangia bado ameshapata sehemu moja anaifuatilia na sehemu nyengine ili kuona kwamba hilo jambo linafanyika. Na amri hii si ya Wizara ni ya Serikali, kwa hivyo naamini kwamba hili jambo ni *serious* na linashughulikiwa kikamilifu naomba utukubalie hivyo.

Mhe. Spika, Mhe.Asha Bakari Makame amezungumzia kuhusu fidia ya familia ya ndugu Majaaliwa katika eneo la Uwanja wa Ndege. Tathmini ya eneo la Ndugu Majaaliwa iliyopo Uwanja wa Ndege wa Zanzibar tayari imeshafanywa, kinachosubiriwa kwa sasa ni malipo kutoka Serikalini. Kwa hivyo hatopunjwa na yeye mwenyewe anaweza akafuatilia kuona ni tathmini kiasi gani ili aweze kujiridhisha.

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh na Mhe. Asaa Othman Hamad walizungumzia kuhusiana na ujenzi wa *arrival lounge*. Mhe. Spika, *arrival lounge* iliyopo kwa sasa ni ndogo kuchukua abiria wote wa daraja la kwanza na daraja la kawaida, hivyo katika mipango yake ya mwaka 2013/14 Mamlaka imekusudia kutanua eneo la abiria wanaowasili kwa kuwatenganisha abiria wa daraja la kwanza na daraja la kawaida. Bado tunaendelea kusubiri ujenzi wa *terminal* mpya ambao utaimarisha zaidi huduma hii.

Mhe. Spika, kulalamikiwa kwa Mamlaka katika uendeshaji wa viwanja vya ndege. Malalamiko ni hoja ya msingi, hata hivyo mamlaka inaongozwa na sheria na taratibu za usafiri wa anga za kitaifa na kimataifa. Ndani ya sheria

hizo zipo za usalama na kamati ya huduma na nyenginezo ambapo wadau wote wakiwemo masheha, *tour operators, taxi drivers, airlines* wanakutana na kutoa malalamiko yao kupitia kamati hizi. Kwa mantiki hiyo nafasi ziko wazi kukaribisha malalamiko tofauti yanayohusu mambo ya viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, mimi ni shahidi kwamba ndani ya kipindi hiki wakati mamlaka inajiimarisha katika kuweka usalama pale kiwanjani, kulikuwa na malalamiko kwamba wale *operators* wa shughuli mbali mbali walikuwa wanatumia ile fursa ambayo ilikuwepo katika Idara ya kupata vitambulisho kadri ya mtu anavyotaka. Sasa kuna utaratibu wa kwamba kila *operator* kama ni *airline* au nyengine kuna watu maalum kama ni wawili waliopewa vitambulisho na ni *non- transferable,* hawezi akakichukua kitambulisho kile akampa mtu mwengine kukitumia kwa sababu ya kulinda usalama wa kiwanja, hichi ni kiwanja cha kimataifa, haiwezekani kwamba mtu akitaka kitambulisho anataka kuingia ndani apewe tu.

Kwa hivyo kuna baadhi ya mambo mimi nayaona kwamba yalikuwa yanafanyika lakini tulitaka yafanyike kwa utaratibu zaidi na kwa ustaarabu zaidi badala ya kuwa labda kwa kuripukiana. Tunaomba wananchi watuvumilie, tukishaingia uwanja wa ndege, tukishaingia Bandarini si Zanzibar tena, na mimi nataka tufahamiane ni kimataifa na ndio maana hivi sasa bandarini kunatakiwa kuwe na hali ya usalama mkubwa kwa sababu ile ni bandari lakini ni bandari ya kimataifa, kwa sababu kuna meli pale za kimataifa zinakuja pale, kuna mizigo inayopakiwa ambayo inakwenda nje ya nchi, sasa ile bandari inatakiwa vile vile kama *airport* kuwa na hali ya usalama wa hali ya juu.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia kuhusu kuzuiwa hisa kwa wachukuzi waliopo uwanja wa ndege. Mamlaka haina mkataba na kitengo chochote kinachohusiana na wachukuzi waliopo uwanja wa ndege. Mamlaka tayari imejipanga kuweka vigari vya kutosha kuwahudumia wageni wote wanaoondoka na wanaowasili. Katika kuviendesha vigari hivyo Mamlaka itateua watu wachache kwa ajili ya kuvisimamia vigari hivyo pamoja na kuwahudumia wagonjwa, walemavu na wazee wasiojiweza.

Mhe. Spika, Mhe. Mwajuma Faki Mdachi yeye kazungumzia ukaguzi wa abiria hadharani katika viwanja vya ndege. Kikawaida kila kituo cha ukaguzi huwa na sehemu ya ukaguzi wa faragha. Katika uwanja wa ndege wa Zanzibar ukaguzi wa faragha unafanyika katika mashine ya pili iliyopo ndani ya jengo la abiria. Tunakiri kwamba mashine ya nje ya ukaguzi bado haijawekwa sehemu ya ukaguzi wa faragha, tutalifanyia kazi suala hili si baada ya muda mrefu ni kwa muda mfupi.

Mhe. Spika, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa alizungumzia kuhusu ndege ndogo ndogo kurushwa na rubani mmoja. Kikawaida idadi ya marubani wanaohitajika kuongoza ndege kwa wakati mmoja hutegemea mazingira mbali mbali ikiwemo uzito wa juu wa kuruka ndege husika, idadi ya abiria, muundo wa ndege husika, wingi wa shughuli za kazi zinazohitajika katika kuiongoza ndege na kuirusha ndege husika. Kulingana na kanuni za usafiri wa anga za hapa nchini za mwaka 2012 yaani *aircraft operation regulations* ambazo zinakidhi matakwa ya kanuni za kimataifa ISRP, ndege yenye uzito usiozidi *kilogram* 5700 kuruka na kuwa na viti visivyozidi tisa huruhusiwa kuongozwa na rubani mmoja, na zile zenye uzito wa zaidi ya huo na viti zaidi ya tisa huhitajika kuwa na rubani wasiopungua wawili.

Mhe. Spika, kwa kuwa ndege nyingi zitumiwazo na kampuni nyingi hapa nchini ni ndogo na zenye uzito usiozidi *kilogram* 5600 na viti visivyozidi tisa, sheria na kanuni za nchi yetu zinaruhusu ndege hizo ndogo kurushwa na rubani mmoja wakati wa mchana.

Mhe. Spika, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu yeye alichangia kuhusu changamoto za kutowepo kwa kipaza sauti na baadhi ya vifaa vyengine katika viwanja vya ndege. Tayari Mamlaka imezingatia changamoto hizo na zinakusudiwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu yeye alizungumzia kuwa na wasi wasi wa bei ya ujenzi wa uzio *kilometre* moja katika uwanja wa ndege wa Pemba. Taratibu zote za ujenzi wa uzio zilifuatwa kwa kumpata mkandarasi ambaye alifanya mapitio ya gharama za ujenzi huo. Ujenzi wa uzio ulilazimika kujengwa kwa zege na waya maalumu. Wizara iliridhika na kazi iliyofanyika tokea mwaka 2009 hadi sasa hakuna uhalifu wowote uliojitokeza.

Mhe. Spika, kuhusu Mamlaka ya Usafiri Baharini. Mhe. Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na Mhe. Marina Joel Thomas walitoa ushauri kupatiwa wataalamu wa Mamlaka ya usafiri baharini ZMA, vifaa vya uokozi, ukamilishwaji wa kanuni na kuijengea uwezo Mamlaka ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, ushauri tumeupokea na kwa taarifa ya Baraza hili tukufu, mimi sasa hivi ninazo mezani kanuni tano za ZMA ili kuzipitia na kuziwekea saini, ikiwemo uajiri wa mabaharia na taratibu zake, makaazi ya mabaharia ndani ya meli na taratibu zake, shughuli yote ya upimwaji wa afya, shughuli za usalama, hivyo hizi kanuni sasa hivi ziko tayari na hakuna tatizo mimi nimeshazipitia mara baada ya bajeti hii zitaanza kufanya kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Hamza Hassan na Mhe. Saleh Nassor Juma walizungumzia kuhusu kutosajiliwa meli za *land craft* kutobeba abiria ikiwemo hii ya MV Khadija na Buraq 3. Mhe. Spika, sote ni mashahidi kuwa mwezi wa Septemba 2011, meli ya aina hii *land craft* iitwayo MV Spice Islander ilipinduka na kusababisha vifo vya watu kadhaa. Kufuatia ajali hiyo, Serikali ilichukua hatua za dharura kusimamisha meli zote za *land craft* kuchukua abiria, hata hivyo marekebisho ya sheria ya usafiri baharini kifungu 17(a) kimepiga marufuku meli za aina ya *land craft* ambazo tangu asili yake hazikujengwa kwa madhumuni ya kubeba abiria.

Mhe. Spika, naomba nielezee kidogo hapa. Watu wale ambao walioambiwa wamekwenda Tanga, taratibu za usajili wa meli yoyote itakayosajiliwa na ZMA, kama itachukua abiria na mzigo, itachukua abiria au itachukua mzigo lazima wale waende kuikagua, kwa hiyo kukaguliwa kwa meli hiyo iliyokuweko Tanga hakukumaanisha kwamba ikija hapa ndio itapewa kibali cha kuchukua abiria, wale walikwenda kujitosheleza kwamba ile meli ina viwango vya kuweza kusajiliwa na daftari la Zanzibar Maritime Authority. Mpaka sasa hivi, msimamo uliopo meli za *land craft,* sisi kwa sababu tuna bahari ya *open sea*, Mhe. Spika, katika kuitafuta ile yetu ya Zanzibar mie binafsi nimepata elimu ya ziada katika huu umri nilionao kwamba meli inapoundwa haihitaji kumuajiri mshauri elekezi; *consultant* ni *automatic*, ukienda kuunda meli *automatic* mshauri elekezi lazima awepo ambapo hapa kwa umaarufu wanajulikana kwamba *Lloyds* ya Uingereza, hiyo lazima iwepo, wewe ukitaka usitake huyo yupo tu, yeye atatizama viwango vyote na ndio yule mwenye kampuni hatoruhusiwa na sheria za IMO kutoa ile meli kama hawajawashirikisha wale wakatoa viwango vyake.

Mhe. Spika, sasa meli za kweli kununua ambazo zimetengenezwa nje ya utaratibu huu wa kuchukua abiria ndio matatizo yake hayo, lakini la pili meli tulivyokwenda kuundisha sisi inapimwa mpaka vina vya maji, mawimbi, pepo zinazopiga, bahari gani, kwa hivyo zote *specifications* zimo. Sasa unapokwenda kununua meli nje inawezekana meli ile ilikuwa ikisafiri katika mto, inawezekana meli ile ilikuwa ikisafiri katika ziwa, au ikisafiri katika *inland seas*, kuna bahari nyengine zimejifunga zimo ndani tu hazina dharuba, lakini unapokuja hapa ukakumbana na mkondo wa Nungwi ni *open sea* hiyo, kwa hivyo mambo yote hayo yanaangaliwa.

Sasa nawaomba sana wenye vyombo ambao wanataka kusajili bado wafuate sheria ile, ZMA hivi sasa ilivyojipanga haitaki fedha ya mtu, haitaki bahasha ya mtu, una chombo chako kifuate sheria usajiliwe. Na mimi naamini mia juu ya mia, kwa hiyo tumesema sisi MV Khadija haijasajiliwa lakini ipeleke maombi ya kusajiliwa meli ya mzigo, haichukui hata saa 24 itakuwa imeshasajiliwa kwa sababu imeshatizamwa. Lakini wamiliki ya meli hii

wanashikilia kwamba lazima wasajiliwe kuchukua abiria, jee tukawapeleke tena Nungwi?

Mhe. Spika, sisi Wawakilishi ndio tuliopiga kelele hapa hapa ilipozama meli na ndio kilichopelekea ndugu yetu kujiuzulu Waziri, baada ya kuzama ya pili, mimi binafsi siwezi nikafanya jambo hilo kabisa kabisa. Nawaomba sana kwa hili mulifuate. Hii meli jambo la pili hiyo MV Khadija ikisajiliwa itakwenda wanavyosema Dar es Salaam na Tanga. Mkurugenzi wetu sisi amefuatilia SUMATRA hawaipi usajili watakwenda Bandari hiyo wafanye vipi, wao wameshasema SUMATRA hawa kama nyie mtawakosesha sisi hatuwapi usajili, kwa sababu haina viwango hivyo vinavyotakiwa. Sasa sisi Wawakilishi kushikilia tu ili tukaue watu mimi simo! Lazima tufuate utaratibu na sheria tulizojipangia sisi wenyewe, kwa sababu sisi tunasikia kulikuwa na meli zikiitwa Al Sayd, Said Khalifa tokea huko, meli ya Serikali hata moja haijawahi kuzama hapa na watu.

Mhe. Spika, mimi nakumbuka miaka ya 1980 MV Jamhuri ilitoka Pemba kuja Unguja ikakaa upande hala hala mpaka ikafika Unguja lakini haikuzama kwa sababu ina mkuku, lakini haya ma-*land craft* tulichukua kwa sababu ya dharura wakati ule ulikuwa usafiri hakuna, sasa wawekezaji wameshaleta vyombo vyao nyie leteni vyenye mkuku vichukue abiria hapana atakayezuiwa.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe alitaka kujua kuhusu kampuni ya PHILTEX kutoajiri mabaharia wa Zanzibar katika meli zilizosajiliwa na kampuni hiyo. Mhe. Spika, katika mkataba wa mwaka 2007 ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilisaini kwa kampuni ya PHILTEX, suala la kuajiri mabaharia wa Zanzibar halikuwemo, na kwenye *open registry* inampa uhuru mwenye meli kuajiri mabaharia kutoka nchi yoyote. Hata hivyo Wizara kupitia Mamlaka ya usafiri baharini itafanya mazungumzo na wakala atakayekuwepo wakati ujao kuingiza kipengele hiki na sasa Zanzibar kwamba itakapoanza mkataba na huyu mpya mshauri elekezi mpya na mshauri mpya itaanza kutia kipengele hicho. Kwa hivyo mimi naamini kwamba haya ndio mabadiliko, tumeshaona kwamba kule kweli kulikuwa na kasoro, kweli mkataba ule ulikuwa na kasoro haikuwahi kuingiza kipengele hicho, vipi tutakuwa na *open registry* bila ya sisi wenyewe kunufaika kiajira, ile ni kasoro na sisi tunaikubali, lakini tunawahakikishia haitotokea tena na mkataba tutakaotia tena lazima tutam-*commit* kwamba *registration* itakayofanyika kuanzia kipindi hicho cha mkataba basi lazima kiwe na nafasi za ajira kwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, kuhusu mapato ya meli za kimataifa. Hili suala liliuliza na yeye na pamoja na Mhe. Jussa. Mhe. Spika, utaratibu wa malipo katika usajili wa

meli ni kuwa meli zinalipa kutokana na uzito wake na sio idadi au wingi wa meli hizo. Idadi ya meli 406 zilizosajiliwa kuanzia mwaka 2008 hadi 2013 baadhi ya meli hizo zinatokana na usajili wetu na nyengine ni zile za Iran ambazo zilitolewa, na hivi sasa meli tulizonazo katika daftari letu ni 179.

Mhe. Spika, naomba niingize kabisa hizo idadi za meli ni kama hivi ifuatavyo: Katika hizo 129 ambazo zilisajiliwa meli 60 zimehamia katika usajili wa taifa jengine, meli 159 zimeuzwa, meli 33 zimefutiwa usajili kutokana na kujihusisha na biashara na Iran. Kwa hivyo, hadi kufikia mwezi wa Julai, 2013 meli zilizobaki katika usajili wa daftari letu ni 179, hii ndio idadi sahihi na sio 429 kama ambavyo ilidaiwa.

Kuhusu malipo ya mwaka, *annual tonnage fees* sio kweli kwamba kwa kila meli inalipia USD elfu kumi, kwa mujibu wa utaratibu wa kimataifa na kanuni zetu za meli zinalipa kwa mujibu wa ukubwa. Mfano, meli yenye ukubwa kufikia tani 499 inalipa Dola za Kimarekani 150 kila mwaka, meli yenye ukubwa wa tani elfu 10 na kuzidi inalipa kuanzia dola 1200 na kuendelea.

Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iliingia mkataba na Kampuni ya *Filtex* mwaka 2007. Katika kipindi chote mapato yalikuwa yakiingia katika *account* ya serikali inayosimamiwa na Wizara ya Fedha. Kuanzia mwezi wa Juni, 2013 *account* hiyo imekabidhiwa rasmi kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini yenye nambari 051203000001 iliyo katika Benki ya Watu wa Zanzibar. Kwa hivyo, suala lile la kuwa fedha zinaliwa halina msingi, kwa sababu ilipotiwa saini mwaka 2007 Mhe. Spika, kulikuwa hakuna Mamlaka ilikuwa idara kama alivyofafanua jana Mhe. Machano Othman Said. Ilikuwa ni Idara ya Uendeshaji na Mipango ndio ambayo ilikuwa ikishughulikia. Kwa hivyo, fedha zilikuwa zikiingia katika wizara kama ni mapato ya wizara.

Mhe. Spika, ilipoanzishwa Mamlaka mwaka 2011 na hapa niliwahi kuzungumza wakati tunapitisha sheria. Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Usafiri Baharini ilikuwa mwaka 2009 lakini ile mamlaka yenyewe iliibuka mwaka 2011. Kwa hivyo, ilipokuja mamlaka ikafunguliwa *account*, na hivyo kutoka kipindi chote hicho mpaka hapo mwezi wa Mei 2013, *account* ile ilikuwa Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ndio waliokuwa wakipata fedha moja kwa moja kutoka kampuni hiyo.

Lakini ni juzi tu baada ya *ZMA* kupata baadhi ya wataalamu na kuona kwamba sasa Mamlaka inajitegemea ndipo ilipopewa *account* yake kama nilivyoitaja hapa. Kwa hivyo, kwamba pale pesa zinafanyiwa ufisadi hazina msingi kwa sababu zinapitia katika Mfuko Mkuu wa Serikali toka mwaka

2011 wala hazipitii katika wizara yetu ya Miundombinu na Mawasiliano. Sasa hiyo ilikuwa ni *transition* kabla Mamlaka haijapatikana, kwa hiyo hoja hiyo inakuwa haina msingi.

Mhe. Spika, suala la *IMO* kuingilia kati mambo ya ajira hii sio kazi yake, *IMO* ambayo ni *International Maritime Organization* kazi yake kwanza ni kusimamia usalama wa usafiri wa majini kwa ujumla wake duniani. Pili kusimamia suala la kiulinzi katika usafiri wa baharini duniani. Tatu kusimamia maji ya bahari yasichafuliwe kumwaga taka na vitu visivyoruhusiwa baharini. Nne, kusimamia shughuli za kiutawala na uendeshaji za usafirishaji wa shughuli za kisheria kwa taasisi za kusimamia masuala ya usafiri baharini.

Sasa sera za *IMO* hajihusishi na suala lolote la kibiashara na haya ni manane mimi nataka kusema kwa vitendo. Katibu Mkuu wetu na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Baharini walichukuliwa kwa udhamini wa Serikali ya Marekani kwenda kutafuta kampuni nyengine ambayo itaondokana na ile *Filtex* kwenda kubadilisha kutokana na tabia za *Filtex* walikwenda Uingereza Makao Makuu ya *IMO*, wamewaambia sisi suala hili sio letu, sisi tutakuja kuwasaidia katika ngazi hii na hii kama tulivyosoma hapa.

Kwa hivyo, sio kweli na kama Mhe. Mwakilishi ameona pahala kwa sababu yeye ni Mjumbe wa Kamati Mhe. Ismail Jussa aende akashirikiane na *ZMA* awaoneshe ili na wao wakione hicho kipengele na waweze kukishughulikia si tatizo hilo. Kusema hapa tu itakuwa haisaidii kitu, namuomba kwa sababu yeye ni Mjumbe wa Kamati aende akakutane na *ZMA* watampokea atawaelekeza, atawapa ushauri wake watamfahamu, lakini kuzungumza hapa tu jambo ambalo wao hawalielewi na katika sheria za kimataifa halimo halitokuwa na faida. Kwa sababu yeye ni mtaalamu wa Kiingereza…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri hakubakia sehemu kubwa tumsikilize kwa makini ili twende kwenye hatua nyengine iliyobaki. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nataka nimpe mambo ambayo yanashugulikiwa na hawa kwa Kiingereza, *Conventions, Protocols, amendments, resolutions, codes, circulars and reports.* Haya ndio mambo yanayoshughulikiwa na *IMO*. Kwa hivyo, Waheshimiwa napenda sana tufahamiane kwamba *ZMA* haiko nyuma kabisa katika kufuatilia haki zake za kimataifa.

Mhe. Spika, tuingie katika suala la bandari sasa hivi, Shirika la Bandari. Kwanza ushauri wa kuongeza urefu wa gati ya Mkoani na kufanyiwa

matengenezo sehemu hiyo iliyotolewa na kamati. Wizara kupitia Shirika la Bandari tayari imeshaifanyia matengenezo makubwa sehemu iliyodidimia pamoja na sehemu ya kiungo cha gati hiyo. Wizara haijapanga kuongeza urefu wa bandari hiyo kutokana na vigezo vya meli zinazotumia Bandari hiyo. Hata hivyo, wizara kupitia Shirika la Bandari lina mpango wa kununua vifaa vya kubebea mizigo kwa ajili ya bandari ya Mkoani.

Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Abdi Mossi Kombo ombi la kujenga bandari ya Mkokotoni pamoja na kufanyia matengenezo ya majengo ya ofisi. Wizara kupitia Shirika la Bandari inakusudia kujenga bandari ya Mkokotoni ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 shirika tayari limeshatayarisha michoro ya gati hiyo pamoja na makisio yake. Aidha, shirika linakusudia kufanya tathmini ya kimazingira katika eneo la gati.

Mhe. Hija Hassan Hija orodha ya makontena yaliyotoka Bandarini bila ya kulipiwa ushuru. Taasisi zinazohusika na utoaji wa mizigo katika Bandari ya Malindi ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Shirika la Bandari (*ZPC*) na Shirika la Meli. Namuomba Mhe. Mwakilishi kuniletea orodha ya makontena pamoja na risiti bandia zinazodaiwa kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa suala hilo na yeye pamoja na mimi tutashirikiana.

Mhe. Salum Abdalla Hamad na Mhe. Abdi Mossi Kombo hatua za uhuishaji wa Bandari ya Malindi ili kuendana na ushindani wa kibiashara. Mhe. Spika, ili kumudu ushindani wa kibiashara wizara yangu kupitia Shirika la Bandari limekuwa likichukua hatua za kuimarisha huduma mbali mbali kwa kuimarisha miundombinu yake ikiwemo kujenga sehemu ya kuhifadhia makontena, ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kuhudumia mizigo, jambo ambalo limesaidia sana kuimarisha huduma hiyo bandarini. Hata hivyo, serikali inakusudia kujenga bandari mpya ya Mpigaduri itakayokuwa na vigezo vya bandari vya kisasa kuweza kumudu ushindani huo kama ilivyoelezwa katika hotuba yangu ukurasa wa 20.

Mpango wa wizara katika urefushaji wa chelezo cha Shirika la Bandari kilichoko Malindi. Wizara kupitia Shirika la Bandari inakusudia kurefusha chelezo hicho ili kiweze kufikia katika kina kikubwa zaidi. Hata hivyo kutokana na majukumu yanayoikabili shirika kwa hivi sasa na kuzingatia hali ya shirika, kazi hiyo imepangwa kufanyika hapo baadae wakati hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Saleh Nassor Juma na Mhe. Salma Mohamed Ali kumruhusu ndugu Bakhressa kujenga jengo la abiria katika bandari ya Pemba. Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari haijapokea ombi kama hilo kutoka kwa muhusika. Hata hivyo, wizara inakaribisha maombi kama hayo kutoka kwa mfadhili

yeyote mwenye nia ya kujenga jengo hilo katika bandari za Pemba. Kwa hapa mimi nasimamia mwenyewe binafsi nachukua jukumu hili kuonana na mfadhili huyu ili aweze kusaidia na bandari ya Pemba katika kuona kwamba nayo inanufaika na *terminal* kama ile.

Mhe. Mgeni Hassan Juma nasaha ya kuyatunza majengo yaliyotolewa msaada na mfadhili Ndugu Said Salim Bakhressa. Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inathamini kwa kiasi kikubwa ufadhili huo na itahakikisha kwamba majengo hayo yanatunzwa ipasavyo ili yaweze kutoa huduma kwa muda mrefu kama ilivyokusudiwa.

Kuwepo na utunzaji wa *cranes* za zamani wakati shirika linanunua *cranes* mpya kila mwaka. Pamoja na kuwa Shirika la Bandari linanunua *cranes* mpya kila mwaka, *cranes* za zamani bado zipo na zinaendelea kutumika sambamba na *cranes* hizo mpya, ununuzi wa *cranes* mpya ni mpango endelevu wenye lengo la kuongeza ufanisi kulingana na ongezeko la mizigo inayowasili bandarini hivi sasa.

Mhe Farida Amour Mohammed kuongeza urefu wa bandari ya Wete. Ushauri wa Mhe. Mjumbe tumeupokea na tutauzingatia, na mimi binafsi nasema kwamba bandari ya Wete ni muhimu kwa sababu inaunganisha rahisi sana na bandari ya Tanga kwa hivyo ni suala ambalo tunalishughulikia.

Mhe. Salma Mohamed Ali kujenga paa katika njia ya kupitia abiria bandarini Mkoani kama ilivyo katika gati ya abiria bandarini Malindi. Mimi binafsi nimeshazungumza na Ndugu Hussein ambaye ni Mkurugenzi wa Ndugu Said Salim Bakhressa na hii *idea* anayo na *Inshaallah* itatekelezwa tukijaaliwa. Lakini mambo huenda kidogo kidogo madhali jana kamaliza hapo tusubirie kidogo ajichume ili na sisi tena tuendelee na mengine. Lakini kuna haja kubwa ya njia kutoka kwenye jengo la kupumzikia abiria mpaka kupanda boti kuna haja kubwa sana ya kujengwa kipaa ili wakati wa mvua ambapo Pemba kunaonesha dalili kwamba kuna mvua zaidi kuliko hata hapa Unguja katika kila mwaka. Kwa hivyo, wakati mwingi kunakuwa na mvua bandarini na abiria wanalazimika kuroa. Kwa hivyo, suala hili nalichukua na mimi vile vile binafsi kama ni Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na kuhakikisha kwamba muda si mrefu tunaona ni hali gani itakayojitokeza.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman suala la upekuzi wa abiria katika bandari ya Malindi. Ofisa wa Forodha ndiye mwenye jukumu la kupekua abiria na mizigo, polisi anaruhusiwa kupekuwa mizigo ya abiria tu, anapekuwa na shaka kwa abiria mbeba mzigo usioruhusiwa kuingizwa nchini kama silaha, dawa za kulevya na kadhalika.

Mhe. Hassan Hamad Omar kusimamishwa kazi kwa wafanyakazi 300 bandarini. Wizara haina taarifa ya kusimamishwa kazi wafanyakazi hao, hata hivyo kwa kuwa kuna taasisi nyingi zinazofanya kazi bandarini namuomba Mheshimiwa anipatie taarifa kamili ya suala hili ili niweze kufuatilia kwa karibu.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu uimarishaji wa Gati ya Mkoani. Wizara kupitia Shirika la Bandari lina mpango endelevu wa kuimarisha bandari zake zote za Unguja na Pemba kwa kuimarisha miundombinu na kuzipatia zana za kubeba mizigo. Shirika linaendelea kununua vifaa hivyo kila mwaka kulingana na hali ya fedha inavyoruhusu. Bandari ya Mkoani itapatiwa vifaa vipya katika awamu ifuatayo ambayo imepangwa kutekelezwa katika bajeti ijayo.

Mhe. Salim Shirika la Meli na Uwakala ambalo tunamalizia. Mhe. Salmin Awadh Salmin kushindwa kuwarejesha kazini wafanyakazi sita hili ameshalizunguzma Mhe. Mwanasheria Mkuu. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuajiri wafanyakazi kutoka nje je, wafanyakazi hao wana vyeti gani na kama kuna mkataba wowote wa makubaliano hayo. Wataalamu hawa walioajiriwa na shirika wanavyo vyeti ambavyo vinaruhusu kufanya kazi waliyoajiriwa, *class one engineering, certificate of competency* na zaidi ya hapo. *Photocopy* zao ninazo hapa hapa katika Baraza Mhe. Spika, kwa ushahidi kama mtu yeyote anavitaka. Wafanyakazi hawa wameruhusiwa kufanya kazi hapa nchini baada ya kupata vibali vya kazi kutoka Wizara ya Kazi na vibali vya kuishi nchini.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu mchanganuo wa mapato ya meli ya MV. Maendeleo na M.T. Ukombozi. Mapato ya M.T. Ukombozi mwaka 2012/2013 ni shilingi 1,504,287,500 na mapato ya MV. Maendeleo mwaka 2012/2013 ni shilingi 1,470,896,565. Mapato ya uwakala wa meli za kigeni mwaka 2012/2013 ni shilingi 1,658,846,006. Jumla ya mapato yote kwa mwaka 2012/2013 ni shilingi 4,645,280,072.

Mhe. Hassan Hamad Omar ulanguzi wa tiketi za Meli ya MV. Maendeleo. Tatizo la ulanguzi wa tiketi za meli ya Maendeleo limedhibitiwa baada ya meli hii kuruhusiwa kuchukua abiria 600 kutoka abiria 450. Vile vile uongozi wa shirika kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri Baharini inaendesha zoezi la kuuza tiketi kwa kutumia kitambulisho cha abiria husika kwa ajili ya kutambuliwa wakati wa safari. Mheshimiwa suala hili tunahitaji ushirikiano wa karibu sana na wananchi kwa ujumla. Kwa sababu wao ndio wanaoona na watuletee na sisi tuchukue hatua.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kabla sijatoa hoja naomba niseme moja tu. Nawaomba Wawakilishi wayapime yote yaliyotolewa kuanzia Mwanasheria Mkuu, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Naibu Waziri na haya niliyotoa mimi, wayapime kwa kina.

Kwa sababu siku moja Mhe. Spika, nilikuwa nikitafsiri mimi, mtaalamu mmoja alikuja nikawa mimi natafsiri kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili kwa wale ambao hawafahamu. Sasa kuna mzee mmoja akanyanyuka, amwambia wewe umekuja kutudanganya hapa kwa sababu tokea siku ambayo tumeanza hapa sijakuona kuandika, haa basi maneno yote hayo unayahifadhi? Unajua tena kwetu Kipemba, haya yote hayo kunayahifadhi? Yule jamaa akamwambia hivi, mimi ziko mashine zinachukua hapa, lakini mimi nakutizama wewe unayesema maneno haya umefundishwa au yako mwenyewe, kamwambia hivi hivi? Kamwambia ukisema mimi nakujua kwamba haya maneno umefundishwa au yako mwenyewe.

Kwa hivyo, nawaomba tena Waheshimiwa Wajumbe watupime sisi tuliozungumza tunafundishana au yetu wenyewe. Hivyo watu-*judge* vilivyo na watuamini, watupe *trust* tufanye kazi katika kipindi hiki kuyatatua yote ambayo au mengi katika hayo kuyaweka katika pahali pake, na tunawahakikishia kwamba kazi itafanyika nzuri, watendaji yote wameyasikia mliyozungumza, tuliyozungumza sisi wameyasikia, ahadi zetu wamezisikia. Kamati ipo tunaiomba ifanye kazi zake, kwa sababu kamati haipindwi wakati wowote kwenda kuwaona viongozi. Kamati ni kiungo kikubwa baina ya Baraza na wizara, naiomba sana kamati chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ili tuweze kufanya kazi kwa bidii.
La mwisho kabisa mtaalamu mmoja alikwenda Afrika ya Kusini kuna hoteli imeandikwa African Hotel, akataka kuingia hivi akazuiwa, basi alikaa hivi akaitizama ile hoteli akasema hivi: *"A Hotel bearing the name of my continent, hindering me because of my color, is stopping me because of my color, is denying me because of my color.* Hoteli yenye jina la kontinenti langu *African Hotel* inanizuia mimi kwa sababu ya rangi yangu; basi jamani rangi ya kitabu ndio tuzuiliwe sisi? *(Kicheko)*

Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu atusaidie naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Usemi huo nadhani ni wa Dr. Aggrey, Dr. Aggrey ndio alisema usemi huo. Haya, sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwa sababu tunajadili suala zito ambalo kutokana na uzito wake hatutawahi kulitolea maelekezo ambayo si ya kawaida, na kwa sababu masikio na macho ya Wazanzibari wote leo wanalipima Baraza hili na umakini wake katika kusimamia kivitendo au ni maneno tu. Naomba unisaidie muongozo wako kwa kunisaidia mimi na Wajumbe wa Baraza tafsiri ya kifungu hiki:

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwenye kanuni yetu hii kuna mambo mawili yameunganishwa, kuna Sheria ya Haki, Fursa za Wajumbe na vile vile kanuni zenyewe za Baraza la Wawakilishi. Anayo-*quote* yeye ni ile Sheria ya Haki, ingawaje kanuni huku juu imeandikwa moja kwa moja kama kanuni lakini mna mambo mawili katika kanuni hii. Kwa hivyo, anatupeleka kwenye ukurasa wa 25 kwenye ile sehemu ya Haki, Kinga na Fursa za Wajumbe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, kama nilivyosema kutokana na uzito wa suala hili naomba muongozo wako utusaidie tafsiri ya kifungu hiki na maelezo mafupi nitakayoyasoma ndani ya katiba pia unisaidie muongozo wako.

Kifungu cha 49 cha Kanuni; Sheria ya Haki, Kinga na Fursa za Wajumbe kinasema hivi:

> "*A member shall in addition to the duties provided under section 88 of the Constitution have the following duties and obligations:-*
>
> *49 (b) to use sitting of the House and committees to defend the rights and interest of the citizens in accordance with the provisions of the Constitution, the Constitution of United Republic of Tanzania 1977 and national ethics.*

Nataka unisaidie muongozo huu Mhe. Spika, nakuomba vile vile mzee wangu kutokana na busara zako unisaidie kulikusudiwa nini katika katiba yetu katika maelezo ya utangulizi; ambayo mara nyingi huwa yanaelezea malengo ya wenye katiba ambao ni Wazanzibari, pale iliposema kwamba,

> "Na kwa kuwa tunazingatia na kuthamini kazi nzuri ya Kimapinduzi iliyofanywa na Viongozi wa Mapinduzi, wakiongozwa na Muasisi wa Chama cha ASP na Mapinduzi ya Zanzibar 1964, Marehemu Mzee Abied Amani Karume, ambaye fikra zake zitaendelezwa na kudumishwa daima, kizazi baada ya kizazi katika kupambana na Ukoloni, Ubepari, Unyonge, Uonevu na Dharau na badala yake kudumisha Uhuru na Umoja, Haki na Usawa, Heshima na Utu".

Na kifungu cha mwisho kabla ya kumalizia pale kinasema:

> "Na kwa kuwa misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambayo serikali yake husimamiwa na Baraza la Wawakilishi, lenye Wajumbe waliochaguliwa na linalowakilisha wananchi, na pia yenye Mahkama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila ya woga wala upendeleo wowote, na hivyo kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinadumishwa na kulindwa, na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa ukamilifu".

Naomba muongozo wako Mhe. Spika, tulielekezwa nini katika kifungu kile cha sheria na vifungu hivi vilivyomo katika utangulizi wa katiba yetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla. Naomba muongozo wako Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri mmemfahamu Mhe. Ismail Jussa na muongozo anaohitaji kwa mujibu wa *preamble* ya katiba hii lakini pia fungu lile la 49 Sheria ya Kinga, Haki na Fursa za Wajumbe hasa sehemu ya (b). Ni kwamba chombo hiki majukumu yake yameelezwa ndani ya Katiba na tuikumbuke ile ibara ya 88 kuna majukumu yake, lakini ikaelezwa katika fungu hilo la 49(b) kwamba, sisi Wajumbe au Kamati au ndani ya Kamati tuna wajibu wa nyongeza mbali ya yale mambo yaliyoko kule kwenye ibara ya 88. Wajibu wa nyongeza ndio huu uliotajwa katika sheria ya haki, fursa na kinga za Wajumbe, kwamba tuna nafasi ya kutumia vikao hivi na pia ndani ya kamati katika kutetea haki za wananchi.

Nadhani kanuni hii pia ukiachia katiba kwenye ile *preamble* na sheria katika eneo lile, lakini hata kanuni pia inasema, hata Mjumbe binafsi ana haki na yeye kujitetea isipokuwa tu, kama kuna jambo anataka kulizungumza ambalo yeye ana maslahi nalo basi kwanza aseme hayo maslahi yake, lakini pia hajakatazwa. Kwa hiyo kama Mjumbe mwenyewe binafsi ana jambo fulani na ana maslahi nalo anaruhusiwa kutumia kikao hiki au mkutano kama huu, hapana shaka hata na kamati yake pia anaweza akatumia, ila kwanza aseme yale maslahi yake na namna na kwa kiasi gani alivyovutika na lile jambo.

Naelewa kwamba Mhe. Jussa kwa vile ilivyokuwa kasikiliza kwa makini sana majumuisho ya Mhe. Waziri anazungumzia pale kipengele alichokisema Mhe. Waziri kwamba hivi maelezo haya ni ya kufundishwa au vipi? Maana mnakuwa makini sana hapa, nafikiri Mhe. Jussa anatikisa kichwa kusema kwamba ndivyo haswa. Ingekuwa Wajumbe wale ambao wamemtetea mwananchi wapo Wajumbe hapa ambao wamemtetea mwananchi fulani mimi simjui, lakini nadhani ni Mhe. Hamza Hassan, Mhe. Saleh Nassor na Mheshimiwa wangu Dr. Hija Hasssan Hija. Hawa wamezungumzia kwa

maslahi ya mwananchi fulani, nadhani ndio katika mambo ambayo Mhe. Waziri inaonekana kama vile *concern* hiyo. Niliwaachia Waheshimiwa hao kwa sababu najua kwamba Sheria hii ya Kinga, Fursa na Uwezo wa Wajumbe zinawapa nafasi humu.

Kwa hivyo, wapo baadhi ya Wajumbe inawawia shida kujisema kwamba jamani mimi nina maslahi fulani. Wapo baadhi ya wananchi wanawajia Waheshimiwa Wajumbe kuwa kuna tatizo lile na lile hebu saidieni huko mbele ndio yale kwa niaba ya wananchi.

Sasa ingekuwa lile jambo si haki anayeongoza kikao angepaswa kuzuia, lakini tumeachia kwa sababu taratibu zote kwenye sehemu ya katiba hii lakini kwenye kanuni yenyewe na pia katika hiyo Sheria ya Haki, Kinga na Fursa ya Wajumbe inaruhusu. Ndio maana tukawa tumejaribu kuachia, ili ujumbe huo kutoka kwa wananchi ufike na Waziri anayehusika au Serikali iweze kutoa majibu.

Kwa hivyo, nadhani sasa isiwe shida ni katika kujaribu kuona ame- *observe* hiyo kwamba kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wameombwa na wananchi fulani asaidie katika tatizo lake na Mhe. Waziri ameonekana kwamba ame- *observe* kuwa hili labda ni maneno ambayo ameambiwa mtu si sawa hata kama kuna mtu ameambiwa amewaomba kati yenu Waheshimiwa Wajumbe. Hicho kitu kinakubalika kwa mujibu wa Katiba hii kwenye sehemu yake, lakini pia kwenye Sheria, ya Kinga, Haki na Fursa za Wajumbe.

Nadhani lisitupe shida mimi nilikuwa nasikia hayo kwa makini sana na nimeacha sikuingilia kati kwa sababu ya kujua tararatibu hizi zinaruhusu. Kwa hiyo, Mhe. Ismail Jussa nikuombe na wewe sasa uyapokee hayo majibu pale penye utelezi kidogo ndio ulimi huu ulivyo. Isituletee tabu na tuendelee na hatua zilizobaki, lakini isitupe tabu kwamba labda kuna watu *of course* nafasi ikitumika vibaya itabidi tueleze, tuelekezwe.

Lakini kama nafasi imetumika kwa mujibu wa taratibu ndio maana tukaachia kwamba ili tuone kila raia wa nchi hii, kila mwananchi anapata haki kupitia chombo hichi na kupitia kwenu na Serikali itimize wajibu wake pale ambapo jambo hilo limefuata taratibu zinazohusika.

Kuhusiana na ajenda hii Mhe. Waziri ameeleza kama imeridhisha au laa ni suala ambalo Waheshimiwa Wajumbe mtaliangalia, lakini ameeleza mambo fulani fulani kutokana na zile hoja alizozitoa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hija Hassan Hija , Mhe. Asaa Othman Hamad kwa ajili ya kumtetea mwananchi fulani.

Kwa hiyo, kama hivyo ndivyo nakumbuka nimemsikia sana Mhe. Waziri kwamba suala la meli ambayo usajili wake kidogo umekawia tatizo ni kuhusu kuchukua abiria, lakini kwa mizigo wakati wowote ndio nilivyosikia. Sasa liangaliwe hilo je, meli hiyo imefikia kile kiwango cha kuchukua abiria, ni kweli matatizo yametokea hapa mifano miwili mikubwa sana katika nchi hii na mingine mingi.

Kwa hiyo, kufuata taratibu nayo kuna umuhimu wake. Nafikiri baada ya maelezo hayo itoshe kwamba sheria inaruhusu na ndio maana Kiti kikawa kimeruhusu maelezo yale ya Waheshimiwa yaweze kutolewa kwa ajili ya kuona haki ya mwananchi huyo iko kwa kiasi gani.

Sasa hatimae tutafikia pahala tuone kwamba je, jambo hili likawa moja kwa moja au wahusika wafuatilie zaidi katika kuona uhalisia wa jambo hili tumelimaliza kwa kiasi gani.

Nafikiri mimejaribu kueleza vya kutosha. Na baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2013/2014 wanyanyue mikono, wasiokubali, waliokubali wameshinda.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naona mlipoona Mwenyekiti anakawia kuja mkasema huyu kakimbia nini. Hapana nilikuwa naweka suti vizuri ili tuendelee na mambo haya kwa umakini sana.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tunaingia katika hatua muhimu sana nilikuwa naomba unisaidie kuhusu utaratibu tu; kwamba kwa kawaida tunapoingia katika sehemu ya mapato huwa unatuhoji yale maeneo ambayo mapato yapo, lakini huwa zinakuwepo idara au mamlaka ambazo huwa kuna ziro kwa mwaka ule, lakini pengine Wajumbe wa Baraza la

Wawakilishi katika michango yao walichangia na kuonesha maeneo ya mapato ambayo yalipaswa yawepo. Sasa nilikuwa nataka muongozo wako, na ili nifahamike vizuri kwa eneo hili kwa mfano maeneo mengi ambayo tumeyachangia yaingie Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo ina ziro.

Naona nitake muongozo wako au utaratibu wako kabla hatujaingia, kwamba je, mafungu yale yanayohusu mapato si katika mambo ya matumizi tutakuwa na haki ya kuyahoji wakati katika fungu lile tutakuwa tunapita tu kwa sababu pana ziro, wakati ukiyapeleka katika mafungu mengine ya mapato yatakuwa hayahusiki na maeneo yale. Nilikuwa naomba utaratibu na muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nikuombe radhi labda sikufahamu unakusudia nini.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, labda nikizungumza mifano utanielewa zaidi. Nilisema katika utaratibu wetu wa kawaida ni kwamba zile idara au mamlaka ambazo zinasimamia eneo fulani. Ikiwa kwa mwaka unaohusika hazikupangiwa mapato huwa panakuwa na ziro na kwa mfano hapa Idara ya Mipango Sera na Utafiti hatujafika, lakini nataka nipate maelezo kabisa ili ukianza kutuhoji nisiingilie kikao chako Mhe. Mwenyekiti.

Sasa kama kuna maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe walipokuwa wakichangia waliyagusa yanayohusu mapato na pahala pale pa kuhojiwa ni hapa, lakini kuna ziro utatupitisha pale Mhe. Mwenyekiti, na nikihoji katika Ofisi Kuu Pemba au katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara itakuwa si sehemu yake.

Ndio nataka muongozo wako kwamba je, na kama hairuhusu ilikuwa naomba tuwe na utaratibu maalumu kwa fungu hili kwa sababu tumehoji mambo mengi hapa yanayohusu mapato na katika masuala ya utafiti tulipitie ili tujiridhishe kwamba tumeridhika na majibu ya Mhe. Waziri, na ikiwa tumeridhika basi tutoke hapa na maamuzi ya pamoja. Nilikuwa nataka muongozo wako Mhe. Mwenyekiti, nadhani umenielewa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Acha nitizame kama nimefahamu sawa sawa. Unazungumzia kwamba kuna baadhi ya idara humu kwenye sehemu ya mapato imewekwa ziro, lakini katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe inaonekana pengine kweli sehemu kuna mapato fulani sijui kama ni sawa.

Sasa tunachunguza vipi kama tunaweza Wajumbe wakapata nafasi ya kuhoji hilo au vipi? Sijui labda kwenye suala hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hilo ni moja. Lakini kama tunapata haki tunahoji vipi kwa sababu pale kawaida huwa hatusomewi kama pana ziro idara ile. Kwa mfano kwa hapa tukitoka Ofisi Kuu Pemba tutakwenda moja kwa moja kwenye Idara ya Ujenzi na Utunzanji barabara ndio maana nikataka kujua yale mambo ambayo tumeyauliza au tumeyahoji. Kwa sababu tunaweza kusema tunakuja kuyauliza kwenye Idara ya Mipango kwenye matumizi.

Lakini kwanza tumekusanya mapato lakini zaidi kuna maeneo mengi ambayo kila mtu anataka kuyauliza kule. Kwa hivyo, nilikuwa nataka muongozo wako kwamba tufanye nini, na mimi ningeshauri kwamba inawezekana kwa uzito wa hoja ambazo zitatolewa kama tulivyokuwa tumefanya maamuzi mengi Mhe. Mwenyekiti ambayo mengine si kawaida.

Lakini tumefanya kutokana na kujali maslahi ya watu basi yale maeneo yanayohusu mapato ambayo tuliyaibua hapa basi tupate nafasi ya kuyazungumza katika Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri kwamba kuna jambo la aina hiyo pahala sahihi pa kuweza kuhoji ni chini ya ile Idara ya Mipango zamani ilikuwa inaitwa Mipango na Uendeshaji. Sasa nafikiri ndio Mipango na Sera, hebu nisaidie.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Ismail Jussa anachosema kama kuna Mjumbe amehoji kuhusu masuala yanayohusina na mapato kwenye Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Lakini kwenye kitabu kikubwa kuna ziro ziro katika eneo la mapato. Je, wanaweza wakaruhusiwa.

Utaratibu uliopo kwamba haya yanaitwa ni Mapato ya Mawizara yanasimamiwa chini ya fungu la Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambapo yuko Katibu Mkuu. Masuala ya Mapato kwa maana ya fedha za miradi yaani zile fedha za miradi zinasimamia chini ya fungu la Mipango Sera na Utafiti. Makusanyo ya Wizara yanayotoka katika Idara tofauti za wizara ukiacha taasisi zinazojitegemea na Mashirika yanasimamiwa chini ya kifungu cha Uendeshaji na Utumishi.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa maana hiyo, kama kuna hoja zinazohusu hivyo ni chini ya Uendeshaji na Utumishi. Sasa kama kuna jambo linalohusu sehemu fulani ambayo Mjumbe aliulizia kuhusu masuala ya mapato na imeoneshwa ziro ziro. Mimi nadhani tumpe fursa ya kuweza kuhoji. Muongozo zaidi Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi suala langu halitofautiani sana na Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Haji Omar Kheri kajibu vizuri kwamba mapato ya wizara ndio yanashughulikia na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Lakini tatizo lililokuwepo kwamba kuna mashirika au kuna hizi mamlaka ambazo huku katika mafungu moja moja hazina mafungu yake. Lakini vile vile kama tuking'ang'ania kwenye fungu la Mipango, Sera na Utafiti kuna maelekezo na maelezo mengi ambayo hayakupatiwa ufafanuzi ambayo ni nje ya haya mapato.

Sasa kwa bahati mbaya na hili nafikiri Wajumbe wengi tunakuwa tunalizungumza sana nafikiri katika kurekebisha kanuni tuje tuangalie utaratibu. Mashirika haya hatuna sehemu ya kuyabana, hasa katika masuala ya mapato yanapovuja. Yaani kifungu cha Mipango Sera mambo yote ya wizara, na lakini ndio maana kwa kuwa haya mashirika hayana mamlaka hazina mafungu yake na ndio maana kunakuwa na kiburi aah hebu tuachie sisi tunajitegemea, tuna maamuzi yetu, wana mamlaka kamili.

Kwa kuwa wana mamlaka kamili huku hatuna mwahala mwa kuwahoji. Sasa hapa mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti lazima utusaidie, aidha maana yake ukitaka kuhoji masuala ya mapato kuna *ZMA*, kuna masuala ya Mamlaka ya Anga, kuna suala ya Idara ya Utunzaji na Barabara na maeneo mengine.
Lakini kuna mambo ya utekelezaji wa kawaida wa zile shughuli za mamlaka au mashirika yenyewe hatuna sehemu ya kuja kuzuia fungu. Ambapo maelezo ya Waheshimiwa Mawaziri hayakutosheleza kwa yale maeneo, au kuna maeneo mengine hayakujibiwa kabisa.

Sasa hapa mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, tutumie busara sote, mimi nashukuru sasa hivi kwamba Serikali yetu na sisi tunakwenda vizuri hasa katika mambo ambayo kanuni ziko *silence* katika kutumia busara.

Mhe. Mwenyekiti, tunapohoji haya mapato tunaisaidia Serikali ili wale waliokabidhiwa mamlaka au mashirika wajue kwamba zile fedha si zao ni fedha za wananchi. Pamoja na kwamba hatuziidhinishi katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tusaidiane. Aidha wewe au Mwanasheria Mkuu, Mawaziri wengine tusaidiane katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mamlaka zinazojitegemea zinaielewa sana, *concern* yake, anachotaka tutumie busara. Lakini kuna busara na taratibu ambazo

tumejiwekea kwa mujibu wa kanuni, kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu Katiba.

Sasa mamlaka zinazojitegemea fungu la kubana, kuhoji ni Uendeshaji na Utumishi ambapo yupo waziri ambaye ana mamlaka ya kule kwenye mamlaka zinazojitegemea, kwa sababu maamuzi ya mamlaka zinazojitegemea yanakwenda kwa Waziri. Kwa hiyo, fungu ni hili sasa jinsi ya kujipanga tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba pengine inawezekana hoja hiyo hiyo moja imezungumzwa na watu watatu.

Kwa hivyo, mimi nadhani sisemi kwamba napanga utaratibu wa kuhoji vifungu, lakini namna ya kujipanga tu kwamba hoja ya mamlaka kama inahusu mamlaka inaweza ikahojiwa kwenye Mipango na Uendeshaji, ndilo fungu ambalo linastahiki kuhoji taasisi ambazo hazina mafungu humu kibajeti, huo ndio utaratibu Mhe. Mwenyekiti. Sasa busara itategemea busara yako Mhe. Mwenyekiti, lakini wa kupitisha bajeti hivyo ndivyo ulivyo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu una nyongeza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru. Lakini alichotaka Mhe. Hamza Hassan Juma ni busara. Sasa mimi nina busara si kanuni. Lakini mimi nadhani cha msingi ninachoogopea katika suala la kanuni ni kuweka jambo leo, na tukasema kwamba huko hatutapata nafasi mambo ni mengi halizuii na Wizara ya Afya kukawa na mambo mengi, Wizara ya Kilimo kukawa na mambo mengi. Sasa ule utaratibu uliowekwa wa kupitisha bajeti ni kuutolea maamuzi na kwa mujibu wa kanuni ya 158 muongozo ambao utatolewa kwa jambo ambalo halipo muongozo wake, ukilitolea muongozo maana yake linaingia katika kanuni.

Sasa mimi cha msingi ninachosema Mhe. Mwenyekiti, hili ni Baraza lina mamlaka ya kupitisha bajeti. Lakini bado ni Baraza la Shura la kushauriana na kuelekezana, la kuambiana si kama mahakamani kwamba lazima ipitishwe hukumu. Lakini pahala pakubwa na madhumuni yake makubwa ni kuelekezana.

Sasa mimi nadhani kanuni zetu zinaweka huo utaratibu kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mimi nadhani tujipange tuone namna gani ya kuzieleza hizi hoja kwa ujumla wake. Lakini mwisho wa siku mimi nadhani madhumuni makubwa ni kuelekeza ili yaende yakatekelezwe na mwisho Serikali iweze kufanya kazi.

Sidhani kama ni kwa ajili ya kutolewa hukumu na sidhani kama hilo ndilo analolitafuta Mhe. Hamza Hassan Juma. Anatafuta ni kwamba tuweze kufanya kazi vizuri na Serikali isikie kilio kilichopo na kiweze kutekeleza kwa mujibu wa Baraza hili linavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri uzoefu wa huko nyuma, unajua mabadiliko haya ya uundaji wa idara yanatafautiana. Lakini uzoefu wa huko nyuma jambo lolote ambalo la shirika au mamlaka ambalo halina kasma zake humu ilikuwa tunakwenda kwenye Idara ya Mipango na Uendeshaji ambayo kwa sasa ndio hiyo masuala ya Uendeshaji na Utumishi.

Kwa hivyo, hiyo iko kotekote; kwa upande wa mapato lakini hata kwenye maamuzi. Kama kuna sehemu ambayo humu mmeonesha ziro ziro na basi Mjumbe alikuwa amechangia, na kwa hiyo ana hoja juu ya jambo hilo. Basi tuitumie hiyo hiyo sehemu ya Uendeshaji na Utumishi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, mimi nilikuwa nahitaji muongozo wako. Kwa mujibu wa kanuni ya 98 kanuni ndogo ya 6 naomba nieleze kwamba, hoja ya kupunguza fungu lolote katika Makadirio ya Matumizi ya mwaka itatolewa wakati kifungu hicho kinachohusika cha fungu hilo kitakapokuwa kinajadiliwa na Kamati kwa namna ifuatavyo:

Zimetajwa hapa hizi namna zenyewe lakini kifungu cha 98(c) na (d) kinasema kwamba Mjumbe anayetaka kutoa hoja ya kupunguza fungu lolote ataeleza nia yake hiyo wakati anachangia makadirio ya wizara inayohusika na matumizi hayo.

Lakini (b) Mjumbe ataeleza kwa ufafanuzi na kwa ushahidi kama upo sababu yake ya kutoa hoja hiyo.

Na (e) ikiwa Mjumbe baada ya kueleza nia yake na sababu zake atakapotoa hoja hiyo na maelezo.

Sababu ya kutaka muongozo wako Mhe. Mwenyekiti, tuna mashirika ambayo mengi na Waheshimiwa Wajumbe wametumia kifungu hiki cha 98 kueleza *concern* yao na kutoa fungu. Na kwa mujibu wa kanuni ya 63 inazungumzia juu ya hoja tatu ambazo ni peke yake zinatolewa.

Sasa nilikuwa nataka muongozo juu ya kifungu hiki na juu ya Wajumbe ambao wametumia kifungu cha 98 kuliambia Baraza lako juu ya kutaka kuondosha fungu ikiwa hawatoridhika na majibu yaliyotolewa na Mhe. Waziri. Na kwa sababu hiki kifungu ni kimoja cha Idara ya Sera na Wajumbe

walioeleza ilikuwa nia yao kupitia kifungu hiki inaweza kuwa ni wengi. Sasa nilikuwa nataka muongozo wako juu ya eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti: Nakumbuka utaratibu wa Bunge maana sisi tuko tofauti. Sasa kama kuna *best practice* iliyotumika pahala fulani. Wakati mwengine inabidi tufuate hii ile aliyozungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu jambo ambalo halikuekewa kanuni, mta- *input under 158* na hii itakuwa ni sehemu ya kanuni, lakini kwa hilo jambo ambalo kanuni ipo labda hapo sasa tuseme utaratibu wa kutenga kanuni kando.

Kwa sababu ndio unaoruhusiwa, na kanuni vile vile kwamba kwa dharura fulani kanuni tuitenge kando ili kuweza kuruhusu dharura ile itumie, lakini kwa yale yalioko kwenye kanuni unafuata kanuni kama kuna dharura inaitenga kando ili kuruhusu. Haliko ndani ya kanuni muongozo *under* 158 ambayo hiyo ndio inayoongoza kitabu. Sasa , *concern* yako Mhe. Salmin Awadh unazungumzia je, kama kuna Waheshimiwa wengi wana hoja juu ya eneo hilo la Uendeshaji kwa sababu ya kutaka kupunguza fungu *of course* hilo ni suala la matumizi tunafanyaje wakati kuna Wajumbe zaidi ya watatu ndio anachozungumza hicho.

Kama zile hoja ni kubwa za msingi sasa labda utaratibu wa kutenga kanuni ndio itumike ili kuruhusu hoja nyingi zaidi nadhani tumeelewana. Basi tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hatujajua tuendelee vipi tunatenga kanuni kando?

Mhe. Mwenyekiti: Hatujafika kwenye dharura hiyo, itakapotokea dharura kuna hoja nyingi zinazohusiana na eneo fulani ambazo zile ruhusa inayokubalika imekwisha ni kuzingatia uzito wa yale mambo. Lakini nafikiri tunaweza tukaweka kanuni kando, tunaweza tukaweka, tunaweza tusiweke.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tukubaliane na rai hiyo kwamba kwa *nature* na mjadala huu tutalazimika baadae tuifikie hatua hii, na kwa kuwa wenye mamlaka ya kuweka kanuni kando ni Baraza sio Kamati, kwa hiyo mimi nadhani tu kwenye kiti kwanza. Kwa sababu kwamba tukikubaliana kwamba tufike hatua hiyo nadhani Mhe. Mwenyekiti, urudi kwenye Baraza lako ili uwe Spika, ili tutenge kanuni kando na baadae tuendelee. (*Makofi*).

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kilichotolewa hapa ni uwezekano wa uwezekano wa dharura, lakini hatujakuwa na dharura. Mimi ninachosema kama vile nilivyosema mwanzo Mhe. Mwenyekiti, kwamba

tunachofanya maamuzi yoyote tunayoyafanya hapa tunaweka kumbukumbu. Hii ya kwamba kuna hoja nyingi naamini inaweza ikatokea kwa wizara hata zote vile vile.

Sasa lazima tupime umuhimu wa hiyo dharura yenyewe tukirudi katika msingi wa kwamba chombo hiki madhumuni yetu ya msingi ni kushauriana Wajumbe wameeleza, Waziri kayasikia ndio msingi wake. Yale ya lazima ambayo kusema kweli kuna kosa kuna kamati na mafungu haya kabla ya kuja hapa yanapita kwenye Kamati. Hayakuonekana kwenye kamati Wajumbe wameyaona sasa hizi kanuni zilipotungwa zilikuwa na msingi wake, wenzetu wana kanuni ambazo ni ngumu zaidi hata kuliko sisi. Sisi tuko huru kabisa mtu anainuka akasema, akanyanyuka anakaa. Wenzetu hakuna utaratibu huo, na wao ni mabunge ambao wanapitisha kama hivi.

Sasa mimi nasema ni suala la kupima kwamba tunataka kuweka kumbukumbu kwa kitu ambacho utaratibu wetu wa bajeti unaanza mbali, haukuanza kwenye Kamati ya matumizi umeanza kwenye mafungu umekuja Baraza zima umekuja Kamati ya matumizi kumalizia. Hapa ni pahala pa kushauriana si mahakamani kutoa hukumu.

Mhe. Mwenyekiti: Nimeeleza kwamba pale itakapotokea haja si kwamba tuanze sasa moja kwa moja pale. Pale itakapotokea haja kwamba kuna hoja nyingi za aina hiyo na tukaona kwamba hoja zile za msingi sana basi tunaweza tukarudi, na tuelewe tu kwamba suala la kutenga kando kanuni ni suala la muda, ni kwa sababu ya dharura ile iliyopo sio kwamba inakwenda moja kwa moja ile tena ni suala la muda kwa dharura iliyopo, mkishamaliza mmekwisha. Haya tuendelee.

FUNGU 26 - WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	50,200,000
Kifungu 0701	Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara	10,000,000
Kifungu 0801	Idara ya Usafiri na Leseni	346,000,000
Jumla ya Fungu		**406,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU - WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya nilipokuwa nikichangia sikupata fursa kutoka kwako kwa mdomo nilichangia kwa maandishi, na bahati mbaya sijui Waziri karatasi niliyompelekea hakuipata au hakuiona, hakunijibu hata hoja moja. Kwa masikitiko makubwa sana, nipo hapa kwa niaba ya wananchi, suala hili viongozi wa Pemba wamekuwa wanapata tabu wakiwa Wawakilishi na Wabunge katika uwanja wa ndege, pamoja na uheshimiwa mimi sijapata kuona utaratibu wowote duniani, hata hapo Dar es Salama ukaonesha kitambulisho ukaambiwa usipite uwanja wa ndege.

Suala hili nilikuwa nalipigia kelele katika Baraza hili, hata katika kipindi cha maswali na majibu, hapo Dar es Salaam mimi nimeshawahi kupita sio mara mbili wala tatu nimeonesha kitambulisho nikapita na gari. Viongozi wetu, waheshimiwa wetu wamekuwa wakipata tabu sijui nidhamu hii iko wapi, kulipishwa shilingi 500, Wabunge wamekuwa wakipiga kelele sana wa kisiwa cha Pemba pamoja na Wawakilishi, na ukionesha kitambulisho mlangoni huruhusiwi kupita

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, samahani sijakufahamu hoja yako ni nini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba, nahoji kuhusu uwanja wa ndege Pemba. Viongozi wetu wakiwemo Wabunge na Wawakilishi wamekuwa wakipata tabu sana kupita pale, ikiwa magari ya SMZ yanapita ikiwa Mbunge, viongozi wa nchi au Mwakilishi wa nchi hii haruhusiwi kupita mpaka alipe shilingi 500, utaratibu huu sijapata kuuona.

Isitoshe Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo uwanja wa ndege ukionesha kitambulisho ukitaka kuingia ndani huruhusiwi. Sijui hoja yangu umeshaifahamu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ulichangiaje, katika maandishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nilichangia kwa maandishi kuwa nitahitaji maelezo viongozi wetu hasa Pemba Wabunge na Wawakilishi wamekuwa wakipata tabu kupita katika mlango ule, pamoja na uheshimiwa wao wakionesha kitambulisho pale hawaruhusiwi kupita mpaka walipe shilingi 500, wakati gari za serikali zinapita na kwa mujibu wa katiba hii hapa Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ubaguzi wowote kulindwa au kupata haki sawa mbele ya sheria.

Mhe. Mwenyekiti: Mlango upi unaokusudia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Chake Chake Uwanja wa ndege Pemba. Mbunge au Mwakilishi akipita pale anapata usumbufu. Ni lazima alipe shilingi 500, na isitoshe hata ukionesha kitambulisho kama Mheshimiwa sasa uheshimiwa unakuwa na thamani gani, mafunzo hayo tunayapata wapi, hakuna duniani. Hapo Dar es Salaam haijafika hatua hiyo kwa ndugu zetu wa Tanganyika, kwa hivyo nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Maelezo Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Mwakilishi, nilimuomba radhi kwamba jina lake sikulitaja na bila shaka nililijibu kwa ukamilifu, kwamba malalamiko haya ya viwanja vya ndege kuhusu malipo tofauti, mimi binafsi nitayachukua serikalini tukae pamoja tuangalie ni lipi lililokuwa lina kasoro na lipi lililokuwa linaeleweka. Kwa hivyo, pamoja na hayo anayoyasema ndio hayo, kwa sababu sasa hivi hapo ada ya kiingilio ni gari yoyote ya *private* inayoingia isipokuwa gari za serikali.

Kwa hivyo, tutakwenda kuangalia, kwa sababu sheria au kanuni na taratibu hizi zinazowekwa na mamlaka au mashirika ni mambo ambayo yamo ndani ya uwezo wao wa kuamua, yanapofika huku juu tukaona kwamba ni kero au nini yanarekebishika. Kwa hivyo namuhakikishia Mhe. Mjumbe tutakwenda kufanya upelelezi zaidi ili kuona ni kitu gani kifanyike ili hali iweze kuwa nzuri. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Anachosema Mhe. Waziri ni kwamba maelezo ya malalamiko hayo anayapokea kuyafanyia kazi. Nadhani kwa kifupi ni hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amekuwa hodari katika Baraza hili na ikiwepo *hansard* naweza kumuonesha. Nilimuliza swali hapa, akasema pindipo ukiwa na kitambulisho uwanja wa ndege wa Zanzibar kama ni Mheshimiwa utaruhusiwa kupita, hayo maneno kajibu yeye Waziri na hii sio mara ya kwanza, ni mara ya pili au ya tatu anatoa kauli hizo na *hansard* zipo, lakini utekelezaji wake Mhe. Waziri anakuwa haufuatilii. Mdomoni ni rahisi kusema lakini vitendo havipo.

Mhe. Mwenyekiti: Unataka aeleze zaidi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Aah! mimi Mhe. Mwenyekiti, mazungumzo yetu mimi na Mhe. Jaku ya nje basi asiyaingize

katika kazi. Anaweza akaniuliza swali nikamjibu, lakini sijajibu kwenye Baraza kinyume na kile kinachotokea, hilo nahakikisha hasa.

Kwa sababu mimi ninapoulizwa swali katika Baraza najibu kwa mujibu wa ninavyoona ni sawa na kama silijui basi nitajibu kwamba silijui na nitalifanyia kazi, kama nilivyosema sasa hivi. Haya malipo ni utaratibu waliojiwekea wenyewe Mamlaka kutokana na sheria tulizowatungia sisi wenyewe kwamba sasa ni Mamlaka kwamba wana uwezo. Sasa kama kuna kitu chenye kero na kinafika serikalini, ni juu yetu sasa kukichukua na wao kutuamini kwamba tutakwenda kukifanyia kazi. Lakini sijajibu kwamba ukenda na kitambulisho, kwa sababu mimi sio wao.

Mimi mwenyewe hivi sasa ninapopita na kigari changu kidogo, nikitoka nyumbani nachukua shilingi 500 sitaki kero na mtu, nachukua shilingi 500 nikifika pale nampa napita nakwenda zangu na ushahidi upo pale uwanja wa ndege, kwamba nikipita na gari yangu ya *private* nalipa. Kwa hivyo, nasema kama hizi ni kero basi tatakwenda kuzifanyia kazi, lakini sio madhumuni yetu sisi kwamba labda kuweka shinikizo au kuweka usumbufu kwa watu wengine, ile ni Mamlaka. Tulipopitisha sheria ya mamlaka kuna mambo yake na hapa ndio tujue ile mipaka yake, kwa sababu idara inapofanya kazi na mamlaka inapofanya kazi ni vitu viwili tofauti.

Sasa madhali mamlaka kuna mambo ambayo yameonekana kuwa ni kero, basi sisi tutayaorodhesha tuyachukue tukakae tujadiliane, ambayo ni sahihi tutawaambia haya endeleeni nayo, ambayo sio sahihi tutawaambia haya musiendelee nayo. Hilo ndio kusudio letu.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri amejaribu kujieleza Mhe. Waziri, suala hili ni la Mamlaka sio la Waziri moja kwa moja, kwa hivyo lile ambalo anaambiwa hapa sasa yeye ni wajibu wake kulipeleka kwenye Mamlaka likafanyiwe kazi kwa pamoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kidogo tu anieleze anayetakiwa kulipa pale ni gari au yule kiongozi. Linalolipishwa pale ni gari au yule mtu.

Mhe. Mwenyekiti: Haya tupate maelezo zaidi, anauliza anayetakiwa kulipa ni gari au yule kiongozi aliomo kwenye gari.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyojua na kwa mujibu wa nilivyopita mimi mwenyewe, basi inaelekea ni gari ndio linalolipiwa. Sasa kama sio sahihi ndio tukasema tutakaa kitako, kwa sababu mimi mwenyewe binafsi nasema nikipita na gari ya WMM

siulizwi, lakini nikipita na ile gari ndogo basi mimi mwenyewe natoa shilingi 500 wala hawaniambii nenda wewe Mheshimiwa hapana, na mimi nawatembelea asubuhi na jioni pale ni waziri wa wizara ile. Kwa hivyo, inayolipiwa ni gari inayopita ni *private* au ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Ni gari. Nafikiri hata uwanja wa ndege Dar es Salaam iko hivyo. Mimi nikipita na SMZ sijazuiwa hata siku moja, ukipita na gari nyengine wanakutoza. Nadhani tuendelee, Mhe. Jaku Hashim una nini tena?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuna tofauti ya mtu na gari. Sasa kiongozi huwa anapita bure pale aeleze pale, gari sawa lakini mtu uwanja wa ndege na sisi tumeshapita Mhe. Mwenyekiti, gari ndio haipitishwi, lakini kama kiongozi unaruhusiwa tu kupita, karibu tu hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani mawazo ya Mhe. Ismail Jussa.

Mhe. Mwenyekiti: Ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ndio ule utelezi wa ulimi. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Naomba radhi.

Mhe. Mwenyekiti: Ameomba radhi mwenyewe na mimi pia namuombea radhi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Naomba radhi kwa hilo. Kitumbatu ningesema ndo vewa kwa vewa. Lakini naomba radhi kwa ulimi kuteleza.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema mawazo ya Mhe. Jaku Hashim Waziri ameipokea na akasema kwamba hili ni jambo ambalo linasimamiwa na Mamlaka kisheria. Sasa serikali inalichukua ili kwenda kuyatizama na kuona hayo yanayofanyika yaendelee au kuna marekebisho kidogo, ndicho alichosema.

Hoja ya Mhe. Jaku Hashim anasema je, kinacholipishwa ni mtu au gari. Serikali bado tunasema ni gari, gari ya SMZ au gari ya serikali ndiyo inayosamehewa, mtu hasamehewi na kwa sababu hiyo hiyo hata Waziri anapotumia VIP na Mwakilishi analipa 20,000 ndani, licha ile shilingi 500 ya gari. Kwa hivyo, hapa haizungumzwi mtu inazungumzwa gari.

Mimi juzi nilisafiri kwenda Dar es Salaam nilikwenda na gari ya SMZ sikulipa, lakini nilipofika ndani nikatoa shilingi 20,000 kwa ajili ya Uwanja. Kwa maana hiyo mtu analipa na gari *private* zinalipa. Lakini waziri ambaye ni waziri wa serikali hii analipa. Kwa hivyo, kimsingi tunachozungumzia hapa ni gari za *private* zote zinalipa, hata huko Dar es Salaam huwezi kuingia kama hujalipa. Hata ukiwa Waziri kama umekwenda na gari ya *private* utalipa na hapa vile vile. Wakati wa kurudi nilikuja kupokelewa na gari yangu *private* nikalipa. Kwa hivyo, mimi nadhani tukubaliane tu kwamba kama tunataka sasa, tunapopanda Waheshimiwa Wawakilishi tupate *exemption.* Hilo sasa ndio Waziri alilosema kwamba serikali inalichukua iende ikakae na Mamlaka ili tuone tunaweza tukafanya nini.

Lakini wakati huo huo hatuwezi kuamua kwamba gari ya *private* hata akienda nayo mwanangu asilipe, kama itakuwa ni suala hilo. Kwa hivyo, mimi nadhani kwamba tukubaliane kwamba gari za binafsi zinalipa, lakini serikali inalichukua kwenda kulifanyia kazi, kama Mhe. Waziri alivyojieleza, amejieleza vizuri sana, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani tukubaliane Waziri alichukuwe akalifanyie kazi. Tukitaka Waziri ajibu hapa ndio ile kuingilia mamlaka iliyowekwa kisheria, ambalo sio jambo zuri sana. Kwa sababu hatimaye mamlaka zile zinazohusika zitakuwa hazifanyi kazi kwa mujibu wa sheria. Haya, tunaendelea basi.

Kifungu 0301

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia nilizungumzia suala la kiwanja cha ndege Pemba. Mhe. Waziri alinijibu, lakini sikuridhika na majibu ambayo amenijibu Mhe. Waziri. Kwa sababu ni yeye mwenyewe aliulizwa swali la nyongeza humu, kwanza ni suala la taa. Tulimuuliza swali la nyongeza humu kipindi kilichopita, akasema kwamba kabla ya kufika bajeti, tumezungumza na watu na tumekubaliana kwamba watatutilia taa, hilo moja.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, limezungumzwa na sasa hivi ni miaka 49. Kwa nini uwanja wa Pemba uko hali ile, leo tunakuja kuambiwa kwamba kipindi hiki ndio utatizamwa *why*? Nipewe jawabu ambalo litaniridhisha, si hivyo nachukua pesa hapa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana tena na hali aliyonayo ya kutoridhika Mhe. Asha Bakari Makame, kama ambavyo nilivyokuwa nayo mimi. Hivyo hivyo, alivyokuwa haridhiki yeye kuwa kiwanja kiko vile, basi na mimi nina hisia hizo hizo na

ndio maana nikasema kwamba ndani ya mwezi wa Machi, 2013 nilihakikisha na Mhe. Omar Yussuf Mzee kama ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni shahidi, tulikaa vikao vitatu, nikawaambia tuhakikishe *tender* ya taa za uwanja wa ndege tunaianzisha na ikaanzishwa kweli, na *document* zipo za kwamba ile *tender* ilianzishwa, kwa mujibu wa taratibu za manunuzi yaani *Procurement Act* ya Zanzibar ni lazima wapatikane wazabuni wasiopungua watatu, kwa bahati mbaya ilitokezea wakapatikana wazabuni wawili. Tukawa tunashauriana, tukasema kwamba katika hali kama hii, kwa sababu kuna shutuma nyingi hapo uwanjani, basi inaweza ikawa tena ni shutuma nyengine, tuiwachie madhali hawakutimia watatu.

Lakini hivi sasa namuhakikishia Mhe. Asha Bakari kwamba itaanzishwa tena utaratibu wa *tender* mpya. Kwa bahati nzuri ni kwamba pesa zote zitaombewa katika bajeti hii, shilingi bilioni 1.7 zimeshawekwa kwa ajili ya kutia taa uwanja wa ndege katika bajeti hii tuliyonayo. Hilo namuhakikishia. Mimi naitaka kuliko unavyoitaka wewe, maana naishi kule kule na wagonjwa wetu tunawapeleka kiwanjani hawapati ndege, angalau wewe una nyumba yako hapo Mpendae, mimi naishi kule kule, naitaka kweli kweli hiyo taa Pemba. Namuona Mhe. Omar Yussuf Mzee anataka kuongezea kitu labda.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa dada yangu hapa Bi Asha Bakari aliuliza maswali mawili ya msingi kuhusiana na Uwanja wa ndege wa Pemba.
Moja ni suala la taa, ambalo Mhe. Waziri amelijibu na hatua tuliyofikia na *Inshaallah* tutalifanikisha tu hili suala la taa. Kama tungekuwa tumewapata *bidder* watatu au zaidi kwa mujibu wa sheria yetu ya *procurement*, nadhani sasa hivi ingekuwa ile *tender process* imeweza kukamilika.

Suala la pili, alizungumzia hali ya uwanja wa ndege wa Pemba kama ulivyo hauridhishi. Nataka nikubaliane naye kwamba uwanja wa ndege wa Pemba hauridhishi kwa maana ya mfupi, hauridhishi kwa maana sio mpana na hauridhishi kwa maana ya majengo. Serikali hatukukaa kimya tuko mbioni *(Makofi).*

Mhe. Spika: Tumsikilize ili tujue hizo mbio zinakwendaje. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Nataka niwaambie kwamba ni mbio za kweli kweli. Tayari tumepokea Kampuni ya Uturuki ambayo wameshaleta MoU yao, pesa kutoka Exim ya Uturuki, ambayo MoU hiyo tumeshaiwasilisha kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu ili aipitie na aweze kutupa ushauri tuweze kukaa nao na hatimaye tukikubaliana tuwape wao.

Lakini jana mchana baada ya kutoka sala ya Ijumaa nimepokea MoU nyengine Kampuni ya Wachina, ambao na wao vile vile wanataka kuufanyia kazi uwanja wa ndege wa Pemba kwa kupitia fedha za Exim ya China.

Mhe. Mwenyekiti: Usichomeke maneno tu Mhe. Ismail Jussa. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ukiendelea kuchomeka chomeka maneno namna hiyo itabidi tukutoe nje bwana, kwa hivyo utulie kidogo usikilize.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mwakilishi wangu namuomba kidogo avute subra, anisikilize mpiga kura wake.

Mhe. Mwenyekiti, uwanja wa ndege wa Pemba tunachotaka kukifanya, kwanza kuongeza *running way* ili ndege aina ya *boeing* 737 ziweze kutua. Lakini la pili uwanja wa ndege wa Pemba ni mfupi kwa wale waliokwenda Pemba, sio mpana, tunataka tuuongeze upana kwa mujibu wa viwanja vya ndege inavyotakiwa. Lakini la tatu, uwanja wa ndege jengo lake sio zuri. Tunataka tujenge jengo la kileo. Lakini hayo yote yamo katika mikataba yetu na hao ambao tutakuja kuwapa hiyo kazi ya kufanya.

La nne, kuna wafanyakazi ambao hawawezi kuondoka pale uwanja wa ndege, tunataka tuwe na *flat* za kuweza kukaa katika maeneo hayo tujenge. Vile vile tunataka kuimarisha Zimamoto, Zimamoto iliopo ni lazima iimarishwe. Haya yote yako kwenye *package* nzima ya kuimarisha uwanja wa ndege. Mimi nataka nimuhakikishie dada yangu kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu anaufanyia kazi ule mkataba, akimaliza kuufanyia kazi sisi wizara zetu mbili, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Wizara ya Miondombinu na Mawasiliano, tutakaa na hawa wanaotaka kutusaidia kujenga kwa kupitia Exim za nchi zao ili hali ile iweze kuwa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina imani kubwa sana kwamba katika kipindi cha mwaka huu wa bajeti basi tutafikia pahala pazuri na uwanja wa ndege wa Pemba, lakini kwanza kama alivyosema Mhe. Waziri acha tuanze na kuziweka zile taa. Tayari tumeshamuelekeza *DG* kwamba zile taa ataziweka pembeni kidogo ili asiingie kwenye yale mashikio ambayo tutakayoongeza uwanja wa ndege, hilo tumeshakubaliana kabisa. Kwa hivyo, nadhani kazi itakuwa imeendelea vizuri, namuomba kidogo awe na ustahamilivu kazi tunakwenda nayo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, *maneno mazuri ya kumtoa nyoka pangoni*. Lakini kwanza Mhe. Waziri aliponijibu kasema yeye ana hamu zaidi. Yeye hana hamu. Hapo nyuma alipokuwa *backbencher* alikuwa

na hamu kubwa sana, lakini sasa hivi ni Waziri ambaye anatakiwa achukue hadhari kubwa sana kwa upande wa Pemba, kwa sababu na yeye anatokea huko huko sasa hivi hamu imempotea. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu alisema kwenye kikao hiki hiki kwenye suala lake, tulimuuliza swali la nyongeza. Lakini mimi nasema tu Mhe. Mwenyekiti, nyinyi kama serikali imepanga mipango yake tuombe uhai na uzima. Mwenyezi Mungu atupe uhai na uzima, lakini, lakini la pili hiyo, lakini nimuulize Mhe. Waziri. Hivi sasa tumefikia miaka 49 je, haitokuja kufikia tena miaka 49 mingine, hivi sasa ni miaka 49, sasa vitukuu vyetu wakati huo mimi nitakuwa nimeshaliwa na mchwa zamani sipo tena, watakuwa ni vitukuu je, haitokuja kufika wakati huo.

Naiomba sana serikali tutizame mbele Mhe. Mwenyekiti tuwe na *vision*, kile ni kisiwa vile vile na ni kisiwa ambacho kinazalisha. Maana yake msiseme mengi kinazalisha. Kwa Pemba ni kisiwa pekee ambacho kinachozalisha karafuu, zinatumika kwa Unguja na Pemba, serikali ikitupie macho kile kisiwa, kwa miaka tunayokwenda sasa hivi sayansi na teknolojia tusibakie na kiwanja kile, tuwe na kiwanja cha kimataifa katika kisiwa cha Pemba sio dhambi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo aliyonipa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, maelezo ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano sikubaliani nayo. Nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa sababu yeye ndiye anayepanga mipango, na yeye ndiye mtumiaji wa fedha wa kufanya mambo yote. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea. Nilitaka niseme kwamba msimuonee Mheshimiwa hatuna vipimo vya hamu. Lakini sote tuna hamu. Haya tunaendelea.

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	1,277,000,000

Kifungu 040

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia eneo hili nilizungumzia Kampuni ya Zantel, na nikamuomba Mhe. Waziri anieleze, hivi ni kwa nini tunapozungumza Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu, serikali haitaki kutusikiliza. Niliuliza swali hili Mhe. Mwenyekiti, pale ambapo Wajumbe wako tuko Kikwajuni, tukasema Kampuni ya Zantel inahama Zanzibar na kuhamia kwa wenzetu na ishara zilipotokea ni pale

ambapo wafanyakazi wa Zanzibar walifukuzwa kwa kundi kubwa mno, wafanyakazi wa Zanzibar walikataliwa kupewa mikataba na hatimaye yakatokea yaliyotokea.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anisikilize. Hivi sasa *documents* ya wafanyakazi 128 imeshasainiwa wafukuzwe na wote ni Wazanzibari. Mhe. Naibu Waziri hili hakulitaja kwenye majibu yake. Hivi sasa kuna muajiriwa kutoka kwa mwenzetu mmoja *partner* mwengine wa kampuni hii kutoka nchi ya Asia, bwana huyu kaja na kasi ya ajabu kuhusu Wazanzibari, na neno ambalo limeniudhi mno ni pale aliposema, *I dont like Zanzibaris are lazy*. Mhe. Waziri kauli hii anaikubali ilitolewa au laa Mhe. Mwenyekiti, nataka maelezo.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka kidogo tusaidiwe utaratibu hasa kutokana na fungu hili kwa sababu kuna hoja nyingi kama ulivyoziona. Mhe. Mwenyekiti, kitu anachokizungumza nadhani hasa ZIPA, sijui utaratibu unasemaje kwa sababu nina wasi wasi, hoja moja ndio una hesabu Mhe. Mwenyekiti hiyo isije ikaja hoja ya pili na ya tatu ikawa sisi wengine tumeshakosa katika wizara hii.

Sasa lakini msije mkaniambia mimi Waziri, hapana! Nauliza tu utaratibu. Hii hoja katika masuala ya *investment* ya Zantel ZIPA si wanahusika zaidi, kwa sababu Mhe. Waziri naona hili hata akilitolea jawabu. Tatizo langu mimi ni katika hili fungu tu Mhe. Mwenyekiti, usije kutuambia moja hiyo, hoja ya pili hiyo na hoja ya tatu halafu tena sisi tukawa ndio tumesharambwa. Naomba utaratibu tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, si mawaziri wapo wanafanya kazi kwa pamoja. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo yupo ndio Mwenyekiti, sasa sema kama kuna majibu ambayo hayakuridhisha kuhusiana na suala hili. Mhe. Waziri maelezo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sisi kwa upande wa *ZANTEL* wizara yetu imeungana katika sehemu ya teknolojia na sehemu inayohusiana na mambo ya minara, na kuhusu uendeshaji itakuwa ni Wizara ya Fedha ambayo ni *share holder*.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, maswali ambayo ameyauliza Mhe. Asaa Othman Hamad tokea siku ya mwanzo kabisa hadi hii leo, sisi serikalini tuliyapata kama alivyoyaeleza na tumekuwa tukiyafanyia kazi kwa nguvu zetu zote.

Kwa taarifa tu Waziri mwenye mamlaka ya ajira Mhe. Haroun Ali Suleiman jana alikaa na Uongozi wa *ZANTEL* kuhusiana na hili tatizo la uajiri, nadhani kwa sababu leo hayupo hapa angeweza kulitolea ufafanuzi kwamba amefikia wapi.

Lakini juzi nilikaa na Uongozi wa *ZANTEL* mimi kuhusiana na kuhamisha kodi kuzilipa Bara na niliwapa maelekezo ya serikali, kwamba huyu *CEO* mpya aliyekuja aendeleze utaratibu alioukuta ambao umefanywa na wenzake. Vile vile nilimwambia kama kuna suala lolote lile la kuhamishwa kodi basi asije akalifanya, na nilimwambia mapema kwamba kodi zote lazima zibakie hapa kwa mujibu wa utaratibu tuliokubalina, na kama kuna kesi ya kujibu basi sisi serikali ndio tutakaojibu na wala sio yeye. Kwa hivyo, nilimuelezea hili na nikamwambia *I'm serious* katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuwadhalilisha Wazanzibari nalo pia tulimwambia kwamba aendelee kufanya kazi na wazanzibari, na kama kuna mzanzibari mmoja mmoja ni mvivu basi asi-*generalize* kama Wazanzibari ni wavivu. Kwa kweli hayo yote tumeshatoa maelekezo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama hii haitoshi tumetoa maelekezo pia Makao Makuu na tumeiarifu kuhusiana na *CEO* mpya anavyoendesha utaratibu mzima wa kikazi hapa Zanzibar. Kwa hivyo, mimi mwenyewe, Mhe. Rashid Seif Suleiman Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Ahmed Nassor Mazrui tumekaa pamoja na kulizungumza sana suala la *ZANTEL*.

Sasa tumekaa na Mhe. Ahmed Nassor Mazrui, kwa sababu yeye ni Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na *ZANTEL* inafanya kazi za kibiashara na Mhe. Rashid Seif Suleiman tumekaa naye timu ya watu wa tatu kwa sababu yeye ni Waziri wa sekta ya *ZANTEL*, na mimi ni Waziri ambaye nina *share holder* kama ni serikali na tumelizungumza sana suala la *ZANTEL*.

Mhe. Spika, juzi tu nimem-*brief* Mhe. Rais matokeo ya vikao vyote hivyo tukiacha kikao cha Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na *ZANTEL* ambapo taarifa zake bado sijazipata. Kwa hivyo, ninachomuomba Mhe. Asaa Othman Hamad pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine wavute subra na sisi tunaiangalia *ZANTEL* baada ya kuzungumza naye atakwenda vipi katika utaratibu ambao ametaka kuuanzisha.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, sina sababu ya shaka naamini ninavyoumwa na kukerwa ndivyo ambavyo wanavyokerwa wenzangu. Kwa hivyo, nitasema kwamba ni wajibu wetu kuwalinda watu

wetu na heshima ya nchi yetu, na kamwe hatutoruhusu kwa namna moja au nyengine kudhalilishwa mtu wa visiwa hivi au sehemu moja ya ardhi ya nchi hii. Mhe. Spika, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikushukuru na pia nataka nimshukuru sana leo Mhe. Mwanasheria Mkuu, asubuhi nilikuwa nikimsikiliza amefanya kazi hasa ya Uanasheria Mkuu, naomba ninukuu kidogo Mhe. Spika pale aliposema kwamba "musifikirie Waheshimiwa kwamba wanaohoji serikali kama wanaichukia serikali na wala musifikirie kwamba unampelekea hoja zangu fulani kama anaichukia serikali". Mhe. Mwenyekiti, leo Mhe. Mwanasheria Mkuu tunamshukuru sana umetusafisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika hoja ya *Handling* ya Uwanja wa Ndege. Kwa kweli nimesikia maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu tunakushukuru sana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tunamshukuru leo ameamua na amesimama na tunashukuru sana kwa kuweza kujisafisha. *(Makofi)*

Lakini mimi Mhe. Mwenyekiti, nataka ufafanuzi, na ufafanuzi wangu Mhe. Mwenyekiti ninaoutaka ni kwamba suala la mradi huu au *tender* hii iliyotolewa. Kwa kweli *tender* hii mwanzo ilikuja kwa njia sizo, na tukasema hapa Barazani kwamba tunashukuru sana serikali ikatusikia na kutoa maelekezo kwamba nendeni kafuateni utaratibu wa kawaida kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu juzi.

Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru utaratibu wa kisheria umefuatwa na mpaka mchakato umefikia tamati. Sasa ghafla azigo la Mhe. Waziri na sisi hatukufichi tulijenga hofu, lakini leo tumepata maelezo mazuri sana kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Hoja yangu iko hapa Mhe. Mwenyekiti, inaonesha itakuwa kuna tatizo, na kwa sababu kama walivyosema kwamba serikali iliuita Uongozi wa Mamlaka nafikiri bodi wakakaa nao na wakawapa maelekezo. Lakini inaonesha bodi pengine haikuridhika na hayo pengine waliyoambiwa na serikali, sasa tuulize bodi Mwenyekiti wake nani na amepatikana vipi, pia wajumbe wa bodi wamepatikana vipi na ile sheria ya mamlaka bodi inaitambua kama vipi?

Mhe. Mwenyekiti, baya zaidi kulikuwa na mashauriano makubwa na serikali, kwa sababu hawa waliomba ruhusa baada ya hii kampuni kuonekana kwamba tayari kuna muelekeo wameshashinda hiyo *tender*, kwenye ruhusa hiyo pamoja na watendaji wa serikali wakaenda mpaka Afrika ya Kusini, kwa ajili ya kufuatilia namna gani ubora wa ile kampuni.

Sasa leo hapa tumepata maelezo kwamba yale maelekezo hakuweza kuyafuata na hofu yangu iko hapa Mhe. Mwenyekiti na ndio maana ninataka maelekezo. Mhe. Spika, kwamba tunapitisha sheria na hawa wamefuata utaratibu wa *tender* na *documents* zote zipo na wameshafikia kufika maamuzi pamoja na kupata maelekezo mengine.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti swali langu je, ule utaratibu walioufuata wote waliokamilisha wa sheria, maana yake bora ingekuwa hawajaanza ile *tender* ingelikuwa sawa, lakini *tender* wameshakamilisha. Sasa je, wawajibu nini wale ambao waliomba ile *tender*, kwa sababu baada ya *tender* anayeshinda lazima inatakiwa yapelekwe maelezo kwa zile kampuni nyengine zilizoshindwa na zipatikane na sababu.

Mhe. Mwenyekiti, je hili katika sheria za Kimataifa haliji kutubana sisi kama serikali kuonekana kwamba tumekiuka sheria tulizozitunga sisi wenyewe, sasa labda nipate maelezo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba alileta hoja na akafuatilia majibu na maelezo ambayo yametolewa kwa umakini, kwa hiyo na mimi nimeona kwamba kwa maelezo yake imeelekea ameifahamu serikali. *(Makofi)*

Kwanza niseme kwamba maelekezo ambayo serikali ilitoa haukuwa utaratibu hasa wa *tender*, isipokuwa ni utaratibu wa *concession* na ambao kwa kutumia utaratibu wa watu ambao tunaona wanaweza wakawekeza kuleta *expression of interest*, ili angalau vionekane vile vigezo.

Kwa hivyo, hili lilielezwa wazi kwamba utumike utaratibu wa *expression of interest* na Mkurugenzi Mkuu akasema yeye haufahamu nakumbuka watu wa *ZIPA* akiwepo Mkurugenzi Mtendaji wa *ZIPA* akasema sisi tutamsaidia, hawa wote wapo na maelezo yao yanaweza yakapatikana wakaelezwa kilichotokea na wengine walikuwepo wakati maelekezo hayo yalipotoka.

Lakini ikienda kimya kimya mpaka ikatoka *tender*, sasa ukitoa *tender* maana yake imetoa kwa *item* moja na ile ilikuwa ni *package* ya mradi wote mzima kwa mwekezaji, lakini imekwenda kuchukuliwa ile *item* moja ya *Ground Handling* peke yake kama ni biashara peke yake moja.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa *tender* wanasheria wenzangu akina Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Ismail Jussa Ladhu watanisaidia. Kwa kweli kisheria *tender* tunasema ni *invitation to offer or to treat*, yaani wewe sio kwamba unayemuambia mtu akubali lile unalolitaka, isipokuwa unamualika mtu akuletee *offer*. Sasa utaratibu wa kawaida mtu ukimwambia

kwamba nataka kununua nyumba yako maana yake ile ni *offer,* akikwambia sawa, maana yake umeshakubaliana hapo na wakati mumekubaliana na bei.

Kutokana na hali hiyo, utaratibu wa *tender* kisheria tunasema ni *invitation to treat*, yaani unamualika mtu akuletee *offer* na *offer* haiwi mkataba au makubaliano mpaka itakapokubaliwa. Kwa hivyo, ukishaikubali pale hakuna kuakhirisha. Kuna Jaji mmoja maarufu anasema yeye kwamba "*Acceptance is to offer what a lighted match is to a tray of govern powder; they both do what cannot be undone".*

Mhe. Mwenyekiti, ukiikubali *offer* ni sawa na iliyewasha kibiriti kwenye baruti hakuna kughairi tena na kitakachotokea nini? Ni moto. Sasa hapa kilichotolewa ni *offer* ni watu kualikwa kuleta *offer* zao na kama hujamwambia mtu kwamba umeikubali *offer* yake basi hapo bado hapajakuwa na makubaliano. Kwa maana hiyo, *tender* yoyote inaweza kuwa *revoke* au kuakhirishwa wakati hujamwambia mtu kwamba *tender* hii wewe ndiye uliyepewa bado hapo hapajakuwa na makubaliano.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hilo alikuja Mhe. Waziri ofisini kwangu, pia alikuja Mwenyekiti wa Bodi, Mwanasheria wao pamoja na ofisa wao mmoja kutafuta ufafanuzi kuhusu hili na hayo ninayoyaeleza hapa ndiyo hayo ambayo niliyowaeleza. Kwa hivyo, nilitegemea kama hawajafahamu watafute mwanasheria ambaye anafahamu zaidi awafahamishe.

Sasa kama wana malalamiko labda hicho kitakuwa kitu chengine, lakini hicho ndicho ninachokifahamu, na kama walikuwa na maswali pengine wanaona *AG* labda yuko, la Balozi basi wangetafuta mshauri huru wa kujitegemea, ili wakapata ufafanuzi na hili jambo serikali ikaweza kuendelea nalo. Mhe. Mwenyekiti, ni hayo tu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia kwa mara nyengine tena maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Sasa mimi hoja yangu iko pale, serikali kwa kuwa imeshatoa maelekezo, lakini hawa watendaji wanapoondoka kwenda nje ya nchi mimi ninavyojua utaratibu wanaomba ruhusa, na hawa waliomba ruhusa kwamba wanakwenda kuikagua kampuni ambao wao wenyewe kama waliambiwa wasitoe *tender* wao walikuwa tayari wameshatoa *tender* wakaenda kuwakagua.

Kwa hivyo, je kama serikali iliwaruhusu wale kwenda kufuatilia katika hiyo kampuni ambao wao waliitisha *tender* ambayo hawakuambiwa si ndio upotevu wa fedha za umma. Mhe. Mwenyekiti, kama wangelikuwa wamekwishaambiwa musitoe *tender* basi nafikiri hata ile ruhusa ya kwenda Afrika ya Kusini wasingepewa.

Lakini serikali wamewapa ruhusa na wamekwenda Afrika ya Kusini, ndio maana wale wakawa na *confidence* kwa kuwa serikali iliwapa ruhusa ya kwenda kufuatilia hiyo kampuni kwenda kujiridhisha na ule uwezo wa kampuni, mpaka leo imekuwa kama mbuzi hataki kuvuka mto.

Sasa kama hii bodi leo imeshafika pahala inavutana na serikali, kwa sababu bodi wanaona wako katika sheria Mhe. Mwenyekiti, serikali na wao kwa utaratibu waliotoa maelekezo haukufuatwa. Mhe. Mwenyekiti, nadhani tuelezwe hapa kuna nini? Nafikiri nipate maelezo ya ziada, kwa sababu kuna ruhusa bila ya shaka lazima imetoka, kuna watendaji katika *level* fulani mimi ninavyojua hawezi kusafiri nje ya nchi bila ya ruhusa ya serikali, hivi ruhusa walipewa na nini?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako. Kwa kweli ziara hizi Mhe. mwenyekiti, zinajulikana kwa jina maarufu linaloitwa *Due Diligence*, ziara za kujiridhisha wewe unayetaka kumchukua yule *contractor* au kampuni kuja kukufanyia kazi yako. Mhe. Mwenyekiti, hizi kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu maana na mimi nagema hapo hapo kwamba ni *offer* zinatolewa kwa zile kampuni.
Sasa serikali hapa ikiwa ziara ile ni rasmi umeiomba serikalini na kwa madhumuni yake na unataja nani atakayelipia, basi serikali mara nyingi huwa inatoa fursa. Kwa mfano, Kamati yetu ya Kushughulikia Uundaji wa Meli tulifanya ziara na tulikubaliana na mpaka tukafikia pahala pazuri na Kampuni ya *Daewoo* ya South Korea na tukawaambia hatumalizi maneno haya mpaka tuje tuwakague mnao uwezo na hiyo ndio inayoitwa *Due Diligence*, tumekwenda baada ya kumaliza ziara ndio tukatia saini ule mkataba. Kwa hivyo, hizi zinafanyika na wala haina maana ukimaliza ziara wewe inakuwa unawajibika kuichukua kampuni ile. *(Makofi)*

Vile vile tumekwenda sisi Netherlands hatukulazimika kuichukua kampuni ile, na tumerudi na serikali imeona kwamba kwa kampuni hii kwa bei yake haituhalisi basi tunaachana nayo kwa wema na amani. Kwa hivyo, hilo si suala la ajabu la kufanya ziara hiyo, kwa sababu ni ziara yenu nyinyi inayowapa fursa kwenda kuikagua ile kampuni na uwezo wake, ili mukiipa ile *tender* mujue kwamba na hapa wamefanya na hichi pia wamefanya. Nadhani hayo ndio maelezo yenyewe nashukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, inaonesha Mhe. Waziri hakunielewa, mimi najua kuna hizo *offers* anazosema.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nenda moja kwa moja kwani tatizo lako nini?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, sawa. Tatizo langu ni kwamba mtendaji yeyote anapoomba ruhusa kwenda safari anaeleza na madhumuni yake na serikali imeshatoa maelekezo kwamba kazi hii iko nje ya utaratibu wa *tender* na iko kwenye utaratibu huu maalum ambao ameutaja Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Kwa hiyo, ina maana hiyo ruhusa ndio maana mimi nikauliza kwamba hii ruhusa walipewa na nani kwa sababu unapoomba ruhusa sio kwenda kutembea tu kwenye makampuni na ingekuwa siku zote watu wanaruka kwenye ndege, isipokuwa lazima unaeleza na yale madhumuni ya ile safari yenyewe. Lakini kama serikali imeshasema katika eneo hili tunataka hapa ndio maslahi ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hiyo barua waliyoeleza wao wanakwenda Afrika ya Kusini walieleza vipi mpaka wakaruhusiwa, kwa sababu kama wameruhusiwa kwenda kwenye hiyo kampuni ina maana serikali aidha ilikuwa na *options* mbili. Kwa hivyo, *option* ya mwanzo ni ile ambayo waliyoelekeza serikali na *option* ya pili ni ile waliyoiona Mamlaka au Bodi. Sasa hapa inaonesha Mhe. Mwenyekiti, aidha huyo aliyetoa ruhusa alikuwa hajui anachokifanya na hawa wamekaidi agizo la serikali na wamekwenda wao wenyewe.

Kutokana na hali hiyo, inaonesha Mhe. Waziri hakunielewa, kwa sababu kama ingekuwa wanasema wanakwenda pahala fulani kwa shughuli ya Mradi wa *Handling* ya Uwanja wa Ndege, wangeliambiwa aa! Maagizo ya serikali haya hapa na huko mnakwenda kufanya nini au huko Afrika ya Kusini ndiko iliko hiyo kampuni ambayo serikali iliyoagiza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya nafikiri nikiri kwanza kwamba yaliyojiri mpaka wakaenda sijui. Kwa kweli sifahamu kama waliomba ruhusa maana yote yanaweza kutokea, kwamba mtu anaondoka bila ya kuomba ruhusa na wapo maofisa ambao si lazima wapewe ruhusa na Mhe. Waziri, na inawezekana waliomuomba ruhusa pengine naye ni kaimu au suala lenyewe halifahamu vizuri na inawezekana hiyo lugha iliyotumika katika kuomba ruhusa sio hiyo. Sasa kuna *possibilities* nyingi ambazo zinaweza kutokea. *(Makofi)*

Lakini kama alivyosema Mhe. Waziri hapa ni kwamba jambo la msingi ni kwamba hayo ndiyo yalikuwa maelekezo na kama kulikuwa ni hilo la kwenda kuangalia basi walitakiwa waangalie na wengine pia ambao walitakiwa. Sasa mtu anachopewa maelekezo hakwenda akaangalia uwezo wao na hayo mimi

ndicho ninachokumbuka kama ni kupewa maelekezo twendeni mukaangalie, basi alikuwa aende akaangalie kwa hii kampuni ambayo serikali iliwapa maelekezo, kama ni vizuri kwenda mkaangalia uwezo wao na mkaridhika, mukayaona mapungufu yao na halafu mukafanya maamuzi.

Kwa hivyo, mtu anapokuwa amepewa maelekezo na halafu akafuata utaratibu ambao anajua kwamba mpaka alipokuwa amekwama ndio baadaye anakuja anakwambia na nyote hamjui hichi kilichokuwa kimeendelea.

Hata hivyo, kwenye maelezo yangu nadhani Mhe. Hamza Hassan Juma atakumbuka kwamba hawa watu baada ya kuonekana imechukua muda mrefu ndio wakaitwa kuulizwa vipi, mbona mpaka sasa kimya aa! Bado tupeni muda baada ya mwezi mmoja na mpaka hatimaye ndio likaja likaelezwa hivi kwamba tumefikia hapa na huu mchakato ilikuwa wenyewe siri yao au ni utaratibu wenyewe ambao walikuwa wanaufanya.

Kwa hivyo, cha msingi ninachosema ni kwamba hayo ni mambo ya kwenda kuangalia, kwa sababu *possibilities* nyingi zipo za kwa nini walifika huko ama bila ya kuomba ruhusa wizara ikajua au inawezekana wizara ilijua, lakini aliyekuwa amesimamia pengine suala lenyewe na hizo *possibilities* nyingi zipo.
Nafikiri Mhe. Mjumbe kitu cha msingi ni kwamba hichi ndicho kilichopo, maana wasi wasi hapa ulikuwa ni kwamba kwa nini haya yametokea, nadhani ndiyo iliyokuwa hoja ya msingi na haya mengine ni mambo ya kuyaangalia yalitokeaje na ninaamini majibu yake yanaweza kupatikana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu amekiri kwamba hamjui aliyetoa ruhusa aidha ni wizara au nani, ama huyo aliyetoa ruhusa alikuwa hajui kama anatoa ruhusa kwa madhumuni gani na kuna nini. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ili tuendelee basi mimi naomba sana serikali kwamba wizara hii tumeshazungumza sana, tabia na khulka za watu tofauti, pia na harufu harufu za mambo fulani fulani na ndio maana yanatokea haya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, unapokuwa umeshaambiwa kwamba jamani mbona hapa hebu paangalieni na serikali hamtaki kuangalia na yanapotokezea kama haya, basi Mhe. Mwenyekiti matokeo yake hivi sasa hakuna jawabu na wala haiwezekani leo watendaji wa serikali tena taasisi tofauti na ingelikuwa angalau wizara tu, lakini taasisi tofauti watendaji wa serikali. Mhe. Mwenyekiti, sawa kwa upande mmoja tuseme wizara fulani wao walikuwa pengine huyo aliyewapa ruhusa hajui vizuri wanakokwenda, taasisi nyengine je?

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na serikali nzima kwa jumla kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hapa tupaangalie na utendaji wetu ndani ya serikali, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti masuala kama haya hivi sasa tunaumbuana, yaani *conflict of interest* na siku zote tunazungumza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba tu, ili sitaki nisimame tena, basi Mhe. Mwenyekiti naomba sana lile suala la yule mama ambaye ametaka kuweka kiwanja cha ndege, na nikataja hofu yangu kwamba nani anazuia. Kwa hivyo, kuhusiana na hili nitaomba sana Mhe. Waziri kwa sababu huko hakuna fungu la kuzuia, isipokuwa nitaomba sana Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi suala hili waje walifanyie kazi, ili Mhe. Mwenyekiti tusipoteze muda wako mwingi kwa kuzuia mafungu.

Lakini lile alilolizungumza jengine Mhe. Mwenyekiti la Mhe. Waziri kwamba suala la malipo ya wafanyakazi wa Uwanja wa Ndege. Kwa kweli sikutegemea kama Mhe. Waziri hajui watu wake wanapokea katika mfumo gani wakati ile bodi hata kama inatoa mapendekezo kwamba hawa wafanyakazi katika kada hii na hii walipwe vipi sijui masuala yale anaya-*approve* nani na hilo sitaki jawabu Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napunguza tu hoja zangu na hayo nitaomba yakafanyiwe kazi, ili na wenzangu niwape nafasi. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa utaratibu utaniruhusu basi naomba na mimi nizungumze jambo kwa aina yake tena kwa unyonge sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nilimpelekea mchango wangu kwa maandishi, lakini wakati alipofanya majumuisho hakunitaja na wala sisemi kama anaringa au vipi, isipokuwa najua binadamu mughuma ukikufika hata kofia unaweza kuivaa kwenye mkono badala ya kuivaa kwenye kichwa na hilo siwezi kumlaumu.

Sasa nilimuandikia kuhusu suala la *tender*. Lakini naomba Mhe. Mwenyekiti, nilizungumze kwa namna yake na wala sio kama alivyozungumza mwenzangu, isipokuwa mimi nitalizungumza tofauti. Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, pia nimemsikia Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa kweli niwapongeze kwa lugha nzuri sana walizozungumzia suala hilo.

Hoja yangu iko hapa ni kwamba Mhe. Waziri anijibu kuwa kweli aliandika barua ya zoezi lote kulifuta? Lakini je, kama ni kweli amefanya hivyo au

hakufanya, basi nani sasa nimuamini kwa kauli yake atayenithibitisha mimi, ili niendelee na shughuli hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hebu tufafanulie zaidi zoezi lipi unalolizungumzia.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu zoezi la *tender* na *handling* kwenye Mamlaka ya Uwanja wa Ndege.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mimi ni Waziri katika Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano, ambaye ninasimamia Mashirika na Mamlaka zote na kwa mujibu wa kifungu Nam. 13 cha Sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga kifungu (c) kuhusu *power of the miniter*, naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga kifungu Nam. 13(c) kinaeleza hivi:-

> "*Give particular direction to the board concerning any matter evolving agreement with or the interest of the authority or public*".

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kifungu hichi nimetumia nafasi hiyo baada ya kuona kuna mizozano, na kabla ya hapo mimi napenda kusema kwamba *tender* ilipokuwa inakwenda, maana yake ilianza kabla ya kuingia mimi na ilivyokuwa inakwenda mimi sijaingilia shughuli zozote za *tender*.

Lakini baada ya kukwama, basi Mwenyekiti wa Bodi alinijia mimi na kunitaka ushauri na wao wakaniambia kwamba wanakwenda kufanya kikao na watatoa maamuzi na watanileta, basi nikawaambia sawa hakuna tatizo kama nyinyi ni bodi munayo sheria ya kufanya kikao na kutoa maamuzi. Kwa kweli barua yao ilipokuja haikuwa na maamuzi, isipokuwa ilinitaka mimi niitishe kikao cha wahusika wote kwa ajili ya kulizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kifungu kile niliona haya yafuatayo. Mamlaka kisheria ina uwezo wa kutoa maamuzi, bodi kisheria inao uwezo wa kutoa maamuzi na Waziri kisheria anao uwezo wa kutoa maamuzi, na tukichanganya watu kikao hicho nitakifanya vipi mimi na maamuzi yatatoka kwa sheria gani.

Kutokana na hali hiyo, nikamfuata Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa sababu hili ni jambo la kisheria na tukashauriana na sheria hizi zikapitiwa na ilionekana dhahiri kwamba kwa maslahi ya kifungu hichi, kwa *interest of the public* basi ile *tender* tuisitishe na tuwatake waitishe *tender* nyengine. Kwa hivyo, mimi

kweli nilitoa barua, lakini sio kwa maslahi au manufaa yangu na wala simjui mtu yeyote na sikwenda mimi Afrika ya Kusini wala wapi, kwa hivyo ni kwa maslahi ya nini. Mpaka hivi leo wahusika wote miye siwajui hata kwa sura. Kwa hivyo sina *interest* katika jambo hili, nilitoa barua kwa maslahi ya umma kwa kupitia ushauri mkubwa wa Mwanasheria Mkuu wetu ambaye nafikiri tunamuamini. Nakushukuru.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kama nitakosea naomba radhi sana. Katika majumuisho hayo ya *tender body* na hata kufika safari alikwenda Naibu Katibu Mkuu naye ni mmoja katika muhusika kwa mujibu wa sheria ya wizara yake. Lakini Mhe. Waziri alivyonambia kuwa yeye hakujua taratibu zote mpaka zikafikia hivi, lakini yeye aliamua tu kuandika barua kuzi- *draw tender* zote.

Mheshimiwa sitaki kusema mengi kwa kuwa mimi sina haki ya kuzuia kifungu hichi. Lakini ninachoeleza Mheshimiwa bado narudi tena na namalizia kuwa naomba sana sasa nisikie kauli ya Mhe. Waziri, na hasa iendane na kauli ya Mwanasheria na Mhe. Makamu wa Pili, huyo mtu ambaye wanataka kumpa wao itoke kauli leo niyasikie kwamba tumefanya hivyo na kuanzia sasa tunasema tunampa mtu fulani ili sheria ione.

Mhe. Mwenyekiti: Hii kauli ya kuanzia sasa itoke humu ndani? Wakati mambo yana utaratibu wa *tender* na kila kitu, hapana hii itakuwa ngumu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mwenyekiti, sikajusikia.

Mhe. Mwenyekiti: Nasema hivi unataka Waziri, Mwanasheria na Makamu wa Pili wa Rais, watoe kauli kwamba kuanzia sasa hii atakuwa mtu fulani. Hapa hatuchambui *tender* Mheshimiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: *No, no*, sikiliza, samahani Mwenyekiti wangu. Mhe. Mwenyekiti, kwa alivyoeleza Mhe. Mwanasheria nilivyomfahamu walisema kuwa waliona kuna kampuni ambayo inaweza kufaa na ikaleta tija katika serikali hii na ikaeneza mambo chungu nzima. Sasa wawe wazi hapo, watwambie kuwa huyu ndiye tuliyeona sisi ndiye anafaa. Imekwisha Mhe. Mwenyekiti, hili suala limeshazungumzwa hapa. Kwa sababu tayari yule mtu ameelezwa 1,2,3, sasa sioni tatizo kwa kusema kwamba sasa hivi huyu ndiye anayefaa. Tatizo gani, bila ya kuzunguka huku, kupita huku, Mheshimiwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani umeshatupa muongozo mzuri kwamba suala lilikuwa mazingira mpaka limetufikisha hapa,

lakini sidhani kama kikao hichi ilikuwa ni kujadili nani apewe hasa. Hata hao waliopewa maagizo ya kutafuta utaratibu wa kuzungumza na hao. Ndio maana katika maelezo yangu mwanzo kabisa nilisema kabla ya hao tulizungumza hata na Waturuki, tulizungumza nao muda mrefu na tukafika pahala nao tukaona aah! haikhalis. Pamoja na kwamba serikali ilishakubali Waturuki kwamba waendeshe, lakini nikaona haikhalis baada ya kufuata ule utaratibu wa kuona kwa masharti tunayotaka twende nayo ni sawa si sawa. Na hawa ni hivyo hivyo walichotakiwa ni kutafuta utaratibu wa kuona kwamba je, katika masharti gani, pamoja na kwamba serikali imeshatoa maelekezo hayo, kwamba hawa tunaweza tukafanya kazi nao.

Bahati mbaya huo utaratibu uliotumika wa *tender*, nadhani Mhe. Mshimba atakubaliana na mimi, yeye ni msemaji mahiri, Mhe. Hamza msemaji mahiri na wengine. Lakini nikisema unafuata utaratibu wa *tender* au kutafuta wasemaji mahiri yeye wa mwanzo anaweza akakosa. Kwa sababu sharti dogo linaweza likakutoa kwenye *tender*. Sasa ndio maana huo utaratibu sio huo nilioagizwa, ni utaratibu wa kufanya *open ended discussion* na hawa watu mpaka tufikie pahala tuone tunaweza tukafanya kazi nao kwa yale ambayo serikali iliona muelekeo wake.

Kwa hivyo kama ulivyotuelekeza Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la kulifanyia kazi kwamba tuseme serikali ilifanyia kazi kwa utaratibu huo mpaka itakapofika pahala ikiona kwamba ni sawa ndio itaamua kwamba *okay* sasa rasmi unapewa. Nadhani umetuelekeza vizuri Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tukubaliane kwamba serikali iendelee kufanya kazi, kuliko kutoa maamuzi hapa hivi sasa. Haya ulitaka muongozo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa kidogo niseme kwa sababu Mhe. Waziri pale sijui kama aliteleza ulimi au vipi. Kwa sababu kidogo alikwenda kinyume na maelekezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, na hili nafikiri ndio hilo linaloleta *confusion* yote hii. Kwa sababu Mhe. Waziri hapa sasa hivi katamka kwamba amewaambia ile kampuni izuiwe, watoe *tender* nyengine.

Sasa hili ndilo linaloleta mashaka na hapa sasa hivi kalirejea. Tunaweza tukawalaumu wale kumbe pengine kauli au maelezo wanayopewa. Sasa hebu angeliweka sawa Mheshimiwa kauli yake ili akarekebisha katika *hansard*. Kwa sababu kwa maelekezo ya serikali mimi nafikiri sio tena kutoa *tender* nyengine kwa sababu mlikuwa mmeshapewa muongozo. Sasa leo Mhe. Waziri anaposema kwamba itolewe *tender* nyengine sasa wale watajiuliza kwani ile tumekosea wapi?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mheshimiwa sasa hivi mimi siyajui *exactly* yale maneno niliyoyaandika mle, lakini niliashiria kwamba hii isitishwe mpaka hapo kampuni zote zitakapofanyiwa *security vetting*, hivyo ndivyo ndivyo nilivyoandika. Hata wao walikuja kuuliza mpaka lini. Nikawambia hii haina mpaka ni kwamba mambo yote ya kiwizara yanakwenda kwa majadiliano. Kwa hivyo uongozi ule usitishe. miye nimetumia uwezo wangu wa kuisitisha ile *tender* isiendelee kama kawaida.
Mhe. Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kwamba *tender* haijafunguliwa imefunguliwa na wenye bodi lakini wote hawa wanajua nani aliyepata, sasa sijui zimetoka vipi. Kwa hivyo tunapata fikra tofauti, ndio maana nikazuia, nikasema sasa kutakuwa mparaganyiko bora twende katika hali ya usalama na mpaka leo hali ya usalama imepatikana.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tufuate maelekezo yale aliyoyatoa Mwanasheria Mkuu tuyafuate, na nadhani ndio muongozo ambao serikali wanataka kuufanya. Sasa kuna lile suala ambalo tumeliona hebu kuna Mhe. Salmin Awadh kuna Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Asha Bakari, Mhe. Mbarouk Wadi, Mhe. Hija Hasan Hija, Mhe. Omar Ali Shehe, kanuni yetu hapa tatu zimeshatimia lakini sasa kumekuwa na hoja hizo kama 6 juu ya eneo hili. Labda nitoe muongozo mmoja katika hapa na hii ni *practice* ya Bunge.

Practice ya Bunge huwa wanasema karibu wote halafu Waziri anatoa maelezo inakuwa imekwisha, hiyo ndiyo *practice* ya Bunge. Tena Spika, huwa anataja hasa Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Omar Ali, Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Asha Bakari, mmoja baada ya mmoja halafu yanatoka maelezo inakuwa kazi imekwisha. Hiyo ndiyo *practice* ya Bunge, tukitaka ku-*adopt* hiyo basi itabidi tufanye hivyo. Lakini kanuni yetu hiyo inataka hoja tatu katika eneo moja.

Sasa mimi hapa nilikuwa nafikiri tujaribu ku-*adopt* utaratibu wa Bunge kwa sababu tunaweza tukawa tusifike pahala, nisikie hoja ya Mhe. Ismail Jussa, niisikie na hoja ya Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Asha Bakari na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, leo nafikiri uliniona kwamba natumia utaratibu ambao sio kawaida yangu, katika kutaka muongozo wako kabla hatujaingia katika vifungu kwa sababu niliyahofia haya Mhe. Mwenyekiti. Na ulitukubalia kwamba tukiwa na haja; na haja sasa imejitokeza kwamba tutarudi katika Baraza kuja kuweka kando kanuni.

Hilo Mhe. Mwenyekiti limeshaingia katika *record* zetu. Sasa nahofia na wewe Mwenyekiti wetu ukaingia katika *record* ya Waheshimiwa Mawaziri wetu kwamba leo wanatwambia hivi kesho wanatwambia vile.

Mhe. Mwenyekiti, msingi hasa anapokuwa Mjumbe kazuia fungu kuna utaratibu wake wa kulionesha hilo fungu ambalo umelieleza katika kanuni ya 98 ambapo kunahitajika maelezo, ikiwa hujaridhika na Waziri, aje kiongozi wa shughuli za serikali na mwisho kuna kura. Sasa kwa utaratibu unaotupendekezea Mhe. Mwenyekiti, kwamba utuchukulie kwa pamoja halafu akishatwambia Mhe. Waziri iwe ndio basi, tutakwenda kama ndo hivi tunafanya mjadala mpya, kwamba nasimama hapa kwa sababu sikuridhika na maelezo yake ya majumuisho. Kwa hivyo nina haki ya kusimama mara tatu katika hoja yangu ili tufikie mwisho huo ndio msingi wake.

Sasa nilitambua kwamba kutokana na ufinyu wa vifungu vilivyokaa humu ndani itatuwia vigumu. Ukatukubalia Mhe. Mwenyekiti, basi ikiwa kuna haja tukifika hapo pahala na Mhe. Omar Ali Shehe alitoa hoja kwamba tutenge kabla, ukasema isitolewe hoja. Sasa hapo ndio penye hoja zetu zote. Mimi ningekuomba sana Mhe. Mwenyekiti, tukasimamia ile kauli yetu ya mwanzo tukarudi tukatengua kanuni kando. Sikuingilii mamlaka yako ukasema ngapi lakini kwamba zisiwe tatu tumeshakubaliana ningeomba tulisimamie hilo Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo tutenge kando kanuni ziwe hoja tisa sasa, ndio tunachozungumza hapa, kwa sababu kuna Wajumbe tisa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nasema mamlaka ni yako lakini itategemea namna hiyo kanuni itakavyotengwa kando. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka hata Mhe. Mwanasheria Mkuu alipoeleza wasi wasi kuwa tuna- *create precedent*, muongozo ukasema tutakapotengua, msingi wa kutengua unakuwa kwa jambo lile lilotenguliwa kwa wakati ule tu, ikimalizika tunarudi katika utaratibu wa kawaida.

Kwa hivyo kutokana na muongozo wako ule ndio maana sote tukaridhika tukasema tuendelee. Na nakumbuka Mhe. Hamza aliuliza tunaendelea kwa utaratibu gani. Ukatuongoza kwamba ni utaratibu huo kwamba tukiwa na haja. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hiyo haja ishajitokeza sasa hivi, mimi ningeomba sana tukayaheshimu yale tuliyokuwa tumekubaliana turudi. Sasa ngapi kama ziwe tisa kama sita hilo Mhe. Mwenyekiti, ni suala la mamlaka yako na kiti chako utueleze. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kuna Mhe. Waziri anayetaka kusema kitu.

Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tuna kanuni zetu tunazozitumia sana katika kuongoza mambo yetu na tumefanikiwa sana. Naamini leo kwa sababu pana hoja mahsusi hapa ndio maana Waheshimiwa wanaomba mazungumzo mengi zaidi kuliko utaratibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi niseme mengi waliyosema Waheshimiwa serikali imeyasikia. Nia na madhumuni ni kuyafanyia kazi na wala kusiwe kuna dhana kwamba kuna jambo linazungumzwa na Baraza hili halafu serikali huwa haiyafanyii kazi. Serikali yote yanayozungumzwa hapa inayafanyia kazi lakini kwa utaratibu wake kwa mujibu wa sheria ambazo tunazitunga hapa na vile vile kuhakikisha kwamba tunatenda haki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba hayo yote yatakayozungumzwa tayari yamezungumzwa na tumeyasikia, kwa hiyo si vizuri sana kujitengenezea taratibu ambazo huko mbele zinaweza kutupa matatizo. Mimi ningeomba tu basi kama ni kuongeza Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu huu na kwa hili basi tuongeze angalau watatu jumla sita kwa sababu tisa wakiongezeka na wengine itafika saa 9 hatujaondoka hapa na Ramadhani hii.

Ninachoomba ikiwa tuongeze basi tuongeze watu watatu wengine, naamini hoja ni hiyo hiyo, maelezo ni hayo hayo majibu ni hayo hayo. Kwa vyovyote vile maelezo yatakayotoka hapa tutayafanyia kazi. Maana ya kufanya kanuni ya hoja ya watu watatu tulifanya hivyo kwa makusudi, wengi tuliona umuhimu wa kuzungumza mambo kama haya yangetosheleza sana kwa watu watatu tu ndio maana tukayaweka katika kanuni zetu. Tusitengeneze utaratibu ambao baadaye ukatuwekea katika hali ambayo huko mbele tukapata magumu zaidi katika kutengeneza. Kanuni hizi zimetuongoza vizuri na tumefanya Baraza letu limekwenda vizuri.

Naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa tuongeze watu watatu, basi baada ya hapo tujue hoja hii imemalizika twende na hoja nyengine. Vyenginevyo basi bora tupige kura tuweze kuamua hili. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa hali tunavyokwenda hivi kimsingi bado tunahitaji maelezo, hakujawa na hoja ya kusema kwamba tunazuia fungu moja kwa moja; hoja zetu zote ambazo tunakwenda nazo, hatujawa na hoja ama ya kupunguza ama shilingi moja kwa sababu ya matumizi mabaya wala shilingi mia moja kwa sababu ya kukataa sera. Hilo tulikumbuke kwanza tunahitaji maelezo.

Pale niliposema kwamba katika utaratibu wa hoja zetu tatu labda tuchukue hoja kwa mpigo tupate maelezo halafu tuendelee. Kwa sababu bado hakuna

hoja ya kupunguza fungu hapa. Hilo moja kwanza tulielewe na hilo ndio imo kwenye lile fungu la 98(6)(a) (b) iko hivyo.

Jengine ni kwamba nilisema kama itakuwepo dharura kuna hoja nyingi lakini ziwe ni hoja. Sasa hatujawasikia Waheshimiwa Wajumbe nini kinachotaka kusemwa, lakini kuna hoja kama sita. Ni juu yetu kusema kwamba *okay* kwa dharura hii tuongeze hoja 2,3, kama itakavyokuwa, lakini tukifungua mlango hapa zinaweza zikaja hoja nyingi sana. Kwa sababu waliochangia ni wengi kwa kuwa fungu fulani maalum nitakalolizuia wengi wanaweza wakasema chini ya fungu hili hili la Uendeshaji, nia na madhumuni yetu ni kwamba shughuli hizi ziende kwa ufanisi tumalize, maelezo yapatikane ili Waheshimiwa tufikie pahali tunapitisha kitu hichi ili wizara ifanye kazi.

Sasa tukubaliane nitarudisha Baraza, Mhe. Salmin una jambo la kuchangia kabla hatujarudisha Baraza.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka kusema kwamba nilipochangia nilisoma kifungu cha 98 kwa lengo la kuondosha fungu la shilingi mia ikiwa hoja za Mhe. Waziri hazikuniridhisha. Kwa hivyo nataka nitofautiane kwamba Wajumbe wote ambao wamechangia hakuna Mjumbe au mtu aliyeeleza azma hiyo. Nilianza na azma hiyo na bado kama sikuridhika nitaendelea nayo.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka kutumia kanuni ya 156 ya kuliomba Baraza lako tukufu litumie kanuni hii kuweka kanuni kando ya 98 kifungu kidogo cha 3 ili Waheshimiwa Wajumbe waendelee kutoa hoja zao katika idara hii mpaka pale ambapo wataridhika kwamba hoja zao zimejibika. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hoja turudi kwenye Baraza, ili hoja chini ya kifungu hicho itolewe. Hapa sipo. Na tujue kwamba hii ni hoja ya dharura hatuweki kuwa ndio *open check, no!* Ni dharura ya hapa. (*Makofi*)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Sasa kwenye Baraza ndio hoja kama hizo za kutenga kanuni kando hutoka. Sasa tupo Barazani tumeondoka kwenye Kamati. Shughuli hizi ziende pamoja na masuala ya uendeshaji wa shughuli za serikali. Nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutoa hoja hiyo inayohitajika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Tupate maelezo kidogo.

Mhe. Spika: Tulikubaliana wakati tupo kwenye Kamati ya Matumizi kwamba itakapotokea haja kwamba kuna hoja nyingi katika eneo fulani, kanuni yetu inaruhusu hoja tatu, hapa zimetokezea hoja nyingi zaidi ya tatu. Tunakusudia shughuli zetu hizi isiwe kazi yetu kuchukua hoja tu hapa na pale, hapana. Tufikie pahala zile hoja tuzikisie ni ngapi ili hatimaye tuweze kuendelea mbele. Hoja tatu imeonekana hazitoshi kwa dharua hii, sasa hoja zile tatu zipo kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (3). Sasa tunataka tuitenge kanuni hii kando ili tuongeze hoja kiasi ili hatimaye tuweze kufikia angalau pahala ili tupate nafasi ya kupata maelezo zaidi ya serikali, nikisema serikali pamoja Waziri pamoja na mawaziri wengine. Kwa hiyo nataka nimuombe anaanza kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutoa hoja hiyo ya kutenga kanuni kando; kanuni 98 (3) ili kupata wasaa wa kuongeza hoja kiasi ili tuweze kupata maelezo ya ziada ya serikali katika eneo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa jambo hili umelieleza vizuri sana, na kwa kuwa pamejitokeza mahitaji ya kupata ufafanuzi zaidi, na hasa pale uliposema kwamba kwa kuwa mpaka sasa haijajitokeza hoja inayoonesha kuondoa fungu kwa msingi huo Mhe. Spika, tulishauri jambo zuri sana. Ingekuwa ni vyema tukawasikiliza Wajumbe halafu baadaye Waziri akajibu. Lakini ilionekana dhana hiyo pia baadhi ya Wajumbe wanagunaguna. Kwa msingi huo Mhe. Spika, basi bado serikali na kwa ajili ya kupata ufafanuzi zaidi, na kwa ajili ya muda pia tunaomba tuweke kando hii kanuni ya 98 (3) ili tuweze kuongeza hoja nyengine 3 ili naamini itaweza kukidhi haja za wale wenzetu wengine wengi.

Kama tutasikiliza wote Mhe. Spika, na muda na ninavyoamini bado hoja zenyewe zote zitakuwa ziko za aina moja. Kwa hivyo naomba tukubaliane na Baraza lako tuongeze hoja nyengine tatu kwa sababu ya jambo hili. Baada ya *issue* hii tuendelee na utaratibu wetu wa kawaida. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Nagawa hoja tatu,

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Asha Bakari Makame

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa busara zako na hekima zako za kuendesha hiki kikao.

Mhe. Mwenyekiti: Tena tukubaliane kwamba, hebu Mheshimwa kaa kidogo. Tukubaliane kwamba wakati mwengine zile hoja hapa watu hupandishia hivi, ikawa sasa kuna rundo la hoja. Hapana ni moja moja Mheshimiwa endelea.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri nilizungumzia suala la wafanyakazi sita wa Shirika la Meli ambao walitakiwa na serikali warudishwe kazini na hadi leo hii hawajarejeshwa kazini.

Nimemsikia Mhe. Mwanasheria akinijibu suala hili kwa ufasaha sana na kueleza kwamba suala hili ni la muda mrefu tokea 2001, akasema ingekuwa kama ni suala la ardhi basi lingekuwa haliwezi kupuuzwa, lakini ninachotaka kusema kwamba suala hili ni la mwaka 2001 lakini sio kama lilikuwa limesimama ni suala ambalo tokea kipindi hicho linaendelea, nalo si suala kwamba limeanza kuzuka leo suala ambalo linaendelea.

Lakini pia alizungumzia suala la kwamba suala hili liko Mahkamani, akataja kifungu cha kanuni hapo ambacho kinakataza kuzungumzia jambo ambalo liko Mahkamani. Mhe. Mwenyekiti mimi sikutaka kuzungumzia suala ambalo liko Mahkamani, niliuliza masuali mawili ambayo hayawezi yakaathiri shughuli nzima ya utoaji wa haki. Nilimuuliza Mhe. Waziri kwamba ni sababu gani zilizopelekea uongozi wa Shirika la Meli kukaidi agizo la Mwanasheria Mkuu la wale wafanyakazi kuwarejesha kazini, ikiwa ni pamoja na Kaimu Mkuu wa Upelelezi wakati ule kwamba wafanyakazi wale warejeshwe kazini, jambo ambalo suala lile baadae lilikwenda mahkamani na kusababisha Shirika lile kupewa adhabu amri ya Mahkama Kuu ya Zanzibar, Mahkama ya Rufaa mara mbili imekwenda kutaka shilingi milioni 45 kila moja alipe kwa wafanyakazi sita, jambo ambalo lingesababisha hasara ya shilingi milioni 270 na hizi zipo hatutoki, hapa hatutoki Mhe.

Kwa sababu kesi hii imesikilizwa na Mahkama Kuu, kesi hii imesikilizwa mara ya kwanza na Mahkama ya Rufaa ikarudia tena Mahkama ya Rufaa, maamuzi hayo bado yamebakia pale pale. Na nikataka kuuliza je fedha hizi ambazo Shirika, serikali, fedha za umma imeingia hasara atawajibika kulipa nani, maana yake hapa pamefanyika uzembe wa makusudi. Sasa mimi nilikuwa nataka masuali mawili hayo kwamba sababu iliyowapelekea

wafanyakazi wale wasirejeshwe kazini, ilhali serikali kupitia Mwanasheria Mkuu na Mkuu wa Upelelezi alisema kwamba hawa hawahusiki, wanaohusika hawa, na uongozi wa Shirika ukakaidi kufanya shughuli hiyo jambo ambalo lilisababisha Mahkama Kuu, Mahkama zote mbili za rufaa kuagiza watu wale walipe fidia ya shilingi 45 kila mmoja ambapo jumla ya shilingi milioni 270 zinatakiwa zilipwe nilitaka kujua pesa hizi atazilipa nani kwa uzembe ambao ulifanywa na uongozi wa Shirika la Meli? Hayo ndiyo niliyokuwa nimesema. Naamini hayo hayawezi kuathiri ushahidi wa mashtaka ni masuala ya utendaji. Nataka jibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mimi naamini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin anajua kwamba mimi na yeye tunazungumza lugha moja; kwamba suala hili kwa sababu Ofisi yetu mwaka 2011 iliwahi kutoa hayo maelekezo, lakini uongozi wa Shirika ukasema aa sisi tunazo sababu nzuri tu za kujieleza mahkamani. Na Ofisi yetu ikasema basi kama mnazo sababu basi tafuteni wakili awatetee na sasa hivi wana wakili wao anaewatetea sio Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Sasa sababu zao za kwamba kwa nini wao hawakufuata watazieleza mahkamani, tusiwatake wazieleze hapa maana sababu hizo hata wakitueleza hapa sisi ndio hizo hizo ambazo itabidi wakazieleze Mahkamani. Wamekwenda mara ya kwanza wameshindwa, mara ya pili wameshindwa, lakini haujesha huu mchakato sisi tutakapofika wakati wa Baraza hili kuwawajibisha ni pale ule mchakato wa kimahkama utakapokamilika. Ndio maana hizi kanuni zetu zikatumia neno marufuku maana tunaambiwa kwenye maneno ukiona limetumika neno fulani basi ujue kilichokusudiwa sio cha kawaida, kuna maneno yakitumika yana maana yake. Na mimi ndio nililosema kwamba hapa hapakutumika neno kwamba tusilizungumze tu ni marufuku.

Sasa kwenye hili mimi ninasema kwamba hizo pesa atalipa nani, tuvute subra, tumeshasubiri miaka 13, huu mchakato uliobaki wa mahkama mimi siamini kama utachukua tena miaka kumi. Tutafika chombo hiki naamini kwamba itakuwa Baraza hili halijavunjwa, na uamuzi wa mahkama utakuwa umeshatoka na wao watakuja hapa kueleza kwamba ilikuaje. Lakini sisi sio kwamba tunapinga hili lakini tunaheshimu hizi kanuni zetu kwamba hili suala pamoja anasema yeye kwamba halitoathiri utoaji wa haki, inawezekana lakini majibu ambayo atatakiwa atoe hapa Waziri ndio majibu hayo hayo itabidi wao waende wakaeleze mahkamani.

Kwa hivyo maadam hili suala ni *sub judice*, liko mahkamani; ni vizuri tuwaachie wakajieleze kwenye huo mchakato halafu na sisi watakuja kutupa maana si neno zuri kutumia. Lakini wengine wanasema *muongo muongoze.*

Wao si kwa sababu ni waongo ni wakweli lakini tuachie huu mchakato ndio hilo tu *point* yangu iko hapo; kwamba majibu yatakayotoka hapa na majibu yatakayotoka Mahkamani nani atalipa ile mahkama yenyewe itasema nani atalipa, Mahkama ndio itatakiwa iseme, hizi gharama alipe nani wala sisi hatutokuwa na haja ya kumwambia Waziri twambie atalipa nani, Mahkama yenyewe itasema na majibu yao itabidi wayatoe huko mahkamani, haya haya ambayo watatwambia hapa. Kwa hivyo busara ipo hapo tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu hebu nisaidie unaniambia kwamba hilo suala bado liko mahkamani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Liko mahkamani.

Mhe. Mwenyekiti: Mahkama ya

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mahkama Kuu lipo, na uamuzi wake utatoka tarehe 17 Agosti, ulivyopangwa, kuhusiana na ombi la kuzuia utekelezaji wa hukumu lakini na pia kuna ombi namba 42 la mwaka 2013 mbele ya mahkama ya rufaa.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Waheshimiwa Wajumbe kuna baadhi ya kanuni hata tukisema tutenge kando inakuwa si sahihi moja hii ya marufuku, na kwa sababu hii imewekwa ili kulinda uhuru wa mahkama nadhani ndio hivi. Sasa kwa kuwa uhuru wa mahkama uko kwa mujibu wa katiba, sasa itabidi hili suala tufikie mwisho hapa tulipozungumza kwa kuwa tuna uhakika, ila kama kuna mtu atasema kwamba lishaondoka mahkamani. Lakini kwa kuwa liko mahkamani na tunaamini hivyo basi mjadala wa hoja hii Mhe. Salmin tunaufunga.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nashukuru kama hatimaye umeniona. Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia nimechangia hoja nyingi lakini hoja ambayo nimeisimamia sana ni hoja ya mradi wa ujenzi wa jengo la abiria kwa maana ya *Terminal II*, nashukuru nimesikiliza kwa makini sana maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo yamekuja kuthibitishwa na Waziri kama ndio pia maelezo yake kwa hoja hii.

Mheshimiwa nasikitika sana sana na kwa hili kwa sababu yale maelezo ya kina aliyokuwa ameyatoa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, na kwa sababu Baraza hili linapaswa lisimamie maslahi ya wananchi wa Zanzibar ndio maana niliomba muongozo wako mapema juu ya kile kifungu cha sheria ile ya Haki, Kinga na Fursa. Ningeomba unistahmilie kidogo Mheshimiwa ili nizi-*counter* zile *argument* ambazo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha

Uchumi na Mipango ya Maendeleo kazieleza katika Baraza hili. Lakini kwa ufupi sana Mhe. Mwenyeiti kadiri nikavyoweza ili chombo chako kifanye maamuzi sahihi katika kuisimamia serikali.

Mhe. Mwenyekiti pameelezwa maelezo mengi lakini yote mimi ninayafanyia muhtasari mmoja tu kwamba yana lengo la kutaka kuhalalisha maamuzi ya kisiasa badala ya kulinda maslahi ya wananchi wa Zanzibar na fedha za wananchi wanyonge maskini wanaotozwa kodi kila siku wananchi wa nchi hii.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti tuelewane kwamba huu si mradi wa ufadhili huu ni mradi wa mkopo, kwa hivyo huu ni mradi wa wananchi wa Zanzibar fedha zao hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti sasa nije katika maelezo, katika maelezo tulichoambiwa kwa muhtasari ni kwamba tulikuja na mfumo wa *design and build* ambao kuwa hatukuwa na uzoefu nao, kwamba kampuni ile ambayo imechukuliwa mwanzo ya mshauri Mwelekezi ATM kutoka Uturuki yeye mwenyewe hakuwa na uwezo mzuri na katika kifungu kile, vile vile hakujakuwa na kifungu kinachohusu katika kazi zao cha ku-*approve design* za jengo na hatimaye ikapelekea hatua ile, lakini pia akatolea na maelezo ya mwisho kwamba tukifanya vyenginevyo tutaathiri mahusiano yetu na Jamhuri ya watu wa China ambao ni rafiki zetu na tuna mahusiano marefu.

Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka kusema kwamba hoja zile si sahihi na ndio maana nataka maelezo zaidi kwamba kwa nini serikali imefanya maamuzi haya, kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilisema katika mchango wangu kwamba Kampuni ya mwanzo kabisa ilikuwa ni *Frederic Know International* ya Uingereza ambayo ilitakiwa ifanye mapitio, na ikafanya mapitio na ikatoa waraka wa kurasa 150. Na mengi yaliyokuja kujitokeza baadae yalishaelezwa katika kampuni ile ya *Frederic Know International* katika ripoti yao.Watendaji Wizara na wakuu wa wizara hawakushughulika kwa sababu labda hakukuwa na maslahi nayo tukaingia katika uoza ule.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti imetolewa hoja kwamba ikiwa tunasema hatukuwa na uzoefu basi ndio inathibitisha kuwa hoja yangu kwamba Wizara hii ivunjwe yote. Kwa sababu kwa nini watendaji wa Wizara wakiongozwa na uongozi wa wizara uliingiza serikali na wananchi wa Zanzibar katika hasara wakati wanafanya maamuzi kwa jambo ambalo hawana uzoefu nalo, hawalijui.

Lakini la tatu Mhe. Mwenyekiti lililosemwa ni kwamba huyu ATC huyu ATM hakupewa kazi hii kwa hivyo hakuwa milioni. Mheshimiwa nilitoa

katika hoja yangu kwamba tunaendelea kuwaingiza wananchi wa Zanzibar katika hasara kwa kuendelea kuleta washauri elekezi ambao wanaendelea kupendekeza lile linakuwa limeshaonekana. Sasa kuthibitisha hoja yangu Mheshimiwa halafu nikae nipate maelezo.

Mheshimiwa ADPI hawa Wafaransa walioletwa washauri elekezi wa mwisho hawa wamewasilisha ripoti yao tarehe 24 Mei 2013 hii hapa. Wakapendekeza kwa sababu ya kuokoa muda sitaki kuyasema yote, lakini wamependekeza lakini wao wenyewe wemethibitisha katika ripoti yao Mheshimiwa na ukiniruhusu na ikiwa tayari nitayasoma kwamba; kukubali kuendelea na *structure* iliopo pale ni kuja kukaribisha matatizo siku za mbele. Ni kama utaratibu wa kukosha uso tu *face washing device* lakini utaratibu sahihi ungepaswa kulivunja jengo lile na kulijenga upya. Lakini Mheshimiwa kama hiyo haitoshi hawa hawa DPI wameiandikia barua mamlaka inayohusika tarehe 4 Juni wao wenyewe wakithibitisha katika barua yao kwamba kuna gharama nyingi ambazo tutapata hasara, kuna faida kubwa ambayo tutapata hasara na hili Mheshimiwa naomba uniruhusu nilisome kwa sababu ya uzito wake, wanasema hivi Mheshimiwa. *'As far as non aeronautical revenue are concerned* samahani kwamba *according the calculation detailed in chapter 5.2 of our review report can be updated as follows:*
Cost estimate for option 1(a) or 1(b) zimeelezwa pale kwamba ni kama 114,350,000 US Dollars, lakini katika kujenga hoja yao wanasema, *'a new design of the terminal governed by energy saving consideration could lead to a saving electricity consumption of approximately 460,000 US Dollars per year'*. Maana yake mkikubali jengo hili kila mwaka mtaendelea kuipata hasara hii. *As far as non aeronautical revenue are concerned, the new design proposal option 2a or 2b takes into account not only the regulatory and operation constraints but aims also maximizing the effectiveness of commercial facilities. To give an idea of the financial impact it they have, we propose the following estimation* hao ni *DPI.*

a) *The impovement of commercial attractiveness in terms of available area, number of facilities and level of qualities likely to allow for an increase by 510 US Dollars of average basket amount spent by the departure passengers. As a matter of comparison and average basket in Male; Republic of the Maldive* Mhe. Spika, ushakwenda huko *is around 50 US Dollars and 30 US Dollars at Mauritius International Airport, respectively 2.6 mps and 2.7 mps 2,012 with both a traffic typology very similar to Zanzibar International Airport.*

b) *Will usually consider the operator collect aproximetly 30% of the turnover generated by the shop installed in the terminal. A new design of the terminal with improvement of the commercial attractiveness may lead to an additional*

resource of 30% percent times 7.5 US Dollars times 0.6 mps average number of departing passengers between 2015 - 2020 ambayo itafikia 1,530,000 *dollars a year*, haya ni mapato ambayo tutayakosa ikiwa tutabakisha jengo lile pale. Kwa hivyo hizo gharama zitakazokuja kuwekwa tunaweza kuja kuzirejesha sehemu kubwa kwa faida kwa sababu kutakuwa na mapato haya ya ziada ya kila mwaka.

Conclusion yake Mhe. Mwenyekiti ndogo sana inasema hivi:

We can conclude that a review design for Zanzibar International Airport Terminal II building forcusing on :-

1. The energy efficiency of the building, and;

2. The commercial effectiveness of the terminal is likely to reduce the operating cost by almost 2,000,000 dollars a year. Therefore we anticipate the diversional investment required by family two solution can be rapidly balanced over a period of approximately five years and will significantly increase the airport benefit after the first five years.

Mhe. Mwenyekiti hii inathibitisha kwamba tunataka kuwaokoa Wachina tunataka kuwatia hasara wananchi wa Zanzibar.

Lakini la mwisho kabisa Mheshimiwa wamesema kwamba haya hayakuonekana na ATM, ripoti ya ATM hii hapa Mhe. Mwenyekiti, ya kwanza hii ni ya Septemba 2012, hawa wametoa Mei, 2013 walichopendekeza, ma-*design* hayana tofauti yoyote na ADPI tumeingia hasara bure ADPI hapa. Mheshimiwa jengine ni hili hapa ripoti nyengine hii ni ya tarehe 8 Novemba 2012 mpaka *design* inaonesha hali yote hii. Mhe. Mwenyekiti katika hili kwa kifupi tunakiuka kama ulivyosema, kunusuru mahusiano ambayo kila siku nasema katika Baraza hili kwamba wachina wana *policy* mpya juu ya misaada yao, wanakuja kufanya biashara yale mambo ya zamani ya kugaiwa hayapo tena. Tunagaiwa kidogo tunatiwa hasara kupitia miradi kama hii ya ujenzi ambayo ina *cost* zake, gharama zake zinakuzwa sana huku nchi inaendelea kuangamia, wananchi maskini wa Zanzibar wanaendelea kuangamizwa.

Mhe. Spika, sijaridhika na maelezo nasikitika sana kama walivyosema kama gharama za uwanja wa Durban ule kwamba *per square metre* ni dola 2,300 lakini kwa gharama hizo walizotupa kampuni hii ambayo inapigiwa debe bado na serikali hii ni dola 5,000 kwa *square metre*. Huku si kuwatendea haki wananchi wanyonge wa Zanzibar waliokombolewa na Mapinduzi ya 1964. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka niseme tu Mwakilishi wangu serikali siku zote inawatendea haki wananchi wake, Mhe. Jussa uwe mstahmilivu, wakati wewe unapokuwa unasema sisi tunakusikiliza, wakati na sisi tunaposema nakuomba na wewe utusikilize. Serikali siku zote inakuwa mstahmilivu, inakuwa msikivu, na ndio maana tunakusililizeni Waheshimiwa Wajumbe, nimeeleza kwa ufasaha kabisa. Serikali ililetewa taarifa na kuambiwa kwamba *airport* ina matatizo. Nikaeleza matatizo gani ambayo tuliyoletewa, serikali ikaunda kamati, wala hatulindi maslahi ya kisiasa la kwanza nilieleza hili matatizo jinsi tulivyoweza ku-*hire consultant* mwengine ili aje atushauri na haya yote aliyoeleza Mhe. Jussa huo ndio ushauri wa *consultant* na huyu *consultant* mpya anai-*design* hiyo *airport* ili iweze kukidhi haya aliyoyasema yeye mwenyewe.

Lakini anachokisahau Mhe. Jussa anasoma taarifa vipande vipande, *airport* hii ikifika mwaka 2015 kwa *design* hii ambayo ikiendelea inge-*serve* only 1.1 *passengers* basi. Lakini kwa kui-*redesign* upya kwa huyu ADPI anavyoifanya itafika 1.6 *million passengers*. Kwa hivyo haya anayozungumza Mhe. Jussa anayazungumza anavyotaka yeye na kwa mapenzi yake, lakini ukweli kwamba huyu *consultant* anairidhi zaidi kwa kukidhi haya *efficiency* ya umeme ili *airport* isitumie umeme mwingi, anai-*redesign* kuongeza *commercial attraction*, ili iweze kupata mapato mengi zaidi.

Lakini mwaka jana hapa Mhe. Spika, serikali ilipokuwa inataka kununua meli tulikatana hapa bilioni 17 leo tutakatana kweli 140 *million dollars*, ukilivunja hilo ukijenga jengine jipya 140 *million dollars*, hapo ndipo tutapokuwa tunapoteza pesa za wananchi. Kwa sababu tushawalipa wachina 35 *million dollars*, 35 *million dollars* unataka kulivunja tu.

Mimi namuheshimu sana Mwakilishi wangu Mhe. Jussa na nataka nimwambie kwamba serikali imeangalia yote isitumie vibaya pesa za wananchi na ndio uamuzi huu hii ripoti ya *consultant* tumeifanyia kazi vizuri sana na ADPI hakuwa na mamlaka ya ku-*approve* yeye mchoro, ndipo alipoanza kugombana na BCG, walianza kuvutana na BCG. Na hii BCG sio kampuni ndogo ni kampuni kubwa sana. Nimesema Wawakilishi wengi tumefika Beijing *Terminal II* pale inaposimama Emirates tumeuona uwanja ule wameujenga wao. Uwanja wa mpiraTaifa wameujenga wa Dar es Salaam wameujenga wao kampuni hii. Lakini nakubaliana na Mhe. Jussa kwamba kuna baadhi ya watendaji wetu hawakuwa waangalifu pale jengo hili lilipoanza na ndio Mhe. Rais akachukua hatua akawaondoa tena sio kama kawaondoa kawachomeka pahala kawaondoa kabisa, hivyo ndivyo lilivyo.

Mimi ninamwambia sana Mhe. Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe, kuvunja jengo hili maana yake ndio kuwatia hasara wananchi wa Zanzibar, wakati mshauri ametoa ushauri wake kwamba linaweza likarekebishika. Jamani suruali zetu, nguo zetu zikichanika ndio tutupe hatutii viraka, tunatengeneza mengine yanafanyika. Gari zetu nyengine zinapata ajali hatuzitupi, tunapeleka *garage* zinarekebishwa tunatumia tena.

Nataka nimuombe sana na nimnasihi sana Mheshimiwa kwamba ukweli niliyompa na maelezo niliyompa ndio ukweli sahihi uliojitokeza kwenye *cabinet* na ndio ukweli sahihi uliomo ndani ya ripoti ya ADPI na wala sio maamuzi ya kisiasa. Yale maamuzi ya kisiasa yalikuja baadae tu kuangalia na uhusiano wetu na China. Lakini *cabinet* ilifanya maamuzi ikasema kama, kama mshauri atatoa maelezo kwamba halirekebishiki vunjeni jengo, hata kungekua na maamuzi gani, uhusiano gani wa kisiasa kama ingelikuwa halirekebishiki tungelivunja tu na tukawaambia wananchi kwamba 35 *million dollars* zimeshapotea.

Nataka niseme tu kwamba hatuko karibu na mchina peke yetu, tuko karibu na nchi nyingi sasa hivi, kwa sababu nchi yetu bado ni changa tutaendelea kutafuta misaada na mikopo, na huu ni mkopo nimesema mwanzo huu ni mkopo, lakini ni mkopo nafuu *concessional loan* una riba ya chini ya asilimia mbili. Ni mkopo wa muda mrefu unalipa miaka 20, *gross period* miaka mitano mkopo huu, sio rahisi kila nchi kama itakupa tu *gross period* miaka 5, mkopo miaka 20, *concessional loan*. Tumechukua muda mrefu, Mhe. Hamza ndiye aliyeanza serikali iliyopita walianza kuutafuta mkopo huu muda mrefu umechukuliwa mpaka ukaja ukapatikana mkopo huu, nataka nimuombe na nimnasihi sana Mhe. Jussa bado serikali inajali sana fedha za wananchi, na tutaendelea kujali fedha za wananchi, na ndio maana tumefikia kufanya maamuzi haya, hayakuwa mepesi maamuzi haya. Tumechukua miezi minane mpaka tukafikia hatua hii.

Na huo ndio ukweli Mhe. Spika, jengo litarekebishika na ndio kwa maana nimeizungumzia kwamba hiyo *lobby* inayowekwa alau vile vile kupunguza matumizi ya umeme. Mambo mengi *edit* ya haya yote waliyoyaeleza wao, wao ndio wanaokuja sasa kui-*design* sasa sio mwengine, yeye mwenyewe aliyetupa huu ushauri tumemtaka sasa hivi yeye afanye hiyo kazi na aisimamie yeye. Na mimi nimeeleza Mhe. Mwenyekiti kamati yangu nilitaka ivunjwe tumalize siku ile baada ya ku-*submit report*, niliomba dua kwamba angalau tungeambiwa basi Kamati imefanya kazi nzuri basi. Baraza la Mapinduzi likasema hapana muendelee kuusimamia uwanja mpaka ufikie hatua. Na mimi nipo na nimeiomba sana kamati ya sekta ya Baraza lako tushirikiane katika kusimamia haya mambo.

Namuomba sana Mhe. Mwakilishi wangu, mdogo wangu, rafiki yangu, ndugu yangu tunaweza tukakaa pamoja usiku tukaongea bado hayo mambo. Sisi sote watoto wa Vikokotoni, usiku ndio wakati muafaka wa kuongea na mimi namkaribisha sana Mhe. Jussa usiku baada ya kuftari tuje tukae tuongee. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ingelikuwa tuko katika kibanda cha karata Mtendeni kwa njia ya kahawa tungekutana usiku, lakini hapa kwa haya usiku tunazungumza leo mchana kweupe saa 8.25 katika Baraza la Wawakilishi; Ngome ya Wananchi wa Zanzibar kama alivyoiita Rais wa pili wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti kwa hili mimi leo kama lile la siku ile niko tayari mnitie kitanzi mnitundike hapa niweke historia leo. Mhe. Mwenyekiti nababaishwa tena naendelea kusema tunababaishwa, tena tunababaishwa wananchi wa Zanzibar, serikali hii haina huruma na wananchi wa Zanzibar naendelea kusema Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti *scenario,* huyo anayezungumzwa *redesign* ni suala la kuamua tu wewe unaweza ukapamba hivi ukapamba hivi, lakini msingi ni kwamba lile jengo ili liweze kukidhi haja ya miaka mingi ijayo, lisiwatie hasara wananchi wa Zanzibar ni lazima liondoke pale lilipo. ATM katika ripoti yake hii Mhe. Mwenyekiti *scenario* (c) hii hapa anapendekeza liondoke lirudi nyuma na liongezewe sijui niitaje kama ni mkonga mwengine ili kuongezea uwezo zaidi.

ADPI anachokipendekeza katika *scenario* zake nyingi moja ni hiyo hiyo, kilichokuja hapa ni kuisaidia serikali juu ya mapendekezo waliyokuwa wakiyataka wao na yote inakuja Mhe. Mwenyekiti bado naendelea kuamini kwa sababu ya kutaka kuwanusuru watu ambao wamefanya hasara hii badala ya kubebesha mzigo ili tukatoa funzo, ili wengine wasije wakarejea tunaendelea kutafuta maamuzi ya kuendelea kuwatia hasara wananchi wa Zanzibar ili kuwafichia wengine waendelee kubakia walipo. *Scenario* ya ADPI hii hapa hazina tofauti yoyote ni suala la *design* tu libaki vipi. Lakini msingi wake kwamba pale lilipo kwa sababu tungekuwa tunafanya kazi ya kitaalamu Mheshimiwa tungeelimishana humu.

Pana suala kwamba pale lilipo kwa ndege kubwa zikikaa wakati wa kutua kuna taratibu za kimataifa zinaongoza utuaji wa ndege kuna eneo fulani hawatakiwi liingiliwe na chochote, ukiweka ndege kubwa pale kwenye mkia wa ndege zitakuwa zinaingiliana na eneo lile yameelezwa yote humu Mhe. Mwenyekiti. Imezungumza hapa sijui dola milioni ngapi tusiwatishe wananchi. Mhe. Mwenyekiti hapa imezungumzwa katika ile barua niliyokuwa nikiisoma kwamba the *conclusion of this review cost analysis is the family II solution, family II solution* Mhe. Mwenyekiti ndio ya kuvunjwa kuonesha

nyuma. *Terminal reallocated I approximately* 7 to 11 *percent more exspensive than family I solution.* Sio kama picha inayochorwa hapa Mhe. Mwenyekiti . *Terminal Current location* inaambiwa ndio hiyo iliyobakia sasa hivi. *In other words; we estimate that family II solution required investment of nine to 13 million US dollars higher than family I solution.*

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti kinachozungumzwa ni ongezeko la baina ya milioni 9 dola mpaka milioni 13 kwa hasara ambayo tutaingia, hata hii si kwa sababu maamuzi mabaya, kwa sababu kuna watu wametaka wenyewe na wakasema hizi zinaweza kurejeshwa ndani ya miaka 5 kwa sababu kutakuwa na *facility* nyingi ambazo zitaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema tusiyachukulie mambo madogo madogo mbona ulitutahadharisha kwamba tusiingie katika maamuzi ya kitendaji, na ingelikua kila mmoja anafanya mamlaka yake yasingefaa sisi kuja kuyazungumza hapa haya, lakini watu hawafanyi wajibu wao Mhe. Mwenyekiti. Watu kila pahala wanaingiza maslahi yao juu ya migongo ya wananchi maskini wanyonge wa Zanzibar, Mhe. Mwenyekiti leo tunataka kulifunika. Lakini mimi nasema hivyo kama tunasema tukilivunja tungekula hasara yote, hasara hiyo anaibeba nani? Ikiwa kuna watendaji wetu ambao walituingiza kwenye hasara ile wakamatwe wao na mali zao zifilisiwe warejeshe gharama ile. Lakini mimi naamini katika hili na kampuni yenyewe inajua ya kichina hiyo Beijing Construction inajua hilo, na Mhe. Mwenyekiti si mara ya mwanzo unakumbuka tuliwahi kushinda kesi kimataifa sisi hapa katika kutuharibia gati yetu, kwa hivyo kushinda kesi kwa mtu kavuruga mkataba ikiwa kaharibu taratibu uwezekano huo upo na imeshawahi kutokea hapa Zanzibar.

Sasa kama Mchina kampuni yake hii ya Beijing Construction imefanya matatizo, isije kuwa inataka kukosha uso wake kwa sababu likivunjwa leo na katika maelezo yao wameandika Mhe. Mwenyekiti, walishtuka kama yameandikwa kwenye magazeti nje, kwa hivyo wao ndio wa kukosha uso wao kwamba wasionekane katika dunia wana kampuni yao imefanya vurugu Zanzibar, kwa hivyo imeharibu inahofia isije ikakosa kazi sehemu nyengine, wao wananusuru uso wao sisi wetu tunaupaka masinzi, tunaupaka uchafu tunajipeleka mbele Mhe.Mwenyekiti, hilo si sahihi.

Kama nilivyosema suala hili ni zito Serikali ishike *position*, la si hivyo tukubaliane kwamba mradi huu iundwe Kamati Teule ikauchunguze wote, wote Mhe. Mwenyekiti, mwanzo mpaka mwisho. Kwa sababu tukisema tunaenda kufanya katika kamati ya kisekta, kamati ya kisekta tunajua inavyofanya kazi na wote wenzangu wanajua ina matatizo matupu, unatakiwa uichunguze Wizara nzima ndani ya kipindi cha wiki mbili.

Mhe. Mwenyekiti, hili linahitaji kazi ya ziada ya kwenda kuyafichua na kuwafichua waliowaingiza wananchi wa Zanzibar katika hasara ya mamilioni, wao wakakaa juu huko wanatikisa miguu wanatuacha sisi tukipiga makelele tu humu, kila mradi unaokuja mtu anataka kutia chake mfukoni, tunataka kuikomesha tabia hii. Mhe.Mwenyekiti, naomba ije Serikali ituambie itachukua hatua gani dhidi ya aliyoitia hasara hii ichukuwe hatua ya kuwaambia kampuni wenyewe walihusika, wachina warejeshe nyuma kwa gharama zao, zile za ziada za kuongeza jengo ndio zibebwe na wananchi wa Zanzibar, na kama si hivyo Serikali hairidhiki tukubaliane tutoe hoja tuunde Kamati tukauchunguze mradi ule.

Mhe. Spika: Labda kabla sijamuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Maendeleo labda ningesema jambo moja. Unajua kuna baadhi ya masuala ni ya kitaalamu sana moja ni hili. Na ndio maana ikawa Serikali imekubali kutafuta washauri waelekezi kwa sababu ya utaalamu walionao kwa kiasi wanavyoaminika kimataifa, na kwa kazi ambazo wameshawahi kuzifanya. Sasa kwa jambo ambalo ni la kitaalamu ya hali ya juu, kuja kuiunda Kamati Teule hapa kidogo hili jambo mimi napata wasi wasi, napata wasi wasi tunaweza tukachukua muda mkubwa sana lakini wala tusipate matunda yake.

Kitu ambacho nilitaka nijiulize lakini bahati nzuri Mhe. Waziri alijibu mapema ni kwamba je, hizi hoja anazosema Mhe. Jussa, Serikali ilipata na kuzingatia mpaka wakafikia maamuzi kwamba tuendelee katika utaratibu ambao Mhe.Waziri ameusema, bahati nzuri Mhe. Waziri alisema yote hayo yamezingatiwa na ndio maana ikawa haja ya ku-*redesign* kufuatana na yaliyotolewa na washauri waelekezi mbali mbali. Sasa sishawishiki juu ya hoja ya kwamba tuteue Kamati Teule, hiyo sishawishiki kwa sababu ni suala la kitaalamu sana na wala ilikuwa sipendelei kwamba jambo hili tupige kura, nilitaka tuelewane tufike pahala Serikali iwe inafanya kazi, kama kuzingatia zaidi izingatie lakini tusipige kura.

Upigaji wa kura una hatari zake wa kuja kufikia maamuzi ambayo pengine yanaweza kuwa na hasara nyengine, kwa sababu nadhani mikataba imeshatiwa saini, sasa kuja kupiga kura juu ya jambo ambalo mikataba imeshatiwa saini kuna hatari ya Serikali kuja kufikishwa Mahakamani na ikawa masuala mengine. Mhe. Waziri, hebu tusaidie maelezo zaidi ili tufike pahala tumalize hili jambo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, huko nje huko kuna ndugu zetu wanasema da! Mhe. Omar na Mhe. Jussa wanafahamiana sana na marafiki sana. Mimi ninawaambia

siku zote kwamba yule ni Mwakilishi wangu ndani ya Jimbo la Mji Mkongwe, na haya ambayo tuliyonayo leo hapa, hayatatufanya mimi na yeye urafiki wetu kuvunjika, anatushitua Serikali na mimi nashituka, lakini ninaposhituka na mimi kumbe najibu na yeye akubali majibu ninayompa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jussa, ameng'ang'ana na *option C,* hebu tumuulizeni A na B ziko wapi na zinasema nini? Kang'ang'ana hapa *option C* katoa maelezo makali sana. Mhe. Jussa, mimi nafurahi uking'ang'ana kweli, lakini kumbe kuna mengine unakuwa unatuficha na wewe hapa, *option C* kaing'ang'ania sana A na B hazitaji zinahusiana na nini. *option A, option B* na *option C* maana yake nini, maana yake mshauri amekupeni nyinyi uamuzi wa kuangalia hali zenu kifedha, kimuda, kiuhusiano angalieni zote *option A* na *option B* hazisemi kuvunja jengo, linasema kufanya ukarabati na kufanya *adjustment* kwa mujibu wa ndege zikalie vipi tena zile ndege kubwa, *option C* anakwambia mnaweza mkalivunja, ndio option c aliyoing'ang'ania Mhe. Jussa tu hiyo A haitaki, B haitaki. Sasa huyu Mwakilishi wangu nampenda sana na nitaendelea kumpenda, lakini nataka awaambie na *option* A na *option* B zinasema nini, mimi nawaambia hazisemi kuvunja, *option A* haisemi kuvunja na *option* B zinasema jinsi ya kuzifanyia marekebisho na zinasema gharama zake zitakuwa kiasi gani.

Mhe.Mwenyekiti, ukilivunja hili jengo na ukajenga upya gharama zake dola milioni 140, ukilifanyia marekebisho ni milioni 115, sasa mimi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar niliyopewa dhamana ya Waziri wa Fedha nitakuwa mpumbavu nikisema livunjwe, nitakuwa mpumbavu sana. Na haya yote niliyapeleka Serikalini kama ulivyoniuliza Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii yote niliipeleka Serikalini, na Serikali wakauliza masuali Mawaziri kama wanavyouliza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, mimi na Kamati yangu tumenyamaza kimya, Serikali wakatoa uamuzi kutuelekeza Kamati. Sasa haya kwamba wanataka kukosha uso BCG mimi siyajui, kama kuna watu wamekula kwenye mradi huu mwanzo sijui, nasema pale nilipokabidhiwa mimi kama ni Mwenyekiti wa Kamati na hadidu rejea zangu zilikuwa ni kutafuta njia itakayotatua matatizo haya matatu.

Mhe. Mwenyekiti, bado namuomba sana Mhe. Mwakilishi wangu nafasi ya kurekebisha jengo lile ipo, Serikali imeshatia saini kuendelea na mkopo wa ziada ili lile jengo liweze kurekebishwa, tumeshaomba *extension* ya mkopo kwa muda wa miezi kumi na nane tena, tunatarajia jengo lile litamalizika Disemba mwaka 2014, mwaka huo tukabidhiwe jengo, Mungu akituweka uhai na uzima Sherehe za Mapinduzi ya 2015 jengo lianze kutumika. Hayo yote Serikali imeshakamilisha kwa kuzingatia haja halisi hasa. Na mimi Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema sioni sababu ya kwamba kuwe na Kamati Teule, hiyo Kamati Teule itakuja kutumia zaidi ya hizi fedha tunazotumia

sasa hivi. Kamati Teule haina utaalamu, sisi ndio tume-*hire* mtaalamu wa kutupa hizo taarifa Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimwambie tu Mhe. Mwakilishi wangu wa Mji Mkongwe kwamba pale ambapo tuna nafasi ya kurekebisha itarekebisha Serikali, na aturuhusu tufanye hivyo turekebishe na kurekebisha siku zote sio kuvunja Mhe. Mwenyekiti, hata katika dini zetu za kiislamu tunaambiwa unapokuwa una ugomvi na mwenzio ndani ya nyumba sio kumpa talaka, ni kukaa mkazungumza mkaona jinsi gani mtarekebisha matatizo yenu. Bado namuomba sana Mwakilishi wangu tuendelee kuwa marafiki mimi na yeye, lakini tuendelee kupeana yale yaliyomo ndani ya mradi huu. Hayo yote ambayo umeyasoma mimi ninayo yote hayo, na ndio kwa maana nikasema mwanzo nilipopewa kazi hii ya kuwa Mwenyekiti wa Uwanja wa Ndege wakati huo huo nilikuwa na kazi nyengine ya Uenyekiti wa Meli, nikasema hapa kweli kazi juu ya kazi. Lakini nashukuru zote zimekwenda vizuri, nashukuru mpaka sasa hivi sina matatizo nazo, Serikali imefurahi kwa kazi tuliyoifanya na vile vile tunashirikiana na Mhe. Waziri wa Miundombinu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mimi Mhe. Mwenyekiti, nina sentensi moja tu nikitaka kuongeza pale alipomalizia Mhe. Omar. Iko jumla moja haikusomwa na Mhe. Jussa, kwa hivyo naomba niitoe. Katika ripoti ya ADPI ukilivunja jengo kuna tofauti ya miezi 12 kamili kuweza kupata jengo jengine na ukilinganisha na kulijenga hili kidogo, hiyo iko sentensi hiyo ndani ya ripoti ile, kwa hivyo sisi tuli-*consider* yote hayo, hatukwenda kwa maamuzi raghba wala chochote, lakini kama ingekuwa imefuatwa hiyo *option* ya kuvunja jengo, basi huo muda aliosema Mhe. Omar wa Disemba 2014 ingekuwa Disemba sasa 2015 kwa ripoti ya muwekezaji ADPI alivyotoa, ni hilo tu mimi nilitaka kusema.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii nimshukuru na kumpongeza sana Waziri wa Nchi Fedha pamoja na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa maelezo yao mazuri. Aidha nimshukuru ndugu yangu na mimi rafiki yangu Mhe. Jussa kwa hoja yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niunge mkono maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi Fedha, pale aliposema kwamba katika jambo ambalo Serikali hii ya awamu ya saba imelifanyia kazi sana, moja ni suala hili la ujenzi wa *Airport*, ni jambo ambalo limechukua muda mrefu sana, ni jambo ambalo lilizungumzwa mara nyingi sana ndani ya Baraza la Mapinduzi. Nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa, Serikali katika mchakato huu inaelewa kwamba kwa njia moja ama nyengine basi imeongezeka gharama kwa sababu ya baadhi ya watendaji ambao hawakufanya wajibu wao vizuri. Mimi nataka

nimuhakikishie kabisa kabisa kwamba Serikali na hilo inalifanyia kazi licha ya hatua ilizozichukua katika kurekebisha uongozi katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano lakini pia Serikali itaendelea kuchukua hatua kwa wale watendaji ambao walitia hasara, walifanya ubadhirifu katika mchakato mzima wa suala la ujenzi wa *Airport* ile, wala hatutokaa kimya, taratibu zinakwenda za kiufumbuzi ili wale wote watakaohusika kuingiza hasara basi hatua zitachukuliwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, Serikali hii ilipoingia madarakani, na kwa sababu ya umuhimu wa *Airport* na hamu yetu ya kutaka *Airport* ifanye kazi hasa ukiangalia maslahi ya uchumi wetu sana tunategemea sekta ya utalii, na sekta ya utalii kwa kiasi kikubwa inategemea *Airport* basi tumefanya kazi kubwa ya kutafuta njia mbali mbali, na haya anayosema Mhe. Jussa ya kulivunja na kujenga pengine pia hoja hizo ilikuwa *raised* katika Baraza la Mapinduzi, lakini bada ya majadiliano marefu na kuona hali zetu za kiuchumi na kujua kwamba suala tukivunja itachukua muda kupata fedha nyengine katika kuendeleza ujenzi huu, ndio maana tukaja na *option* hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Jussa aelewe kwamba hakuna hata mmoja aliyependelea tupate hasara hii, lakini tulikuwa tumekuta hili tatizo, tukawa hatuna *option* nyengine lazima tulitafutie dawa. Na mimi nataka sana sana hapa Waziri wa Nchi Fedha ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ile, wamefanya kazi nzuri sana yeye na wenzake katika kutafuta njia; na ndio maana tulikaa muda mrefu kuzuia ujenzi ule kwa sababu tukingojea ushauri wa kitaalamu ambao ama ingetuwezesha kuvunja ama ingewezesha kuendelea na shughuli hiyo, lakini pale tulipopata ushauri ambao umeonesha wazi kwamba unaweza kuendelea na mradi huu bila ya kuvunja ndio maana tukafikia hatua hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali ya China bado ni rafiki zetu wa kweli na sio sisi tu Tanzania na Zanzibar wenye mahusiano makubwa na Serikali ya China, nchi nyingi leo ulimwenguni wana mahusiano makubwa na Serikali ya China na inafanya mengi kwetu na ni ndugu zetu madhubuti wa enzi. Kwa hivyo kosa ambalo limefanywa ama na kampuni ya kichina au na mchina isishirikishwe na Serikali ya China, kwa sababu Serikali ya China ni Serikali nzuri, Serikali makini, ina uongozi mahiri ambao una imani kubwa na nchi yetu. Yapo makosa yaliyofanywa na wajenzi, hayo tumewa-*task* watendaji pale ambapo ipo hasara iliyosababishwa na wajenzi basi nao hiyo waioneshe, na katika kufanya vyovyote vile na wajenzi nao wagharimike kutokana na hasara zinazojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo hili jambo Waheshimiwa Wajumbe limezungumzwa sana na limezungumzwa kwa nia kwamba Serikali ina imani na wananchi

wake, Serikali ina huruma na wananchi wake, na Serikali inapenda ifanye mazuri kwa wananchi wake kwa maslahi yetu sote. Na yoyote yule mwenye nia yoyote mbaya basi Serikali haitomvumilia na itachukua hatua za kufaa. Hivyo naomba tu kumuomba sana Mhe. Jussa na wenzetu Wawakilishi wengine kwamba maamuzi tuliyoyafanya hatukuyafanya kwa sababu ya maslahi ya kisiasa, wala hatukuyafanya kwa sababu maslahi ya mtu, lakini tuliyafanya kwa sababu ya maslahi ya Wazanzibari wote na kwa sababu ya umma wote ili tupate ufumbuzi muafaka utakaosaidia maendeleo ya nchi yetu, na tunaamini kwamba *Airport* ni chanzo kikuu cha uchumi wa nchi yetu.

Mhe.Mwenyekiti, sasa naomba nimuombe tu Mhe. Jussa, haya yote aliyoyasema sisi tutayachukua tukayafanyie kazi zaidi, na pale popote pale tutakapogundua yuko mtendaji ama kiongozi anashiriki kwa njia moja ama nyengine katika kuitia hasara Serikali au katika kufanya ubadhirifu wowote nataka nilihakikishie Baraza hili tukufu kwamba Mhe. Mwenyekiti, hatua zitachukuliwa kwa kila hali, kwa sababu sote linatuuma jambo hili. Tungependa leo tuwe tumeshakuwa na *Airport* yetu inafanya kazi ndio kwa mujibu wa *plan* iwe hivyo. Lakini bahati mbaya mambo tumeyakuta, yamekosewa na huwezi kuacha makosa unafanya marekebisho. Kwa hivyo ninachoomba Waheshimiwa watuunge mkono na waiamini Serikali yao; kwamba italifanyia kazi jambo hili na wahusika wote watachukuliwa hatua wale waliofanya ubadhirifu na yote tunayafanya kwa maslahi yetu ya kuhurumia wananchi kwa pamoja.

Mhe. Spika: Mhe. Jussa nakuomba radhi. Waheshimiwa Wajumbe suala hili limeshachukua muda mkubwa sana kimsingi hoja ya kupitisha fungu hili tumeanza kazi tangu asubuhi ya leo na muda wetu wa kawaida umemalizika, kwa hiyo ninaelekeza nitamuomba Katibu hapa aturejeshe Barazani ili nipate kusema maneno halafu tumalize hii kazi.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Spika: Najua kuna baadhi ya mambo kama hukujisifu mwenyewe ukangoja usifiwe basi unaweza ukaumia bado hujasifiwa. Ninachotaka kusema kwamba kama kuna chombo cha kutunga sheria ambacho kina demokrasia kubwa kimoja ni cha kwetu. Nasema hivyo kwa sababu gani, tunatumia muda mkubwa sana katika kumsikiliza Mhe. Mjumbe kwa makini na kuwataka Mawaziri watoe majibu; hiyo ndio demokrasia yenyewe. Na madhumuni ni nini? Madhumuni ni kwamba tufikie pahala ili mambo yetu yaende kwa ufanisi kwa faida ya wananchi wetu sote upande wa Serikali na upande wa *backbenchers*, madhumuni ndio hayo hayo.

Jambo hili ambalo tumekuwa nalo tokea asubuhi kushughulikia fungu 26 limechukua muda mkubwa sana na hasa hasa hili suala la Uwanja wa ndege; suala kubwa, suala muhimu ambalo ni uwekezaji ambao tunategemea kwamba nchi yetu ipate mapato makubwa na kwa jinsi ya muda mrefu iliyochukua yule mwekezaji yuko pale bila shaka ilikuwa ni kuona kwamba uamuzi wa kufikia sasa kuendelea na jambo uwe umezingatiwa kwa makini sana, tumesikia maelezo wakati wa majumuisho kutoka kwa Waziri, lakini maelezo marefu sana kutoka kwa Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo, lakini tumefikia hatua ya kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu, hii inatuthibitisha kwamba Serikali imezingatia kwa makini sana suala hili, hilo lazima tuamini, ndio maana ime-*engage* kampuni mbali mbali na washauri elekezi, kutaka kufikia pahala tuwe na kitu ambacho kitakuwa kina faida kwa nchi yetu na wananchi wetu.

Sasa inapofika pahala imeshachukua muda mkubwa. Kwanza niseme kwamba hoja hii ambayo tumeizingatia kwa kipindi kirefu zaidi hii ya Uwanja wa ndege, tufike pahala kwamba *commitment* na *seriousness* ya Serikali mimi kama kiongozi wa chombo hichi kwa kweli nimeridhika; kwamba Serikali imefanya kazi kubwa maana ukweli tuueleze, tumefanya kazi kubwa. Kwa hiyo nilitaka jambo hili tufikie pahala iwe tumemaliza kazi. Nataka tukubaliane kwa kumuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tuongeze muda, lakini hii kazi tuimalize leo tena wala sio muda mrefu. Najua wakati mwengine kuna baadhi ya mambo inakuwa na hasa taratibu zetu, hivi ni vitu ambavyo vina uhai, unapopungukiwa inakuwa wakati mwengine unakopa, unakopa ili uweze kuendesha mambo yako, na mimi sasa hapa nataka nikope, niwakope nyinyi Wajumbe kwanza ili mkubali kutuongezea muda ndio mkopo wa kwanza huo, lakini mkopo wa pili tutumie kama wenzetu wanachofanya, wanatumia wakati muafaka inapobidi ili kumaliza kazi iliyokusudiwa, sasa basi na sisi inapofika pahala mshaelezana mengi basi tuongeze muda fulani tumalize hii kazi ili tuje tuendelee na shughuli nyengine.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa maana hiyo nataka nitumie mkopo huo kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa muendeshaji wa Kiti hichi chini ya fungu 158, kukopa utaratibu ambao hatimaye huko mbele tutapozingatia kanuni tutaweka rasmi katika kanuni hii. Utaratibu wa kuongeza muda kiasi tutaona tunaweza tukamaliza shughuli hii, na mimi nadhani haitakuwa vyema kufika hapa mpaka laasiri tukaanza kudondoka dondoka mpaka *quorum* ikawa haikutimia kabla hatujamaliza kazi hii. Kwa hiyo tutumie dakika 45 ili tutumie wakati muafaka tumalize kazi hii tupate kwenda kupumzika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu, na kwa kuwa Mhe. Spika, umetoa muongozo mzuri wa kusaidia kumaliza jambo hili kwa wakati muafaka ili Waheshimiwa Wajumbe wapate nafasi wale watakaokwenda kusali laasiri wawahi kusali laasiri kabla ya muda wa laasiri kufika, na kwa kuwa mambo mengi yamezungumzwa kwa kina yale makubwa sana, kwa hivyo naomba Mhe. Spika, Baraza lako liridhie tena kuongeza muda wa kumalizia shughuli hizi kuanzia sasa tuongeze tena kwa dakika 45 ili shughuli hizi ziweze kumalizika kabla ya saa kumi kasoro, na ikiwezekana tumalize mapema zaidi ili tuwahi msikitini. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kutoa hoja ili tuongeze tena dakika 45 tumalize shughuli iliyo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Haya rudisha Kamati ya Matumizi halafu tuendelee na Mhe. Asha Bakari Makame.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nitayoyaeleza yanawiana na Mhe. Ismail Jussa Ladhu nikuombe sana japo kidogo tu. Mimi kwanza niishukuru sana Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa wako hawa wa *backbencher* maana yake mimi nasema kama mtu mzima sasa hivi. Wasionekane kama maana yake alivyotwambia Mhe. Mwanasheria Mkuu ametusaidia sana leo Mhe. Mwanasheria Mkuu na katupa moyo. Sasa na mimi niwaombe *backbencher* wenzangu Serikali na chombo hiki kiwe baba mmoja na mama mmoja. Lakini *backbencher* ni kwamba wanaona yale ambayo yanatolewa na *backbencher* Serikali haichukui hatua.

Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, nisamehe kidogo kwa sababu tunataka kutengeneza hii leo inaonesha *backbencher* kama inaweza na sisi hatutaki tufikie huko Mhe. Mwenyekiti. Mihimili hii mitatu lazima ishikane hata mmoja usitetereke. Sasa kwa utu uzima wangu wa Baraza hili nawaomba wenzangu *backbencher* kwa hili tuipe fursa Serikali kwa nia safi kabisa, nakuombeni sana kwa nia safi kabisa mimi sikufichi Mhe. Mwenyekiti,

ilikuwa isipitishwe wizara hii mimi nakwambia kweli, lakini naiomba Serikali ituoneshe mifano bora.

(1) Ndio nikasema linagusana na Mhe. Ismail Jussa Serikali ilipotoa *stop order* iliona kwamba kuna kasoro na kasoro hizo zimetupotezea muda, kasoro hizi zimeongeza gharama.

Maana yake nasema ile ukweli. Lakini sasa tunajiuliza hawa waliofanya haya ni hatua gani ambayo Serikali itachukua. Gharama si ndogo Mhe. Mwenyekiti, sitaki nirudie nyuma. Lakini naiomba Serikali na nawaomba wenzangu *backbencher* Serikali ichukue hatua kwa wale ambao wametia kasoro na dosari kuwa mpaka leo *terminal 11* inayumba.Ikifanya hivyo Serikali hatuna matatizo Mhe. Mwenyekiti, maana kamati nyingi Mhe. Mwenyekiti zimeundwa; ni nyingi tu mno Kamati Teule. Sasa hawa wenzangu tunaogopa maana pamoja na mimi kwa sababu na mimi nilikuwa katika Kamati Teule naogopa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, niwaombe, mtoto wangu Mhe. Ismail Jussa nakuomba sana mwanangu ambaye miongoni niliokufundisha kazi ni mimi. Nakuomba na namuomba mwanangu Mhe. Omar Ali Shehe nikubalieni hili kama mtu mzima wenu. Tuisamehe leo Serikali lakini haya niliyoyaeleza yafanyiwe kazi. Nimesahau kumtaja Mhe. Hija Hassan Hija maana sisi tumekwisha lakini watoto kama hawa ndio damu inawachemka. Lakini pia nisimsahau na Mnadhimu wangu Mkuu tukubaliane sisi tutumie utu uzima, niseme tu kwamba baada ya kusema hayo kwa sababu Serikali leo imetueleza mambo mengi na wamekiri kama kuna makosa ndani yake. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na mengi lakini utu uzima umenijia na niwaombe wenzangu tukubaliane ili tuipitishe Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, nasema tuiachieni.

Tutizame hiki kipindi ambacho tumeelezwa na Serikali ili baadae tukae pamoja tukubaliane. Baada ya kusema hayo mimi niseme naanza kuunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Bakari tunakushukuru. Lakini umeeleza suala moja na inafaa Serikali itoe majibu kidogo, hatua zitakazochukuliwa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimkumbushe tu Mhe. Asha Bakari Makame kwamba nilipopelekwa mimi pale pamoja na haya yote wanayoyazungumza Serikali ilichukua hatua ya kumuondosha Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mkurugenzi Mipango na Sera kwa wakati mmoja ambazo si hatua ya kawaida

kwa Serikali, na hiyo namuhakikishia imenisaidia sana katika kuendesha shughuli.

Kwa hivyo, naamini mimi kwamba limewezekana kubwa lile basi naamini hatua nyengine za wadogo wadogo maafisa wengine wa kawaida inaweza kuchukua hatua mara moja. Kwa hivyo, namuhakikishia mimi nikishirikiana na Serikali Kuu kupitia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tutamshauri vilivyo ili wale ambao hawaitendei uzuri waweze kutizamwa katika jicho jengine. Hiyo namuhakikishia Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Haya maelezo ya ziada Mheshimiwa Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Baada ya maelezo mazuri ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, na baada pia ya maelezo ya mama angu Mhe. Asha Bakari Makame; mpezi wangu, na ajue kuwa bado wamo, bado hajazeeka.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeshaanza kuchukua hatua na hivi sasa vyombo husika vimepewa kazi hii ya kuchunguza wale wote ambao watahusika kwa njia moja au nyengine basi mkondo wa sheria utachukua nafasi yake. Hatutomvumilia yoyote yule ambaye atasababisha hasara kwa nchi yetu ama ubadhirifu wa aina yoyote, na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi tunasema hapa kutokana na hoja mbali mbali zinazojadiliwa na Waheshimiwa Wajumbe ndani ya Serikali tunachukua hatua za kujipanga.

Hata kuanzisha hii taasisi ya kuzuia rushwa msingi wake ni huo, na wao pia wanayo kazi wataifanya kuhusu jambo hili na vitu vyengine. Ili kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwamishwa na hayatokei kwa nia ya kuhakikisha kuwa maisha ya wananchi wa Zanzibar yanakuwa mazuri zaidi na maendeleo yanapiga hatua kwa hatua.

Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa tu kwamba hatua zitachukuliwa na wahusika wote watakwenda katika mkondo wa sheria. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Haya sasa tuendelee.

Kifungu 0401-	Idara ya Mipango na Sera	288,000,000

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, *page* 318 kifungu 0701 Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.

Mhe. Mwenyekiti, ni mara yangu ya kwanza hii kuingia Baraza la Wawakilishi kupiga buti. Lakini nimepiga buti kwa sababu hili naamini ni

Baraza Tukufu Baraza ambalo linaheshimika kwa wananchi wa Unguja na Pemba, na sisi tuliomo ndani humu tumechaguliwa na mimi mmoja wapo nimechaguliwa na wananchi wa jimbo la Uzini.

Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa swahiba wangu, mwenzangu Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano katika majibu yake kwa niaba ya waziri alisema kwamba sikuwa na mkataba wa masuala haya ambayo nilikuwa nimeyazungmza, na vile vile amenambia nirejee kwa Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, namuheshimu sana Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, na hatua ya kufika hapa Baraza la Wawakilishi yeye amenisaidia sana, kwa sababu yeye alikuwa mfuatiliaji mzuri, kwa kuenda Shaaban Robert kwa kuhakikisha kwamba mimi nimemaliza kidato cha 12, alifika kwenye Ubalozi wa Canada kuthibitisha kwamba mimi si raia wa Canada. Kwa hivyo, mimi nashukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamedraza Hassanali twende kwenye hoja kwa sababu muda wetu umebaki dakika 30.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, mimi si muongo wala si tapeli wala si mnafiki, nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi, lakini ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri si uzuri kumwambia muongo, lakini hakuwa mkweli na hili kalichemsha! Kasema uongo!
Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamedraza Hassanali, pale uliposema kwamba labda maelezo hayakuwa ya kweli ilitosha, na kuingia kusema muongo sasa hiyo kidogo si lugha nzuri kwa Baraza.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, makubaliano haya yalifanyika chini ya Wizara ya Miundombinu barua hii ambayo Katibu Mkuu aliyenitaka nilipe milioni ishirini kwa niaba ya Jimbo la wananchi wa Uzini, na barabara hizi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara ya Mindombinu na Mawasiliano gharama zake zilikuwa milioni 87 na barabara zenyewe zilikuwa Pagali-Umbuji, Ndagaa-Ndondongwe, Kwakipawa-Matora, Ndondongwe-Mkuku, na nimetakiwa na Katibu Mkuu tarehe 5/03/2012 nilipe milioni 20 kwa makubaliano na nikaenda Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano nikapewa risiti zake.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja yako.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, sikutendewa haki na nimeambiwa kuwa sikuwa mkweli. Sasa ninachotaka mimi hapa kwa sababu uthibitisho wote ninao hata Mhe. Waziri

wa Miundombinu tarehe 17 mwezi Januari, 2013 nilizungumza suala hili mbele ya Rais wa Zanzibar kwenye mkutano wa *Zanzibar Partnership* ya Wafanyabiashara na akakiri. Lakini yote Mhe. Mwenyekiti, Naibu Waziri mwenyewe alikiri kwa *cassette* yake ya DVD walipofanya mkutano wa hadhara Umbuji akakiri hii hapa *cassette* kwamba kulikuwa na makubaliano kati ya Mwakilishi wa Jimbo la Uzini na Wizara ya Miundombinu kwamba nilipe shilingi 20 milioni, kilichobakia watalipa wizara na kama anasema hii picha si yake naweza kuwaleta wananchi wa Uzini wote walioshuhudia kwenye mkutano wa hadhara wakaja wakathibitisha.

Ninachoomba mimi Mhe. Mwenyekiti, lazima tuwe wakweli hili Baraza lina heshima, tumekuja hapa kwa maslahi ya wananchi wa Unguja na Pemba. Nataka Mhe. Waziri anipe kauli ya kusema barabara hii lini itatengenezwa na muda gani, hilo ndilo ninalolitaka, kwa sababu nina makubaliano yote na Mhe. Rais barua hizi zote zimemfika, serikali nzima inayo makubaliano haya.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kuna tofauti baina ya barua na mkataba, Mhe. Raza alivyojibiwa ni kwamba kweli alichangia shilingi 20 milioni za utengenezaji wa barabara zilizomo katika jimbo lake, na matokeo yake kazi ilifanyika mashine iliharibika na hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, tunavyozungumza bado imo msituni katikati ya njia hiyo ambayo imetengenezewa hiyo barabara mpaka leo haijatengenezwa hiyo mashine, kwa sababu iliungua moto hasa jambo ambalo si la kawaida. Sasa alichojibiwa ni kwamba sisi *commitment* yetu ule wajibu wetu ilikuwa ni kusaidia katika mchango wake, leo gharama aliyotoa haina maana kwamba ni mkataba wa kumfanyia kazi zote.

Hata hivyo, wizara kupitia Idara ya *UUB* haijakataa kutengeneza hiyo sehemu lakini sasa itatengeneza kwa mashine gani na mashine imeharibika imo ndani ya msitu na inahitaji zaidi ya shilingi 16 milioni sasa hivi. Kwa hivyo, sisi tunachosema si kwamba kaambiwa hakutoa pesa, zinathibitishwa pesa za kuchangia ametoa shilingi 20 milioni na mimi alipokuja kuzungumza nikaiagiza risiti nikaipata na nikamhakikishia kwamba risiti ipo na mimi nimeiona, lakini kinachozungumzwa ule ni utaratibu wa kuchangia sio utaratibu wa kwamba ni mkataba kuwa unafunga na kuwa lazima itimizwe ile kazi yake. Kwa sababu kazi yenyewe ikiwa inahitaji shilingi 86 milioni nyengine zitoke wapi, sasa ile *contribution* yake ilipokewa ili kusaidia mafuta, lakini bahati mbaya mashine ambayo ilikuwa ikifanya kazi imeharibika na yeye anaijua ilipo ndani ya msitu imo.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini nia ya serikali kusaidia bado ipo?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nia ipo na kaambiwa hivyo.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, nasema namheshimu sana Waziri wangu na baba yangu, kuna mambo yameniridhisha hapo, kwamba hii risiti haikuwa sadaka, haya yalikuwa makubaliano yametajwa hizo sehemu nilizokuwa nimezifanya. Sasa mimi katika kumsaidia kwa sababu naipenda hii nchi yangu, naona uchungu na nchi yangu, kuna mambo mawili kasema wanaweza kumaliza hili jambo, lakini wanasema Wizara ya Miundombinu serikali wana mapungufu ya shilingi 16 milioni, kwa kumfahamu yeye ili kuweza kukamilisha hili jambo na wanasema wanayo ahadi na watalitekeleza. Je, Mhe. Waziri hizo shilingi 16 milioni nimletee kesho akaifanye hiyo kazi kwa niaba ya wanachi wa Jimbo la Uzini, akiniruhusu kesho nitamletea mimi Jumapili. Kwa sababu Rais keshatoa kauli na yeye.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kama nimemsikia vizuri Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano hakusema kwamba wizara yake ina upungufu wa shilingi 16 milioni, amesema kwamba kutengeneza hiyo mashine inahitajia shilingi 16 milioni. Na mimi nimemfahamu kwa nini hakuweza kuitengeneza hiyo mashine, kwa sababu hatujampitishia bajeti. Mimi naliomba sana Baraza hili tumpitishie hiyo bajeti ili aweze kuitengeneza hiyo mashine ili aweze kufanya kazi kama vile ambavyo wameombwa na Mhe. Raza, huo ndio utaratibu wa kiserikali. Kwamba shilingi 16 milioni wanazo ndani ya vifungu vyao tuwapitishie hii bajeti watengeneze hiyo mashine halafu waweze kufanya hizo kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Raza nikuombe sasa tukubaliane na hii kauli.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii ilikuwa mwaka jana na suala hili lilikuwa mwaka jana sio mwaka huu, sasa mimi nipewe hiyo ahadi tu kwamba lini litakwenda kutengenezwa hilo jambo ili na mimi niridhike na bajeti hii, kwa sababu hili suala lilikuwa la mwaka jana. Sasa Mhe. Waziri anihakikishie au serikali tu itoe tamko kwamba lini watakuwa tayari na kama kupitisha bajeti watakuwa tayari mimi nitakubali, lakini nataka kauli ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani kuna mambo mawili; kuna suala la kutengeneza mashine hicho chombo hicho ni suala moja, lakini kuna na fedha za uendeshaji ambayo ndio imo ndani ya bajeti. Kwa hivyo, nadhani wala hatujapingana hapo, tupitishe hii tuone tunafika wapi ili tuweze kulimaliza. Kwa hivyo Mhe. Raza wewe tulia, unaweza ukarudi tena kwa mchango huu

ambao unataka kutoa, lakini na bajeti hii itabidi tuipitishe kwa sababu chombo kikishatengenezwa kuna fedha za uendeshaji ambapo ndio wakati wake ni huu.

Sasa hapo tumemaliza Mhe. Raza wewe tusubiri bajeti hii ipite baadae nenda wizarani kama mchango huo wa kutengeneza hiyo mashine wataupokea sawa, lakini vyenginevyo wanaweza hata kutengeneza kutokana na vifungu vyao. Hiyo kwa mujibu wa waziri pale alivyosema ina maana hiyo. Haraka haraka nimsikilize Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi miongoni mwa waliochangia sikupata fursa ya kuchangia kwa maneno kutokana na muda na nilichangia kwa maandishi. Lakini ni miongoni mwa wale ambao hawakutajwa katika orodha ya Mhe. Waziri mimi na ndugu yangu Jaku.

Katika mchango wangu wa maandishi Mhe. Mwenyekiti, pia sijasikia hata ule ufafanuzi uliotolewa. Nilizungumzia kwanza niliipongeza serikali kwa jitihada inazozionesha katika kutengeneza barabara zetu za mjini na vijijini, lakini nilieleza masikitiko ya kutotengenezwa barabara za ndani ambazo zinaitwa *feeder roads* na nilizitaja. Nilitaja Biziredi-Misufini, Mwembeladu-Miti Ulaya, Gulioni-Mlandege na Weles inayotokezea Michenzani. Sasa nilitaka kumuuliza Mhe. Waziri anipe maelezo anisaidie namna wizara ilivyojiandaa katika kutengeneza barabara hizi baada ya kutengeneza barabara kuu sikupata maelezo yoyote.

Lakini katika hilo pia nilielezea jitihada ya serikali ambayo ilionesha kuwaondoshea kero wananchi wa Jimbo la Kwahani kwa kutengeneza barabara ya Jumapweza-Kwaalamsha na Mikunguni-Mwembenjugu. Lakini katika suala la barabara hizi pamoja na pongezi kwamba nilizungumza kuwa barabara ya Mikunguni/Mwembenjugu wakati ilipokuwa haipitiki ina mashimo ile barabara ilikuwa na matuta Mhe. Mwenyekiti, lakini baada ya kutengenezwa kwamba barabara ndio zinapitika kwa kasi zaidi yale matuta hayakurejeshwa, sasa nataka Mhe. Waziri anisaidie kwa sababu tangu barabara ile imetengenezwa Mhe. Mwenyekiti, idadi ya vifo vilivyotokea vingi katika Wilaya ya Mjini basi vimetokea katika barabara ile, na naamini kwamba ajali nyingi zikitokea kanda ya mjini basi zimetokea katika barabara ile ya Mikunguni - Mwembenjugu. Naomba maelezo zaidi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi. Aidha, katika *concern* ya Mhe. Mjumbe alizungumzia barabara tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe zikibakia dakika kumi tunapitisha vifungu tu moja kwa moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mheshimiwa alizungumzia barabara tatu, barabara ya kwanza aliyozungumza ilikuwa ni barabara ya Misufini ambazo katika majibu yetu ya msingi tulieleza kwamba barabara hizi zote kwa ujumla tutazungumza na wenzetu wa Halmashauri kwa maana ya kwamba Manispaa ya Mji wa Zanzibar tuweze kuona namna gani tunaweza kutengeneza. Barabara ya Weles tumeeleza katika kitabu chetu cha bajeti kwamba tutaijenga katika mwaka huu.

Lakini suala la matuta nimhakikishie Mheshimiwa kwamba tutawaomba wenzetu wa Bodi ya Usafiri na Leseni wakae, kwa sababu wao ndio wenye mamlaka kisheria waone kama maeneo haya yanastahiki kuwekwa matuta watatuletea wizarani na sisi tuchukue hatua zinazostahiki.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, kidogo tu, maelezo si mabaya, lakini hoja yangu ya msingi iko hapa, ndugu yangu Mhe. Naibu Waziri nilichozungumza kabla ya barabara hii haijafanyiwa marekebisho ilikuwa ina matuta na iliombwa kwa taratibu hizo za kisheria, lakini baada ya ukarabati na kutengenezwa barabara mpya yale matuta ndio hayakurejeshwa, pamoja na jitihada za masheha wangu, madiwani kufuata taratibu za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti: Maelezo haya ni ya mwisho sasa tunapitisha vifungu moja kwa moja ndio ile niliyotoa maelezo kabla.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nadhani *concern* ya kaka yangu nimeielewa, nilichomuelekeza kwamba ni utaratibu. Bodi ya Usafiri ndio yenye Mamlaka, bodi itakaa ikijiridhisha inawezekana ikawa hapo mwanzo matuta yaliwekwa kinyume na utaratibu. Kwa hivyo, utaratibu itakapokuwa imekaa bodi wakituletea wizara hatuna pingamizi matuta yatawekwa, lakini lazima kikao cha bodi kikae kitoe maamuzi kwa mujibu wa taratibu za sheria.

Kifungu0701Idaraya Ujenzi na Utunzaji Barabara	250,000,000
Kifungu 0801 Idara ya Usafiri na Leseni	300,000,000
Kifungu 0901 Idara ya Uendeshaji na Utumishi	2,583,400,000
Kifungu 0902 Mamlaka ya Usafiri Baharini	238,000,000
Kifungu 1001 Idara ya Mawasiliano	255,600,000
Jumla ya Fungu	**5,192,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba	15,794,368,000
Kifungu 0401 Idara na Mipango na Sera	32,501,644,000
Jumla ya Fungu	**64,056,012,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe maana ya kitanzi maana hiki leo ni kitanzi, na kitanzi huja wakati huo hukumu zote zimekwisha mpaka Mahkama ya juu kabisa. Sasa tulitoa mwanya tu kidogo ili kusikiliza maelezo ya hapa na pale, lakini kimsingi ilikuwa tunakwenda kwenye vifungu moja kwa moja. Sasa tuelewe hilo jambo ambalo huko siku za usoni tutazingatia ndani ya kanuni.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko au pamoja na mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na makadirio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi kukushukuruni kumaliza shughuli hii leo, na kwa kuwa hatukuwahi kuanza ile shughuli ya Wizara ya Fedha basi ule umuhimu wa kuja kesho upo kama tulivyokubaliana katika hoja ya awali aliyotoa Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa maana hiyo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 04/08/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 9:31 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 04/08/2013 saa 3:00 asubuhi)